## ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

## MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu. |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani. |

| | |
|---|---|
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |

| | |
|---|---|
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake. |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh’d Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |

| | |
|---|---|
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |

| | |
|---|---|
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni |
| 74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 76.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 78.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 79.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Sita - Tarehe 29 Oktoba, 2014**

*(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 62**

**Kujengwa Sehemu ya Mazoezi ya Viungo *(GYM)* katika Eneo la Baraza la Wawakilishi**

**Mhe. Saleh Nassor Juma** - Aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la maradhi yasiyokuwa ya kuambukiza *(NCD)* kwa watu wa rika na kada zote wakiwemo viongozi, wafanyabiashara, watumishi wa umma pamoja na wananchi wengine. Kwa kuwa mazoezi ya viungo ni moja kati ya tiba ya maradhi haya na hivyo wananchi kushauriwa kuwa na ratiba ya kufanya mazoezi kila siku. Kwa ushauri huu Mabunge mengi yakiwemo ya Barani Afrika hujenga maeneo maalum kwa ajili ya kufanyia mazoezi Wabunge wake *(GYM)*, kwa kuwa hapo awali iliwahi kuelezwa kuwa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar limedhamiria kujenga *GYM*.

Je, dhamira ile ipo pale pale au kuna mabadiliko.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 62, lakini kabla ya kumjibu swali lake naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli inaelezwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la maradhi yasiyokuwa ya kuambukiza *(NCD)* kwa watu wa rika na kada zote wakiwemo viongozi, wafanyabiashara, watumishi wa umma pamoja na wananchi wengine. Aidha, mazoezi ya viungo ni moja kati ya tiba muhimu ya maradhi haya na hivyo wananchi kushauriwa kuwa na ratiba ya kufanya mazoezi kila siku ni jambo la msingi.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali lake Nam. 62 kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kwa sasa imejipanga kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mingi ya kimaendeleo, ikiwemo matengenezo mbali mbali ya jengo la Baraza ili kuimarisha utoaji wa huduma. Pia, Baraza kwa sasa lina dhamira ya ujenzi wa *mini press, hostel*, maktaba, ofisi zaidi za watumishi na viongozi wa Baraza.

Mhe. Spika, kutokana na gharama kubwa za miradi hiyo iliyotajwa haitakuwa rahisi kushughulikia miradi hiyo yote kwa wakati mmoja. Hata hivyo, Baraza litatekeleza miradi hiyo kadiri fedha zitakavyopatikana. Baada ya kukamilsha miradi hiyo, Baraza litafikiria kujenga *GYM* ili Waheshimiwa Wajumbe, wapate sehemu ya kufanya mazoezi kwa ajili ya kujenga afya zao.

Mhe. Spika, ili kujikinga na maradhi hayo kwa wakati huu ambapo *GYM* ya Baraza haijakuwa tayari, Waheshimiwa Wajumbe, wanaweza kutumia fursa za kujiunga na klabu mbali mbali za mazoezi ya viungo na vile vile, kushiriki kikamilifu kwenye mazoezi ya timu ya Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kujenga afya zao.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, maarufu muasisi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo kwa pamoja.

Mhe. Spika, kama nilivyosema awali sisi ndani ya Baraza la Wawakilishi tunaona umuhimu mkubwa wa kuwa na *GYM* kwa ajili ya viongozi wetu na kwa kweli ameeleza sana athari za kufanya mazoezi njiani njiani kwa wakati wa leo sasa. Lakini nilivyomuelekeza katika suala la msingi kwamba yapo maeneo mazuri ya kufanya mazoezi na ukawa salama, lakini kwa sababu kupanga ni kuchagua na hichi chombo cha Wawakilishi na shauri la Wawakilishi siku zote ndio linalotizamwa kama dira ya kuendesha chombo hichi. Kwa hivyo, ushauri wake tunaupokea tunakwenda kuufanyia kazi na Ofisi ya Baraza tuone namna gani tunaweza kufikia uamuzi mzuri kuhusu jambo hili muhimu kwa maisha ya viongozi wetu wa Baraza hili.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. waziri na amekuwa hodari wa kupokea tu na sijui lini ataanza kuyafanyia kazi kuyatatua masuala mengi anayopokea kwenye kipindi hichi. Nimuulize swali moja dogo sana la nyongeza.

Mhe. Spika, chini ya Baraza la Wawakilishi kama ni ofisi yake imesaidia kiasi gani au mchango gani na nani aliyemkabidhi katika timu ya Baraza la

Wawakilishi ili tupate kujua kuwa timu ya Baraza la Wawakilishi ina viongozi. Nini anachosaidia katika timu ya Baraza la Wawakilishi ya mpira wa miguu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, ijapokuwa sikumsikia vizuri, lakini nafikiria hivyo alivyosema pengine nimefahamu.

Mhe. Spika, na muhimu sana tunaposema tuelekeze kwenye hivi vipaza sauti vyetu kwa sababu ya kusikikana vizuri. Kwanza ningependa Mhe. Mwakilishi, aamini kwamba tunayoyasema hapa nia na dhamira yetu ni kuyatekeleza vizuri. Unapokuwa *negative* na mwenzako ana nia njema, inakuwa inaonesha wewe huna dhamira kwa sababu mwenye dhamira njema humfikia mwenzake kufanya wema.

Hata kidini unapokuwa na dhamira njema ya kufanya jambo jema, unapata thawabu kabla ya kulifanya na unapokuwa na nia mbaya ukataka kufanya jambo baya, basi unapata dhambi pale unapoanza kulifanya. Kwa hivyo, naomba aungane mkono kwamba nia na dhamira yetu ni njema kufanya shughuli hizi ziende vizuri kwa manufaa yetu wote Wajumbe na wananchi kwa jumla.

Mhe. Spika, lile swali la pili, sikulisikia vizuri, ningeomba alirudie.

**Mhe. Spika:** Rudia swali la pili Mhe. Jaku.

**Mjumbe Fulani:**Washa *speaker*.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Nishawasha ndugu Issa. *(Kicheko)*

Mhe. Spika, tokea kuwepo kwa timu ya Baraza la Wawakilishi Mhe. waziri, umesaidia nini timu ya Baraza la Wawakilishi, ndio swali langu hapo, kote huko sikuuliza wala mimi sikutaka kujizonga huko, ilikuwa ni swali dogo na jepesi. Tokea kuwepo kwa timu ya mpira wa miguu ya Baraza la Wawakilishi, Ofisi yako imesaidia nini, sikutaka kote huko ulivyojibu Mhe. waziri.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, sasa nimemuelewa Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Kama nilivyosema dhamira yangu njema peke yake ni mchango mkubwa katika kusaidia timu yetu, lakini nashiriki kikamilifu kwenye mipango, mikakati, mawazo mbali mbali kwa ajili ya kuimarisha timu yetu ya Baraza. Ukiliona jambo linakwenda vizuri jengo hili la Baraza basi ujue na Mohammed Aboud yumo ndani, maana ndiye waziri anayesimamia shughuli za Baraza. *(Makofi)*

**Nam. 28**

**Waandishi wa Habari wa Zanzibar Kutonufaika na Ziara za Nje za Rais Kikwete**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza:-

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa muda mrefu amekuwa na utaratibu wa kuchukua waandishi wa habari wa vyombo vya habari vya Serikali na binafsi na kuambatana nao katika safari zake za nje ya nchi, lakini hali hiyo haipo kwa upande wetu na wala waandishi kutoka Zanzibar hawapati fursa ya kuambatana na Mhe. Rais katika safari kama hizo.

a) Je, kwa nini waandishi wa habari kutoka Zanzibar wamekuwa wakitengwa katika ziara hizo wakati na wao ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

b) Kitendo cha kutochukuliwa waandishi wa habari kutoka Zanzibar katika ziara hizo, sio kuwanyima haki wananchi wa Zanzibar ya kupata taarifa za kiongozi wao kwa wakati kupitia vyombo vya habari vya *ZBC*.

c) Kwa kuwa utaratibu wa kuchukua waandishi wa habari umekuwa na tija kubwa kwa Serikali na wananchi kuweza kupokea taarifa za viongozi wao wakiwa safarini kwa wakati, SMZ ina mpango gani kwa Rais wa Zanzibar kuwa na mpango wa kuchukua waandishi wa habari katika ziara zake za nje.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 28 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza nataka kutoa maelezo kabla ya kulijibu swali lenyewe. Katika muundo wa Ofisi ya Rais kuna Ofisi ya Faragha ambayo hujumuisha vitengo mbali mbali kikiwemo cha Mawasiliano na Habari. Ndani ya kitengo hichi umo uandishi wa habari, wapiga picha na watayarishaji vipindi ambao walitoka taasisi mbali mbali za habari. Watendaji hawa ndio wenye jukumu la kutangaza taarifa zote za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi. Baada ya kutoa ufafanuzi huo sasa naomba kujibu swali hili kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, waandishi wa habari wa Zanzibar hawatengwi kwa kutokuchukuliwa kwenye ziara ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nje ya nchi. Mhe. Rais anapofanya ziara hizo hutegemea kitengo chake cha mawasiliano kilichopo Ikulu. Hata hivyo, ikiwa kuna chombo cha habari kinataka kushiriki katika safari hizo hakizuiliwi kufanya hivyo iwapo kitajigharamia wenyewe. Mhe. Spika, baadhi ya vyombo vya habari vya Tanzania Bara katika safari za Mhe.Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

b) Si kweli kwamba kitendo cha kutokuchuliwa waandishi wa habari kutoka vyombo vya habari vya Zanzibar katika ziara ya nje ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kunawanyima wananchi haki ya kupata taarifa za kiongozi wao kwa wakati kwani waandishi wanapofuatana na Rais kutoka Kitengo cha Mawasiliano Ikulu wanatuma taarifa mbali mbali nje ya nchi na kwenye vyombo vya habari vya ndani.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, tokea jana ya kusikitisha. Nilichouliza na swali linajiuliza, sikuuliza swali langu la msingi sikuuliza Kitengo cha Ikulu wala Faragha. Swali langu kwa nini vyombo vya habari havichukuliwi katika safari ya nje na Mhe. Rais, ndio swali langu. Sikutaja suala la faragha wala Ofisi kutoka Ikulu, swali langu la msingi aliangalie nilivyouliza.

**Mhe. Spika:** Sasa moja kati ya sababu ya kutokuchukuliwa ni kwamba Marais wetu hawa huwa wanategemea Kitengo cha Mawasiliano katika Ofisi zao. Kwa hivyo, kimsingi masuala ya habari na kila kitu wanafanya Kitengo hicho cha Mawasiliano kwa upande wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pia, kwa upande wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hiyo ndio sababu yenyewe.

Ila anasema hawazuiliwi kama wataomba kuingia katika msafara huo na watafanya utaratibu wa kujilipia. Sasa naona na majibu yapo mazuri. Wewe yamekusikitisha, lakini nadhani mazuri. Kama una la nyongeza uliza. Huna Mhe. Shadya Mohamed Suleiman.

**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman:** Mhe. Spika, ahsante sana kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali moja la nyongeza lenye sehemu (a) na (b).

a) Mhe. Spika, Maafisa wa Habari wanatoka katika taasisi gani katika wizara yako.

b) Je, kwenye mikoa na wilaya wapo maafisa wa habari.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, maswali yake mawili kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwenye swali la msingi ni kweli Wizara ya Habari na Taasisi zake tisa ikiwemo habari, maelezo na kwenye mikoa na wilaya tunao maafisa wetu wa habari na tunao ambao wanakuwa na vyombo vya *TV* na habari na mawasiliano.

Mhe. Spika, nakushukuru.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi asubuhi ya leo kuweza kunipa niweze kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Spika, katika kuliingilia suala hili kumsaidia Mhe. Jaku, ulisema neno la kusema kuwa wanaweza kuomba. Je, Mhe. Naibu Waziri, wataombaje safari wakati wao hawajaalikwa. Lakini pili, wenzetu kule utakuta *TBC* kama juzi walikuwepo China na wakawa wanatuonesha jinsi gani Rais anavyotembelea sehemu mbali mbali.

Mhe. Spika, je, huoni kuwa hichi ni chombo ambacho cha Serikali na kinawaelimisha wananchi jinsi gani Rais anapokwenda nje? Je, kutokuwachukua hamuoni kama munawanyima haki?

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, nakushukuru na naomba Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kama jibu la msingi ambalo Mhe. Naibu Waziri, amejibu na ambalo umelitia nguvu ni kwamba ziara za viongozi wetu huwa sio siri, zinatangazwa kabla na vyombo mbali mbali vya habari kwamba mfano Rais wa Zanzibar atakuwa na ziara ya nchi fulani fulani kabla. Kwa hivyo, yeye mwenyewe kama ulivyosema ni kwamba kuna Kitengo cha Mawasiliano

Ikulu ambacho kimsingi ndio chenye jukumu la kuhakikisha kwamba taarifa mbali mbali za habari zinazomuhusu Mhe. Rais zinatangazwa zinapelekwa kwa vyombo vya habari kwa ajili ya kutangazwa. Hilo ndio jukumu lao na ndio wapo pale kwa ajili hiyo.

Mhe. Spika, ila kama kuna chombo chochote cha habari kina hamu *(interest)* ya kuwaambatana na viongozi wetu, basi wakishapata habari kwamba mfano Rais wa Zanzibar anakwenda mfano Vietnam basi wanawasiliana na Kitengo cha Habari Ikulu na wao wanakuwa ni sehemu ya ziara ile, isipokuwa ni lazima wajilipie gharama za safari yenyewe, wao tu watakuwa ni sehemu ya msafara ule wa Mhe. Rais, lakini gharama zenyewe zitabebwa na chombo chenyewe.

Kwa hivyo, kama *TBC* wameonekana China ayumkini wameomba kwa Idara ya Habari ya Mawasiliano Ikulu ya Jamhuri ya Muungano wameruhusiwa na wamejilipia. Kwa hivyo, hilo sio jambo geni, ni jambo la kawaida kwa vyombo vyote vya habari ambavyo vinataka kuambatana na viongozi wa nchi zao. *CNN* wanafanya hivyo na *BBC* wanafanya hivyo, lakini sio kwamba wao ni sehemu ya msafara wa Rais.

**Nam. 73**

**Usumbufu Wanaopata Watalii Wanaopitia Uwanja wa Ndege**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza:-

Kuna tatizo kubwa katika kutangaza utalii nchini kwetu hasa baada ya usumbufu wanaopata watalii siku ya Jumatano ambayo mara nyingi ndege kubwa nne za watalii ambazo ni Meos, Meridian, Condor na Alitali huwasili. Watalii wengi wanaowasili kwa ndege hizo hupanga foleni kubwa kuelekea eneo la Uhamiaji ambapo baada ya kufika kwa wahusika wanaambiwa wakafanye malipo ya *Visa* benki ya *CRDB* eneo jengine na wakimaliza hutakiwa kupanga tena foleni upya na kuwasababishia usumbufu mkubwa.

(a) Kwa nini Serikali haitoi mwongozo sahihi utakaorahisisha kuondoa usumbufu huo hasa kwa kuwakutanisha wahusika wote kama vile Uhamiaji, Benki ya *CRDB*, wizara yenye kuhusika na utalii na mamlaka ya uwanja wa ndege.

(b) Je, utaratibu huo wa usumbufu ukiendelea kiwanjani hapo hautachangia kurejesha nyuma maendeleo ya sekta ya utalii huku jitihada kubwa zikifanyika kutangaza utalii wetu, hali ambayo inaonekana kama kutwanga maji kwenye kinu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake namba 73 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, naomba kutoa maelezo yafuatayo.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Serikali imeanzisha mfumo mpya wa ulipaji wa *Visa*, ambapo kwa sasa malipo hayo hufanywa kwa kupitia Benki ya *CRDB* badala ya kitengo au idara ya uhamiaji. Lengo kuu la Serikali ni kuhakikisha ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ambao hutumika katika kuleta maendeleo ya nchi kwa ujumla. Wakati wa utekekelezaji wa mfumo huo mpya, kumejitokeza changamoto ya mpangilio wa ulipaji wa *Visa* na ugongaji wa *Visa*, ambao unaonekana kuwaletea usumbufu wageni wanaowasili nchini.

Mhe. Spika, changamoto imejitokeza kutokana na ufinyu wa eneo la kuwasili abiria. Aidha, changamoto hiyo imechangiwa na;

1) Mfumo wa zamani wa kiuhamiaji, uliopo katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Aman Karume, unaotofautisha mfumo wa utambuzi wa madawa ya kulevya, yaani *antibiotic;*

2) Mfumo wa kipolisi wa Kimataifa, yaani *interpol;* na

3) Mfumo wa uhamiaji, yaani *migration*.

Mhe. Spika, kwa utaratibu huo kila mfumo unalazimika kuwa na kompyuta yake na afisa wake ndani ya chombo kimoja cha uhamiaji.Utaratibu wa sasa unaotumika duniani na hata katika Uwanja wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wa Dar es Salaam. Mifumo yote hiyo mitatu huunganishwa ndani ya kompyuta moja na hivyo ni Afisa mmoja tu hutumika kwa kufanya kazi hizo zote tatu.

Mhe. Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali kwa kupitia Wizara ya Fedha ilifanya mkutano na wadau wote, kutoka Benki ya *CRDB*, Mamlaka ya Shirika la Ndege ambapo pamoja na mambo mengine, changamoto hiyo ilizungumzwa kwa kina.

Kwa upande mwengine Wizara ya Habari, Utalii na Michezo ilifanya ziara rasmi katika Viwanja vya Ndege kuangalia na kukagua eneo la tukio. Aidha, Serikali ina lengo la kufanya mazungumzo na Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi, ili kuiunganisha mifumo hiyo mitatu katika mfumo mmoja na hivyo,

kutoa nafasi ya kuweka kibanda kipya cha *CRDB* pembeni ya kibanda cha uhamiaji na hivyo kurahisisha utoaji wa huduma.

Mhe. Spika, majibu;

(a) Serikali imeshazikutanisha taasisi zote husika kuona namna tulimaliza kadhia hiyo. Aidha, matarajio yetu jambo hili tunalichukulia uzito unaostahiki katika kulipatia ufumbuzi wa kudumu.

(b) Ni kweli kuwa utaratibu huu ukiendelea utachangia kurejesha nyuma juhudi kubwa ya Serikali za kuleta maendeleo ya sekta ya utalii. Naomba Baraza lako tukufu litambuwe kwamba wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani, kwamba tatizo hilo litapatiwa ufumbuzi muda mfupi ujao. Tayari wizara tumeshaanza kufanya mawasiliano na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana na ya kutia moyo ya Mhe. Naibu Waziri, Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chwaka ambaye panapo uhai asilimia 99 kurudi tena katika kipindi chake, kwa kazi nzuri aliyofanya kwa wananchi wake, naomba kumuuliza swali moja dogo tu la nyongeza.

Mhe. Spika, ni utafiti gani uliofanyika ikiwemo kutafuta uzoefu kabla ya utaratibu huo kufanyika, ili kuepusha usumbufu kama huo kutokea?

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, utafiti wa ulipaji wa *Visa* kwa njia ya kibenki, yaani kwa njia ya kadi. Ulifanyika hapa Tanzania kwa mara ya kwanza katika Uwanja wa *KIA*, yaani *Kilimanjaro International Airport*.

Pamoja na kasoro zilizojitokeza, madhumuni makubwa Serikali kuja na mfumo huu, ni kuona kwamba inadhibiti mapato yanayotokana na *Visa*. Mfumo huu sio mbaya, changamoto ziliopo ni eneo na namna ya ku-*set*. Tunaamini kwamba tukiweza ku-*set* vizuri, mfumo huu wa ulipaji wa kadi hauna tatizo kubwa. Changamoto inayotokea ni kwamba eneo letu ni finyu, linahitaji kuwa- *rearrange* upya ili tuweze kutoa huduma hii vizuri bila ya usumbufu kwa wale, lakini mapato yetu tuweze kuyadhibiti vizuri zaidi.

Hivi sasa kunajitokeza usumbufu mkubwa kutokana na watu kuwa wanakuja katika *que* mbili tofauti. Anapinda kwanza kwenda kulipa kwa ajili ya *Visa*, halafu arudi tena kwenye mstari kwa ajili ya kwenda kugongewa *Visa*. Jambo hili linaleta usumbufu kutokana na eneo letu dogo. Tunaamini kwamba

tukikaa pamoja, usumbufu huu hautojitokeza. Kwa hivyo, utafiti umeanzia katika Uwanja wa *Kilimanjaro International Airport* kule Kilimanjaro.

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi nimuulize swali dogo la nyongeza Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri, amesema kwamba fedha zile za *Visa* zinakusanywa kwa kupitia Benki ya *CRDB.* Swali langu Mhe. Naibu Waziri, nilikuwa nauliza ni kwa nini mkachagua Benki ya *CRDB* msichaguwe Benki ya Watu wa Zanzibar, kwa sababu fedha hizi ni za Wazanzibari?

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, naamini malengo ya Serikali ni kuona kwamba ufanisi ndiyo madhumuni makubwa. Benki hii ni sehemu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaamini kwamba kilichotumika ni kigezo na uwezo pamoja na uzoefu, ikibidi kwamba kuna haja ya Benki ya *PBZ,* Serikali haitosita kushirikiana na *PBZ* katika kutoa huduma hiyo. Tayari Serikali inashirikiana na *PBZ* katika maeneo tofauti katika kutoa huduma kama hizo.

Kwa hivyo, kigezo kikubwa naamini ni uzoefu na kwamba ndiyo tunaanza, ikifika wakati kwamba kuna ulazima wa *PBZ*, basi tutawachukua na wao watafanyakazi.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante Mhe. Spika na mimi naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali la nyongeza.

Mhe. Spika, nimesikitika sana baada ya kusikia jibu la Mhe. Naibu Waziri, kusema kuwa *PBZ* haina uwezo.

Mhe. Spika, hivi sasa *PBZ* imejitawala vizuri katika fani yake ya biashara mpaka Bara na imefikia lengo la ki-*international*. Hata *Visa card ATM* sasa hivi wanazo. Je, Mhe. Naibu Waziri, huoni kutumia lugha hiyo ni kuwaangusha hawa *PBZ* katika utendaji wao?

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, kwanza naomba Mhe. Mwakilishi, asinitilie maneno kinywani. Sijazema kwamba *PBZ* haina uwezo, sijasema neno hilo.

Nimesema *CRDB* ina uwezo na uzoefu katika mambo kama haya. Ninachokisema kwamba *PBZ* ni sehemu ya Wizara ya Fedha, wanaosimamia zoezi hili ni wao Wizara ya Fedha. Kwa hivyo, kama vigezo na uwezo wao wenzetu ndiyo waliozingatia zaidi.

Mhe. Spika, kauli yangu naamini sana uwezo wa *PBZ* na utendaji kazi wa *PBZ*. Kwenye hili wenyewe Wizara ya Fedha waliona uwezo wa ziada wa *CRDB* katika kutekeleza hili. *(Makofi)*

**Nam. 74**

**Makontena Uwanja wa Malindi na Mchangani**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub -** Aliuliza:-

Mhe. Spika, naomba tena Serikali itowe majibu ya swali namba 74 ambapo ni suala linalowakosesha usingizi wananchi wa Shehia ya Mchangani na Malindi na kwa kupitia chombo chao cha wananchi kupata jawabu muafaka hivi sasa.

Kwa kuwa Uwanja wa Malindi na Uwanja wa Mchangani ni miongoni mwa viwanja muhimu sana vinavyotumika kwa michezo kwa kipindi kirefu sana na kwa kuwa Serikali sasa imeamua kuhamisha makontena yaliyopo Bwawani, sasa yanahamishwa kupelekwa katika viwanja vya Malindi na Mchangani.

(a) Je, ni kweli kuwa makontena hayo yanapelekwa maeneo hayo.

(b) Kama ni kweli, je, Serikali haioni kuwa kufanya hivyo ni kuvunja haki za wanamichezo wanaotumia eneo hilo na kudumaza michezo hapa nchini.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake nambari 74, lenye vifungu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo.

Mhe. Spika, shirika la bandari limeruhusiwa na Serikali kulitumia eneo la Bwawani, ambalo lilifukiwa wakati wa mradi wa geti mpya ya Malindi mwaka 2005 hadi mwaka 2008, wakati ujenzi huo ukiendelea, kwa ajili ya kuwekea makontena matupu baada ya bandari kuzidiwa na idadi ya makontena. Eneo hilo ni muhimu sana kwa kazi ya ufanisi wa Bandari ya Malindi, kwani eneo la ndani ya bandari haliwezi tena kukidhi hali ya ongezeko kubwa la makontena yanayoingia kutoka nchi mbali mbali.

Mhe. Spika, shirika la bandari kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, imeiomba Serikali kuipatia eneo mbadala kwa ajili ya kuhifadhia makontena matupu, baada ya kutakiwa kuyahamisha makontena yote hapo Bwawani na kupisha mpango wa Serikali wa uendelezaji wa eneo hilo.

Mhe. Spika, hivi sasa Serikali inaendelea na mchakato wa kutafuta eneo mbadala kwa ajili hiyo, ambapo moja ya maeneo yaliyopendekezwa ni eneo la kiwanja cha Malindi, pamoja na maeneo mengine yaliyokaribu na bandari. Kazi hiyo bado inaendelea kwa kupitia Kamati maalum iliyoundwa na Serikali.

(a) Mhe. Spika, dhamira ya Serikali ni kuondoa usumbufu unaotokana na ufinyu wa eneo, katika eneo la bandari na kutafuta eneo muafaka litakalokidhi haja ya kuhudumia uwekaji wa makontena.

(b) Serikali watafanya kila jitihada kuona inaendeleza michezo nchini, wakiwemo vijana wa maeneo husika ya Malindi, Mchangani na Shehia nyengine zinazotumia uwanja huu.

(c) Sababu ya msingi ni ufinyu wa kuweka makontena matupu huko bandarini ambapo Serikali lazima kupata eneo muafaka lililokaribu na maeneo ya kibandari.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mdogo tu. Kwanza nafikiri atakubaliana na mimi kuwa shirika la bandari limeshindwa majukumu yake hivi sasa, ambalo halitaki hata tochi jambo hilo, hivi sasa tumeone usumbufu uliokuwepo pale, makontena kutolewa mchana yakafanya foleni kubwa, kutokea njia ya Gulioni Kinazini mpaka kule magari kusimama, sijui utaratibu ule ameuona wapi Mhe. Naibu Waziri, duniani kufanywa kazi wakati wa mchana. Gari moja kubeba kontena moja mpaka kwenda kumwaga Bwawani masaa sita, huku watu wakiwa wanateseka kuendelea kufanya kazi zao kwa utaratibu.

La pili, nafikiri yale makalbi mpaka leo yamekuwa ni usumbufu kwa wananchi ambayo ni moja katika majukumu ya shirika la bandari kushindwa. Sasa naomba kumuuliza swali.

Kwa kuwa Mji wa Zanzibar umekua na idadi ya watu inaongezeka, ni vigezo gani vimetumika kuamua makontena hayo kuweka katikati ya Mji na kushindwa kuweka kama ndugu zetu wa Dar es Salaam yako katika maeneo

ya nje ya bandari na *Airport* na kazi zinafanywa vizuri. Lini watakuwa tayari kwenda kujifundisha kazi kwa ndugu zetu wa Tanzania Bara. Hilo la kwanza.

Kwa kuwa eneo hilo ni la wazi na linatumika kwa maendeleo ya michezo na kituo cha daladala kilichowekwa kwa muda, hivi karibuni sasa kuanzisha *yard* ya kuhifadhi makontena. Hali hiyo ya mgongano katika sehemu moja huoni tunawasumbua wananchi wetu. Kwa hivi sasa pale pana kituo cha daladala, leo yanawekwa makontena na ujambazi unaweza ukazidi pale, pana benki pale. Sijui Serikali imeangalia vipi suala hilo?

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, kwanza naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi, kwamba mimi sikubaliani na maelezo yake kusema kwamba shirika la bandari limeshindwa kazi. Mimi naamini kwamba shirika la bandari linafanyakazi zake vizuri na zenye ufanisi, kitija, wafanyakazi, vifaa na maboresho mengine. Changamoto ni sehemu ya ufanisi wa kazi, kazi mafanikio yanavyokuja ndivyo changamoto zitakavyokuja na ubingwa wake ni kukabiliana na changamoto hizo na kuziondoa.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba ukiangalia kwa haraka unaweza ukaona kwamba kuna haja na ulazima wa kuwa na eneo jengine nje ya bandari kwa ajili ya kuhudumia uwekaji wa makontena matupu. Lakini maeneo mfano aliyotoa ya Dar es Salaam, tayari miundombinu ya barabara ilikuwa inaruhusu kuweza kuyatoa makontena bandarini kwenda katika maeneo haya. Kwa upande wetu bado barabara zetu hatujajenga kwa msingi huo wa kuweza kuchukua hilo.

Lakini la pili, barabara hizo zina upungufu wa uwezo wa kubeba mzigo kiasi hicho, lakini pia, zina upungufu wa wembamba kuweza kutoa huduma hiyo. Ukififikiri kwa haraka haraka makontena yale yataanza kutumika kwa barabara kuweza kwenda nje ya mji, tutegemee usumbufu mkubwa sana katika usafiri.

Lakini kubwa zaidi gharama ya kontena moja kulitoa bandarini kulipeleka eneo la pili na ukijua mzigo ule utamrudia tena mwananchi anayekuja kutumia huduma au bidhaa zinazokuwemo ndani ya makontena hayo.

Changamoto yetu kubwa ni ufinyu wa eneo katika eneo la bandari kwa ajili ya uwekaji wa makontena matupu. Eneo la Bwawani kwa wakati ambao lilikuwa likitumika, haikuwa kigezo cha ajabu kusema kwamba katikati ya mji. Maana mwanzo lilikuwa ni shimo ambalo linatuama maji, Serikali hii hii ndio iliyochukua mchanga wakati inajenga bandari, ikenda kufikia eneo lile na kuona kwamba ipo haja kutokana na ufinyu wa eneo lililokuwepo bandarini, kutumia eneo lile ambalo limefukiwa kwa ajili ya uwekaji wa makontena.

Suala la pili, kituo cha daladala. Tunaamini kwamba mipango ya matumizi mazuri ya mji, lengo ni kuwaondoshea usumbufu wananchi wetu. Kituo kile tunaamini kipo kwa muda ukifika wakati kitaondoka na kutafuta eneo jengine zuri, ili tuweze kuwa na huduma za usafiri katika mji wetu zinaimarika zaidi na wananchi wetu wanaondokana na usumbufu wowote unaojitokeza.

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi nimuulize Mhe. Naibu Waziri, swali moja dogo la nyongeza. Katika majibu yake alikuwa anaeleza kuhusu ufinyu wa uwekaji wa makontena. Sasa Mhe. Naibu Waziri, nilikuwa nataka kujua, hapo zamani kulikuwa na *yard* ya makontena kule Saateni ambayo mlikuwa mnahifadhia, *yard* ile hivi sasa haitumiki sijui ni kwa sababu gani?

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, ni kweli Saateni tulikuwa tuna eneo ambalo lilitumika kwa ajili ya uwekaji wa makontena. Lakini eneo lile limeonekana kwamba ni dogo haliwezi kukidhi idadi kubwa ya makontena. Mipango ya Serikali ni kutafuta eneo ambalo litaweza kukidhi idadi kubwa ya makontena kukaa sehemu moja. Eneo lile la Saateni ukiweka makontena yakitimia 100, hata uwezo wa gari kuzunguruka unakuwa haupo.

Tayari Serikali tumekwenda kulikagua eneo hilo na tumeona ufinyu wa eneo hilo kwamba halikidhi na halitoshi kwa ajili ya uwekaji wa makontena, kama vile mipango ya Serikali kutafuta eneo litakaloweza kukidhi kwa ajili ya huduma ya uwekaji wa makontena matupu yanayotoka eneo la bandarini.Lakini pia, miundombinu kwa maana kwamba barabara husika nalo pia ni kikwazo kwa ajili ya makontena kufika katika eneo ambalo umelisema la Saateni.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nataka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, pamoja na majibu yake mazuri sana kabisa. Lakini linalonisikitisha ni kwamba mara nyingi sana tunafanya mambo bila ya kufanya *feasibility study* ili kuokoa fedha za wananchi.

Je, Mhe. Naibu Waziri, mwenye maneno matatu, hamuoni kufanya vile ni kupoteza pesa wa wananchi, bila ya kuwa na malengo ya kuendeleza lile eneo vizuri.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, samahani huku mwisho sikumpata vizuri, eneo lipi uliokuwa unakusudia la Bwawani au la Saateni?

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Eneo la Saateni mule ndani, ndiyo ninalolizungumzia sasa hivi hapa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, majibu ni kwamba kama wote tunavyoshuhudia mfumo wa usafiri duniani umebadilika, zamani mizigo ilikuwa inakuja katika mfumo ambao ni nje ya makasha.

Hivi sasa takribani kila siku zinavyokwenda ndivyo mzigo unavyokuja katika mfumo wa makasha, kwa maana ya kwamba ni makontena. Kwa hiyo, kama juzi na juzi eneo lile lingeweza kukidhi, lakini hivi sasa kutokana na idadi ya makotena yanavyokuja nchini eneo lile haliwezi kukidhi.

Kwa maana hiyo, kama *study* ilifanyika wakati ule, sawa ilikuwa ni sawa sawa, lakini hivi sasa kulingana na idadi ya makotena yanavyokuja kutokana na mfumo wa usafirishaji ulivyobadilika, eneo lile haliwezi kukidhi, isipokuwa lazima Serikali itafute eneo jengine kubwa pana litakaloweza kukidhi mahitaji ya uwekaji wa makontena matupu.

**Mhe. Spika:** Nakushukuru Mhe. Naibu Waziri. Tunaendelea.

**Nam. 82**

**Hospitali ya Wagonjwa wa Afya ya Akili Pemba**

**Mhe. Mussa Ali Hassan -** Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imekuwa na juhudi kubwa za kueneza huduma za afya katika maeneo yote ya Unguja na Pemba. Kwa kuwa kwa upande wa Unguja Serikali imeweza kujenga Hospitali ya Wagonjwa wa Afya ya Akili, iliyopo Kidongochekundu ambayo inasaidia kupatikana huduma hiyo kwa wananchi. Kwa kuwa upande wa kisiwa cha Pemba, wapo wananchi wanaohitaji huduma kama hiyo.

(a) Je, kwa upande wa Pemba ipo Hospitali ya Wagonjwa wa Afya ya Akili kama ile iliyopo Kidongochekundu mjini Unguja.

(b) Kama hakuna, Serikali ina mpango gani wa kujenga hospitali kama hiyo, ili huduma hiyo iweze kupatikana kwa wananchi wa Pemba.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia wote

tukiwa wenye afya na uzima na kuja kuwatumikia wananchi wa Zanzibar katika majukumu yetu ya kuliendeleza Taifa.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mjumbe, swali lake Nambari 82 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwanza kabisa ni ukweli usiofichika kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi mahiri na wa uadilifu wa Dkt. Ali Mohammed Shein (Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi), inaendelea na juhudi zake kubwa za kueneza huduma za afya katika maeneo yote ya Unguja na Pemba. Vile vile, kujali afya za wananchi wake kwa kuwasogezea huduma za afya katika maeneo ya karibu na wanakokaa.

Hivyo, naomba kumjuilisha Mhe. Mwakilishi, kuwa wodi ya wagonjwa wa afya ya akili ipo katika eneo la Hospitali ya Wete Pemba, jambo ambalo ni faraja kubwa kwa upande wa Pemba. Wodi hiyo hivi sasa ina uwezo wa kuwahudumia wagonjwa wapatao 20 kwa mara moja na wagonjwa wanaendelea kupata huduma kama ipasavyo katika hospitali hiyo.

Mhe. Spika, hadi jana jioni wodi hiyo ilikuwa na wagonjwa wanane tu ambao wanaendelea kupatiwa huduma ya matibabu. Ahsante sana.

**Mhe. Mussa Ali Hassan:** Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Kwa kweli si mara nyingi hospitali ya wagonjwa wa akili kuchanganywa na hospitali kuu katika nchi yetu. Sasa kwa nini hospitali hii imechanganywa pamoja na hospitali ya watu wambao hawana maradhi haya.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Spika, kutokana na ufinyu wa nafasi iliopo Pemba hakuna hospitali maalum ambayo imetengwa kwa ajili ya wagonjwa wa akili. Hivyo, kuna wodi ambao imetengwa hivi sasa katika Hospitali ya Wete ambayo itakuwa inaweza kushughulikia wagonjwa hao wenye matatizo ya akili.

Vile vile, katika hospitali inayojengwa mkoani kuna eneo maalum ya Abdalla Mzee, yaani kuna eneo maalum ambalo limetengwa na litakuwa kando ya hospitali, ambayo itakuwa ni kama wodi pia na wala sio Hospitali Maalum ya wagonjwa wa akili, isipokuwa ni kama wodi.

Mhe. Spika, la tatu, kwa Pemba pamoja na takwimu zote tulizozipata kutoka Pemba bahati nzuri wagonjwa wa akili sio tatizo kubwa kwa Pemba ni wachache. Hivyo, kwa takwimu za wodi hawajawahi kuzidi kupindukia wagonjwa 10 au 12 maisha wako chini ya wagonjwa 10.

Kwa maana hiyo, tunaweza kukidhi mahitaji yao kupitia wodi hiyo na wodi hiyo tayari imeshatengewa huduma zote pamoja na *restriction area,* yaani kutowaruhusu kutoka eneo moja kwenda eneo jengine la hospitali. Ahsante.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, ambaye ni mwanangu Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa *psychitric ward* ni *too exclusive* kutokana na kwamba wagonjwa wake ni wa aina yake. Kutokana na kwamba nchi nyingi za Jumuiya ya Madola hujenga wadi za wagonjwa wa akili mbali kabisa na wadi ya wagonjwa wa kawaida, ili kukimbiza zahama na kitahanani inayoweza kutokezea kwa wagonjwa wale pale ambapo wamechanganywa na wagonjwa wa kawaida.

(a) Je, haoni Mhe. Waziri, kujenga *psychitric ward,* yaani wadi ya wagonjwa wa akili ndani ya Hospitali ya Wete, badala ya kuitenga na hospitali ile ni kupeleka usumbufu kwa wagonjwa wa kawaida badala ya kuwapa huduma, isipokuwa ni kuendelea kuwadhalilisha zaidi wale wagonjwa wa kawaida.

(b) Mhe. Spika, anasema Mhe. Naibu Waziri, kwamba wagonjwa Pemba ni wachache hawazidi 10. Kwa kweli, hii ni kutokana tu kwamba wagonjwa wa Pemba wanapopata tatizo la kichaa huletwa Hospitali ya wagonjwa wa akili Kidongochekundu.

Je, haoni hicho kiji-*ward* wanachokijenga hapo Pemba hakitatosha kuwahudumia wagonjwa wa akili wa Pemba, kitajaa haraka na hatimaye itabidi kazi ile ile ya kuhamisha kuwaleta Unguja ifanyike tena. Sasa, je, isingekuwa vyema kujenga hasa Hospitali ya wagonjwa wa akili katika eneo fulani kule Pemba, badala ya kujenga hicho ki-*ward* kidogo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kuanzia mwisho huku, *that is* (b) na halafu nitakuja (a).

Mhe. Spika, hatutegemei kwa upande wa Pemba takwimu zote zinaonesha kwamba hatutegemei kuongezeka kwa wagonjwa wa akili, kwa sababu kuna *sources* mbali mbali za wagonjwa wanaotokana na ugonjwa wa akili hata malaria inasababisha ugonjwa wa akili pale inapopanda kichwani. Kwa hiyo, takwimu zote za kipindi hiki cha nyuma hatutegemei ongezeko.

Kwa maana hiyo, tunadhani nguvu za wizara pamoja na Serikali zisielekezwe huko, isipokuwa zielekezwe zaidi katika kujaribu kukinga yale maradhi ambayo tunategemea kutokea. Hivi sasa tunatumia nguvu pamoja na fedha nyingi kujitayarisha na Mwenyezi Mungu atuepushie mbali kama *Ebola* itatokezea hapa Zanzibar na ndio maana tunaweka mifumo mikubwa ya kukinga na hata njia za kuingilia wageni pia zinatazamwa. Hivyo, hilo hatulitegemei. Kutokana na hali hiyo, sio rahisi kuanza ku-*invest* kwenye Hospitali ya wagonjwa wa akili hatulitegemei hilo.

Pili, naomba nimjibu Mheshimiwa Mjumbe, kwamba teknolojia imeendelea sasa na pia teknolojia ya afya imeendelea. Kwa kweli, wagonjwa wa akili hivi sasa sio kama ilivyokuwa zamani *egration*, yaani kule kuwa na nguvu ya kutaka kupigana au kupiga makelele ama kuwakera wagonjwa wengine inadhibitiwa kwa mifumo ya kisasa ya teknolojia iliyoendelea kwenye dawa.

Kwa mfano, kuna mambo ya *sedation* ya kumtuliza mgonjwa, pia kuna mambo ya *peridose* ya kumfanya awe mtulivu, kuna madawa mbali mbali ambayo wagonjwa wanapatiwa kutokana na teknolojia ya sasa. Kwa hiyo, si kero wao hata wadi yao ikiwemo mule ndani sio kero tena kwa wagonjwa wengine na huwa wanatengewa nafasi zao maalum. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hata ukienda pale Muhimbili Dar-es-Salaam ambayo ndio Hospitali Kuu ya Rufaa Tanzania nzima, utakuta kuna *ward ya psychitric* kule pembeni mwisho kabisa baada ya Mwaisela na Kibasila ukeshapita kule pembeni utakuta *ward ya psychitric* ipo pale imetengwa iko pembeni na haileti matatizo yoyote.

Mhe. Spika, lakini katika swali lake la awali mpaka hivi sasa nimesema wagonjwa 10. Nilichokisema sio kwamba hakuna wagonjwa, isipokuwa nimesema *at a time average* ni wagonjwa 10. Sasa haileti maana kubwa kwamba kuchukua fedha zote za Serikali kwa ajili ya kwenda ku-*invest* katika hospitali maalum ya wagonjwa kama hao ambao idadi yake iko chini na wala hakuna ishara yoyote ya idadi hiyo kukua, kwa sababu magonjwa yanayosababisha magonjwa ya akili yanaendelea kupungua siku hadi siku.

Lakini la mwisho kabisa tumejaribu kufuatilia kwamba hakuna *cases* nyingi za kutoa wagonjwa kutoka Pemba na kuwaleta Hospitali ya wagonjwa wa akili Kidongochekundu mpaka hivi sasa hakuna, yaani hakuna *case* kama hiyo. Kwa hivyo, *cases* zote zimeweza kuwa *managed* huko Pemba na zimeweza kutatuliwa huko Pemba. Hata hivyo, wagonjwa ambao wanasema wanawa-*discharge,* ni *almost* wawili mpaka watatu kila baada ya mwezi ipo katika wastani huo. Ahsante.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Nampongeza sana Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri na anavyoweza kuyafafanua kwa vizuri na tukaweza kuyafahamu. *(Makofi)*

Lakini naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, alisema kwamba Pemba kuna wagonjwa kiasi 8 mpaka 10. Je, kwa utafiti wako Unguja kuna wagonjwa wangapi wanaozidi idadi hiyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante Mhe. Spika, nimesema kwa wastani *at a time* wanakuwepo wagonjwa bati ya 8 hadi 10 na nimesema wadi hiyo ina uwezo wa kuchukua wagonjwa hadi 20. Sasa haijapatapo, naomba kuzungumza kwa lugha hiyo hivi sasa, kwamba haijapatapo wadi hiyo kujaa. Kwa hiyo, tatizo hili sio kubwa kwa upande wa Pemba kama vile ukilinganisha na matatizo mengine ikiwemo kichocho na kadhalika, yaani haijapatapo wadi hiyo kujaa.

Pili, kwa Unguja tatizo hilo kubwa kabisa linasababishwa na madawa ya kulevya. Kwa hiyo, tatizo la madawa ya kulevya pamoja na mambo mengine haya kama vile bangi na kadhalika liko zaidi Unguja kuliko Pemba.

Mhe. Spika, *source* kubwa ya matatizo haya ya akili kwa hapa Unguja linatokana na mambo hayo. Kwa wastani hospitali ya wagonjwa wa akili Kidongochekundu inakuwa na wagonjwa kati ya 40 mpaka 50. Ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Nashukuru, tunaendelea na swali linalofuata, Mhe. Mussa Ali Hassan.

**Nam. 83**

**Wauguzi Kuvaa Beji zenye Majina yao**

**Mhe. Mussa Ali Hassan -** Aliuliza:-

Kwa kuwa moja ya kada muhimu katika hospitali zetu na vituo vya afya ni ile ya wauguzi, ambao utendaji kazi wa wauguzi hao ni wa heshima na uliotukuka kwa vile wanashughulika kutengeneza afya za wananchi pale zinapokuwa na matatizo. Vile vile, wahudumu wetu wanapokuwa wanafanyakazi ya kutoa huduma huwa hawana utambulisho kwa wagonjwa wanaowapa huduma, kama vile kuvaa beji maalum inayoonesha jina la muuguzi anayemhudumia mgonjwa.

Kwa nini wauguzi wetu wasiekewe utaratibu wa kisheria au kanuni za sheria ya kuwataka wavae beji maalum zenye majina yao, ili wagonjwa wanaowapatia huduma wajue na kuwafahamu muuguzi anayewapatia huduma kwa wakati ule.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 83 lenye kifungu kimoja tu (a).

Mhe. Spika, ni kweli kabisa kwamba kuna umuhimu mkubwa kwa wauguzi wetu wa hospitali zetu kuvaa beji za utambulisho zenye kuonesha jina la muuguzi, cheo chake, kazi yake pamoja na picha yake.

Hali hii itamuwezesha mgonjwa kumjua na kumtambua muuguzi aliyemhudumia na kumuwezesha kujenga uhusiano mzuri baina yao au pale panapotokezea mapungufu yoyote basi kuweza kumtambua au kujua namna ya kuripoti tatizo hilo husika, kwa ajili ya kuweza kushughulikiwa haraka iwezekanavyo.

Mhe. Spika, kwa hivi sasa Hospitali ya Mnazimmoja haina vitambulisho kwa wafanyakazi wake wote. Kwa hivyo, tumo mbioni kukamilisha zoezi hilo kwa wizara nzima na sio wauguzi tu, lakini ni wizara nzima pamoja na wafanyakazi wake wote Unguja na Pemba. Kwa kweli, tayari mazungumzo hayo yameshaanza na yamefikia hatua nzuri na kampuni ambazo zinazalisha vitambulisho pamoja na chombo cha Serikali.

Hivi karibuni wakati wa Mswada wa Sheria ya Kuunda Baraza la Wauguzi na Wakunga uliopitishwa hapa katika Baraza lako tukufu, pia kifungu hicho cha sheria kipo kwa upande wa wauguzi na baada ya kusainiwa tu na Mhe. Rais sheria hiyo na kuundwa kwa Baraza hilo, basi litakuwa na nguvu zaidi ya kuweza kutoa vitambulisho kwa wauguzi wetu. Ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Mhe. Mussa Ali Hassan, swali la nyongeza.

**Mhe. Mussa Ali Hassan:** Ahsante Mhe. Spika, pamoja na maneno mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwa vile katika wizara ama mahoteli makubwa huwekwa *boxes* za kutiwa maoni ya wananchi aina mbili; mazuri na mabaya, yaani anayesifiwa sana kwa utendaji wake bora ama mtendaji mzuri kuliko wote, kwa utamaduni wetu mzuri basi mhusika hupewa zawadi ya mfanyakazi bora wa mwaka ama utendaji uliotukuka.

Je, huyu wa pili aliyetia maoni mengi mabaya kwenye *boxes* la maoni, wizara inampa nafasi au inachukua hatua gani wizara kwa mtu kama huyu, ambapo mambo mengi anayoyafanya kama vile kunyanyasa wagonjwa ama kuchukua rushwa kwa wagonjwa.

Mhe. Spika, naomba swali hili Mhe. Naibu Waziri, anisaidie.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante sana Mhe. Spika, ni kweli kuwa *suggestion boxes* zipo hospitalini na ukiingia pale ofisi ya Daktari Mkuu nje kabisa utalikuta *box* hilo na pia, kwa Mkurugenzi, isipokuwa naomba nikiri kwa kuwa wazi kabisa kwa sababu hayapo ya kutosha, yaani yanatakiwa kila wadi nje na wala sio kule kwa *nurses* au madaktari.

Kwa kweli, kila wadi inatakiwa kuwa nayo hii *suggestion box*, ili uweze kama mgonjwa au anayehudumia mgonjwa ama mtu yeyote anayetumia huduma za hospitali aweze kuandika maoni yake, yakiwa mazuri au mabaya ama malalamiko au ya kusifu basi linatumika *box* hilo hilo na wala hakuna *box* jekundu au la kijani ambalo moja linachukua maoni mazuri au mabaya, aaa! *Box* hilo hilo moja.

Pili, naomba niseme kwamba hivi karibuni tunatarajia kuwa na semina kubwa sana kiwizara na hii nashukuru Mhe. waziri, ndiye anayeongoza jambo hili, kati ya wauguzi, madaktari pamoja na wale askari wa mlangoni kwa sababu kuna malalamiko tumepokea kuhusiana na wale askari wa mlangoni wakati wale wauguzi au watu wanaokwenda kuangalia wagonjwa kidogo wanapata matatizo.

Kwa hivyo, tumegundua kwamba kuna *linkage*, yaani mawasiliano ambayo yanakosekana, hivyo hayo tutayashughulikia katika hiyo semina. Lakini ajenda moja wapo ambayo inatarajiwa kuzungumziwa katika hiyo semina ni kuanzisha mfumo wa zawadi kwa yule anayesifiwa mfanyakazi bora, tuseme mfano kila mwezi, yaani mfumo wa zawadi wa mfanyakazi bora, ili wauguzi, madaktari pamoja na wafanyakazi wa hospitali wapate kuwa na moyo zaidi kuitaka ile zawadi kwa kuwa mfanyakazi bora. *(Makofi)*

Sasa kwa yule ambaye hajasifiwa ama amelalamikiwa basi tunatarajia huyo kwanza (a) kumwita na kuambiwa na *management* yake, yaani viongozi wake watamwita na kumwambia, lakini likiendelea tatizo lile basi kuna mifumo ya kutoa onyo ndani ya utaratibu wa hospitali atapewa onyo. Kwa hiyo, yote mawili hayo yatafanyika la kusifiwa na la kuitwa kupewa ovyo. Ahsante sana.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu

Waziri, kwa kuwa ni muda mfupi tu amepewa nyadhifa hiyo na kuweza kutujibu vizuri kwa fasaha kama alivyosifiwa na Mheshimiwa Mwakilishi, mwenzangu aliyepita.

Mhe. Naibu Waziri, wewe ni mtembeaji katika nchi tofauti na hasa katika mambo ya hospitali za wenzetu katika nchi za nje. Wenzetu wanakuwa na *special uniform* pamoja na vitambulisho, *incase* kwa kuwa umo katika harakati za kuweza kukamilisha masuala ya vitambulisho.

Mhe. waziri, ni lini suala hilo ambalo utaweza kulikamilisha kwa sababu kuokoa hiyo *leakage* iliyotokezea kati ya walinzi na madokta kuweza kuwekwa nje.

Lakini pili, Je, kuna sheria ya kuwa mtu hakuweza kuvaa *uniform* anakuja kazini kufanya kazi sheria hiyo ipo ya kuweza kumstopisha?

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mheshimiwa, sheria hiyo ipo na juzi tena katika mswada uliopitishwa hapa Barazani ya kuunda Baraza la Wauguzi na Wakunga, nilisisitiza jambo hili lipo na nashukuru Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, alitoa mchango mzuri sana katika sheria ile, kwa hivyo, hilo ni kwa upande wa wauguzi na wakunga lipo tayari na litakapoundwa tu Baraza, naamini litakuwa na meno makali kwa kusimamia sheria hiyo.

Lakini kuna sheria nyengine ya wizara ambayo kwa wafanyakazi wote, *infect* maana yake ametaja hospitali za nje; hospitali za nje hata *attendant* yule anayekwenda kumtizama mgonjwa lazima apewe kitambulisho kuingia kumtizama mgonjwa na anapotoka anakiacha, sisi hilo bado hatujafikia huko, lakini ndio inavyotakiwa hata kama wawili watatu mnapokwenda basi mnapewa na vile vitambulisho vya kule nje vinakuwa na rangi *category (a), category (b)* na *category (c); category (a)* ni yule ambaye anashughulika na mgonjwa, saa zote yupo pale pale hospitali, anampatia huduma mgonjwa, pengine mgonjwa anahitaji huduma za ziada ambazo anahitaji kupewa kwa muda wote.

*Category (b)* ni yule anayeingia katika nyakati za kuona wagonjwa asubuhi na jioni, lakini *category (c)* ni yule ambaye anapewa kuingia kumuangalia mgonjwa anatoka hapo hapo anaacha kile kitambulisho, hayo yamo mbioni na *Inshaalla* tukifanikiwa huko mbele, kila anayeingia pale hospitali kuanzia getini atapewa kitambulisho kwenda kumuangalia mgonjwa na atakapotoka atatakiwa kuacha kitambulisho. Baadhi ya maeneo mengine tayari yameshafanyika mambo hayo kwa magari; magari yanapewa vitambulisho kuingia ndani na yanapotokoka kile kitambulisho unakiwacha.

Kuhusu suala la *uniform*, suala la *uniform* hilo lipo hospitali na hivi sasa *orderly* anatakiwa kujulikana *orderly* anavaa *uniform* hii, *assistance nurse, senior nurse* na wenyewe wana vyeo vyao humu kwa wale wanaotembelea hospitali sana utaona kuna vyeo mule mstari mmoja, mistari miwili, mistari mitatu na somo hili pia linafundishwa katika Chuo cha Afya Mbweni cha *uniform* na jinsi ya kumtambua *nurse na middle wife* ama *senior nurse, assistance nurse* na kadhalika. Ila wale wakuu wa idara husika au wakuu wa wadi husika hawatakiwi kumruhusu *nurse* kuingia wadini bila ya *uniform*, sasa hatua gani zinachukuliwa hilo ni jukumu lao wao kama wakuu wa idara na wadi hizo, lakini sisi kama wizara tutaendelea kusisitiza sheria zile zifuatwe na namshukuru Mheshimiwa Muwakilishi, kwa kulileta hili kwamba litaendelea kusisitizwa ili *uniform* zivaliwe na wakuu wa idara ama wadi *chief nurses* waweze kuchukua hatua kwa wale ambao hawafuati sheria hizo. Ahsante.

**Mhe. Spika**: Swali la mwisho fupi Mhe. Saleh.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe.Waziri, napenda niulize swali moja tena fupi la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa wauguzi kwanza kabla ya hapo, naomba nitoe pongezi za dhati kwa wauguzi pamoja na maslahi madogo wanayoyapata pamoja na kada mbali mbali za afya, napenda kuwapa pole kwa kazi nzito wanayoifanya, baada ya pongezi hizo naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa suala la msingi lilitarajiwa kwamba wauguzi wavae beji na kwa kuwa wauguzi kazi zao wana-*deal na* wagonjwa wa kila sampuli na wenye maradhi kadhaa wa kadhaa ambayo ni ya hatari ambayo ni *contaminated* na kwa kuwa beji inaweza, aidha ikatoka ikamgusa mgonjwa au yeye akagusa kwenye beji ile na hatimae beji yenyewe ikawa *contaminated* na ikawa matatizo pale itakapokwenda kuguswa na mtoto wake au mtoto wa familia kule nyumbani kwake na hatimae kusambaza maradhi kwa watu wengine.

Je, isingekuwa vyema kwa wauguzi badala ya kuwapa beji kwa sababu wanavaa zile sare zao zikaandikwa jina lake pamoja na nambari yake ya *registration*, badala ya kuwavisha beji tukawaandikia nambari kwenye majina yao pamoja na nambari zao kwenye *uniform* zao kama wanavyofanya wapiganaji wetu katika vikosi vya jeshi la wananchi, polisi na kadhalika, badala ya kuwatengenezea mabeji.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mimi nakubaliana naye kwamba ikiwezekana *uniform* ziandikwe na kadhalika, lakini katika *security* ya hospitali kuna *issue*

ya picha pia inabidi umu-*identify* sasa ile picha huwezi kuchora kwenye nguo lazima iwe katika kitambulisho, kwa sababu unahitaji kumu-*identify* yule mtu kwa picha kama ndiye huyu mwenye beji hii ambaye sura yake inafanana na hichi kitambulisho chake. Hilo la kwanza.

La pili, kuhusiana na ku-*protect* beji zile zinakuwa za kuvaa hapa za kubandika hapa, kwa hivyo, si rahisi kumfikia mgonjwa, lakini tunataka kumu-*introduce* mgonjwa kwa kuvaa zile beji mkononi ili kutambuliwa kwamba huyu ni mgonjwa fulani, ana maradhi fulani au ana tatizo fulani, ili tusianze tena kuchanganya matibabu kama yaliyowahi kufanyika hospitali nyengine kichwa kwenda kwenye miguu na miguu kwenda kwenye kichwa. Hilo tunatarajia kulifanya.
Mhe. Spika, sasa naomba Wajumbe watupe muda tu ambao bado tunaendelea kuwasiliana na kampuni hizi baada ya kuanza wataona mabadiliko katika kumtambua muuguzi, daktari, *orderly*, mfagiaji na hadi askari wa pale mlangoni. Ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Mhe. Naibu Waziri, tunakushukuru ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe, nataka niwaombe radhi, ninapenda sana niendelee na kikao kwa sababu kama siku tatu nyuma huko nilikuwa sishiriki kwa sababu hali ilikuwa hairuhusu, nilifikiria leo ninaweza nikaenda vizuri, lakini nimeshuhudia kwamba bado hali hainiruhusu, sasa naomba radhi sana kwamba sitoendelea na kikao hichi na nitamuomba Mheshimiwa Mwenyekiti, aje akalie kiti na aendelee na shughuli iliyopo mbele yetu ambayo ni majadiliano ya Mswada mpya wa Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2014 ambayo jana uliwasilishwa.

Kwa hiyo, sina shaka umeungwa mkono kuonesha kwamba sasa mswada huo unaweza ukajadiliwa ndani ya Baraza hili. Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi hii basi kuwashukuru kwa mashirikiano na sasa naomba nimkaribishe Mheshimiwa Mwenyekiti, aje aendelee na kikao.

*(Hapa Mheshimiwa Mwenyekiti alikalia Kiti)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar ya Mwaka 2014

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba kwa mara nyengine tena kuweza

kuendelea pamoja na shughuli hii, lakini tumuombee dua Mhe. Spika, ili aweze kurejea haraka na tuweze kuendelea katika masuala yetu.

Waheshimiwa Wajumbe, katika orodha ambayo ninayo hapa tunampa nafasi Mhe. Ali Salum Haji, ili aanze kuchangia na baadae Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ajiweke tayari na vile vile, kama ambao wanataka kuchangia naomba walete majina yao ili tuweze kuwekeana utaratibu kama zilivyo taratibu zetu. Ahsante Mheshimiwa Ali Salum Haji.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa dhati kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia mswada huu wa sheria ya kufuta sheria namba tatu ya mwaka 1935 ya Manispaa ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nichukue fursa adhimu ya kumshukuru Mhe. Waziri, kwa namna pekee baada ya kuleta muda mrefu na kubadilisha sheria hii ya Manispaa juu ya mambo au kadhia ambayo ilikuwa inawakuta wenzetu au juu ya suala zima la baadhi ya sheria hizi kugongana baadhi ya taasisi na taasisi na hatimaye mswada huu umekuja na nina imani kwamba mimi pamoja na wenzangu tutauchangia kwa kina kabisa katika kuona kwamba tunaweka mustakabali mzuri kwa Waheshimiwa wetu madiwani pamoja na masheha katika majukumu yao ya kazi ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, kwa muda mrefu sheria za manispaa zilikuwa zikileta migongano baina ya manispaa na taasisi nyengine na hususan katika taasisi za Mji Mkongwe, kulikuwa kuna muingiliano mkubwa na ulikuwa unapeleka ufinyu wa watendaji kazi katika taasisi hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niingie kwenye mswada huu kwa kuangalia baadhi ya vifungu hadi vifungu na mimi kuweza kutoa maoni yangu.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 232 kifungu cha 4(3) unasema kwamba mipaka ya kila Serikali ya Mitaa itaainishwa kwa mujibu wa masharti ya sheria hii. Mimi hapa nilikua naomba kutoa tahadhari tu kwa wizara wakati utakapofika wakitangaza hiyo mipaka kuangalia kwa makini zaidi suala la kijografia, kwa nini niseme hivyo?

Mhe. Mwenyekiti, unajua mipaka yetu ya Zanzibar ina matatizo, jografia yake ina ugumu wa muingiliano wa mitaa na hili niliwahi kuzungumza kipindi kirefu unaweza ukaja ukakuta nyumba na hususan mitaa ya Chumbuni huko na Kwa Mtipura mlango wa mbele uko shehia nyengine na mlango wa nyuma uko shehia nyengine. Sasa hili linatupa ugumu wa muingiliano wa kazi za kiutendaji pale mipaka inapokuwa imegawiwa na hili hata kwangu mimi limenikuta.

Mhe. Mwenyekiti, wadi yangu ya Mikunguni ina shehia mbili; Shehia ya Muungano na Shehia ya Mikunguni, lakini cha kustaajabisha katika ukataji wa mipaka yake, yaani diwani anayefanya kazi katika eneo lile Shehia ya Muungano baina ya shehia ya Muungano na Shehia ya Mikunguni katikati inaingia Shehia ya Kwaalamsha, maana diwani anafanya kazi kwenye Shehia yake ya Muungano anaruka Shehia ya Kwaalamsha ambayo ni wadi ya Kwahani anaingia katika shehia yake nyengine. Sasa nasema hili suala la mipaka kidogo linakuwa na mashaka sana, kwa hivyo, nimuombe Mhe. Vesta, aangalie kwa makini zaidi, yaani kuangalia masuala ya mipaka kijografia.

Mhe.Mwenyekiti, na nikiingia kwenye jografia nimuombe hebu tuangalie zaidi katika suala zima la kukata mipaka kwa kuangalia hizi barabara zetu angalau japo za ndani, kwamba eneo ambalo litakuwa limezungukwa na barabara basi linaweza likawa ndio eneo la shehea nzima kuliko kwamba eneo lile lile katikati unakuta njia za ndani ndio zinagawa mipaka, hili suala kidogo linakuwa linaleta ugumu katika utendaji wa kazi na muingiliano maana yake kujijua mimi niko shehia gani na mwenzangu yuko shehia gani.

Mhe. Mwenyekiti, jengine naomba niingie katika kifungu cha 7(d) kinasema kwamba; "Kuwezesha na kukuza elimu kwa jamii" na pia, kifungu cha 7(f) kinasema kwamba; "Kukuza na kujitegemea baina ya watu kwa kupitia uhamasishaji wa rasilimali zilizopo wa kuhakikisha upatikanaji wa huduma kwa jamii ambazo ni endelevu".

Mhe. Mwenyekiti, katika vifungu hivi viwili hapa katikati labda niongeze neno dogo tu kama itakuwa inawezekana Mhe. waziri, atanikubalia, kwa mfano katika hiki kifungu cha 7(d) kinasema; "Kuwezesha na kukuza elimu kwa jamii baina ya elimu" na kwa naomba liongezwe neno "bora".

Maana yake nakusudia kwamba tuweke "Kuwezesha na kukuza elimu bora kwa jamii" na kile kifungu cha 7 (f) vile vile, naomba "baina ya huduma" na pia, tuongeze "huduma bora kwa jamii ambazo ni endelevu".

Mhe. Mwenyekiti, pia, naomba niingie katika kifungu hicho hicho cha 7(k) ukurasa wa 224, kifungu hichi kinasema kwamba; "Kuhamasisha na kusaidia shughuli na mafunzo ya kada ya utawala kwa wanawake vijana, wazee na watu wenye ulemavu". Sasa mimi kilikuwa kinanipa mashaka hichi kifungu kwa sababu namna kilivyoandikwa; "Kuhamasisha na kusaidia shughuli na mafunzo ya kada ya utawala kwa wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu nikajiuliza sisi wanaume maana yake shughuli za mafunzo na utawala maana yake hazitugusi.

Sasa ningemuomba Mhe. waziri, kama itakuwa inawezekana kwa sisi wanaume basi angalau kabla ya kuweka kitu wanawake tungeweka watu wote wakiwemo wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu, sasa tukiweka watu wote maana yake nakusudia hata na sisi akina baba katika kifungu hichi tunaweza kutambulika kuliko kuweka hivi ukakuta kama kina baba wao hawatambuliki kwa lolote na chochote.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye ukurasa wa 225 kifungu cha 11 (2) (a) Baraza la Jiji ambalo litakuwa ni chombo kinachojitegemea na litakuwa limegawiwa katika Baraza la Manispaa. Mimi kidogo tu naona lugha haijakaa vizuri hapo labda Mhe. Waziri, angekiangalia na akajaribu kukiweka vizuri, yaani tunapozungumza kwamba Baraza la Jiji ambacho kitakuwa ni chombo kinachojitegemea na litakuwa limegawiwa katika Baraza la Manispaa. Mimi kidogo sijafahamu vizuri lakini baadae kidogo Mhe. waziri, atakuja kutupa ufafanuzi labda ataelimisha zaidi namna walivyokusudia kuliweka katika suala hili.

Lakini katika kifungu hicho cha 11(5) kinasema kwamba; "Wadi ikiwa mjini au kijijini itajumuisha si chini ya shehia mbili na kila sheria itakuwa na vijiji visivyopungua viwili, kwa maeneo ya kijijini na mitaa isiyopungua miwili kwa maeneo ya mjini. Sasa nataka Mhe. waziri, anapokuja anisaidie nataka anipe ufafanuzi wa vijiji, vijiji maana yake nini? Kwa sababu nimejaribu katika ufafanuzi sijaona vijiji vilivyofafanuliwa ni kitu gani.Sasa labda amekusudia mitaa kwa sababu unajua kuna tatizo la hapa Zanzibar kwamba hili suala la kuwa na vijiji kwa halisia hasa bado halijakuwepo, eneo dogo lakini labda utakuta hapa panaitwa Muembe Maringo, muembe sijui nini, yaani eneo dogo tu, sasa eneo dogo linakuwa na mitaa mingi, sasa sijajua wao watatumia taathira gani katika kupata vijiji katika maeneo haya.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba nichangia katika eneo jengine la Sehemu ya Nne muundo wa kazi na uwezo wa Serikali na Mitaa. Katika eneo hili naomba niingie katika kifungu cha 18(2)(e). Hapa pametajwa ule uanzishwaji wa muundo wa Baraza wale ambao watatunda hilo Baraza lenyewe. Katika waliotajwa kwenye Baraza hili kifungu hiki cha mwisho cha (e) kinazungumza madiwani wasiozidi watano ambao watateuliwa na waziri wawili miongoni mwao angalau wawe wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze kwamba ile *fifty fifty* inaanza kuonekana katika sheria zetu hizi za Zanzibar na natumai kwamba wanawake sasa hivi wataanza kufarajika katika kupata haya masuala ya ajira. Lakini jambo linalonipa mashaka ni moja tu, hata kwamba hizo sifa za madiwani ambao watateuliwa hazijaainishwa, sijapata kuziona. Nimejaribu kusoma maeneo mengi, lakini sifa sijapata kuziona za madiwani watakaoteuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika sheria iliyopita iliainisha wazi uteuzi wa madiwani watatu ambao watateuliwa na waziri, basi watakuwa na sifa maalum wakiwemo ma-*engineers*, ma-*accountants* na wanasheria. Sasa katika huu uteuzi wa watu watano hapa sijaona sifa za hao madiwani ambao watakaoteuliwa, ni vyema basi Mhe. waziri, akatengewa watu ambao anatakiwa ateue, basi watakuwa na sifa zifuatazo, kuliko kuiacha wazi ina-*hangs* kidogo itakuwa haileti mantiki nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba nichangie kifungu cha 19 kuhusu Kazi za Baraza la Jiji. Katika kifungu cha 19 (c) kinasema; "Kuongeza mapato kwa lengo la kutekeleza majukumu yake". Mimi hapa kidogo napata mashaka katika suala zima ambalo na hususan katika sheria iliyopita, sheria iliyopita ilikuwa na mapungufu makubwa sana, lakini nafikiri mswada huu ukipita labda sheria itatuwekea ufafanuzi, itatuwekea wazi zaidi katika hii namna ya kukusanya kodi.

Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na muingiliano baina ya taasisi ya Manispaa na taasisi nyengine na kumekuwa kuna migongano mikubwa sana inafika mahali hata wakati mwingine kukosa sintafahamu baina ya taasisi na taasisi. Kwa mfano sasa hivi kuna mgongano wa ukusanyaji wa kodi ya vile vitu vinavyoelekea kama ni vitu vya utalii, kwa mfano vinyago, hata zile nguo za aina ya seruni na batiki.

Sasa kumekuwa na mgongano Manispaa wanapotaka kwenda kukusanya kodi katika maeneo yale au kukata leseni, unamkuta mfanya biashara anakwambia kwamba mimi nimeshakata leseni katika Shirika la Utalii kwa sababu hivi vitu ni vya utalii. Sasa hii sintafahamu ilikuwa ni kubwa, lakini ukiachilia hapo katika eneo jengine ambalo lilikuwa linaleta migongano ni katika suala zima la leseni za biashara. Kuna *level* ya leseni ya biashara ilikuwa ikifika basi unaambiwa kwamba leseni hii imekatwa katika Serikali Kuu, watu wamekwenda zao kukata katika Idara ya Forodha.

Sasa ninakuwa ninapata mashaka labda kwamba watumiapo mamlaka ya kuongeza mapato katika Manispaa yao na sheria hii ishawapa nguvu ya kukusanya mapato. Lakini katika maeneo yale yale kuna biashara baadhi ya taasisi wanasema hizi ni biashara ambazo zimo ndani ya mamlaka yao.

Sasa Mhe. waziri, labda atakuja kutuainishia na kutusaidia, pamoja na kwamba nimezungumza watu kuhusu huu mswada kwamba, aa, watafuata sheria za nchi, lakini sasa mimi nafikiri tungewapa fursa halisi kwamba biashara ambazo zitafanywa katika maeneo yao basi mamlaka yawe ni ya Manispaa, kuliko kwamba biashara nyengine hizi unazikuta zinaingiliwa na Manispaa, biashara nyengine zinakwenda katika masuala ya utalii inakuwa

inawapa mashaka kuweza kuipambanua kwamba biashara hii kweli inastahiki utalii au biashara hii ni biashara ya kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba kifungu cha (d) kimezungumza kuendeleza biashara ya utalii na uwekezaji. Sasa kifungu hiki kimezungumza hivyo, lakini bado mashaka yanakuwa yanaingia unaweza kuendeleza biashara, lakini muingiliano wa kodi ukawa na matatizo. Sasa naomba Mhe. waziri, aje kutusaidia katika kuliweka wazi.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa huo huo kifungu cha 20, nazungumza tena wale wale madiwani wa kuteuliwa, hapa katika kuanzisha hili Baraza la Manispaa kutakuwepo na madiwani, si zaidi ya 10 ambao watateuliwa na Mhe. waziri. Bado naendelea kwamba pia madiwani hawa hawajajua sifa zao watakuwa na sifa gani katika kumpa nguvu Mhe. waziri, kufanya uteuzi. Lakini katika kifungu hiki cha 20, kimenipa mashaka, sijaangalia katika marekebisho huku, nilijaribu kuangalia lakini sikuona kwamba marekebisho yamefanywa au vipi, kwa sababu kinasomeka kifungu cha 20(1); "Kuanzishwa Baraza la Manispaa ambalo litaundwa na Wajumbe wafuatao:

(a) Meya ambaye anateuliwa miongoni mwa madiwani, naibu meya ambaye anateuliwa miongoni mwa madiwani na madiwani wote walioteuliwa na wananchi kutoka wadi zao".

Sasa naona kwamba imesomeka uteuzi baada ya uchaguzi. Sasa nalo hili nafikiri suala la mapungufu ya *typing error* linaweza likawa sawa. Lakini ukurasa wa 230 Ibara ya 22(d), vile vile, ukija pana uteuzi wa madiwani wasiopungua 10, nafikiri kama la mwanzo linaweza likakaa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 231 pana kifungu hapo cha (h) kusimamia uchimbaji wa mawe, machanga na uvunaji wa mbao au rasilimali nyengine za asili kama itakavyoainishwa na waziri mwenye dhamana na rasilimali za asili, nafikiri patakuwa na matatizo ya *typing error* tu, hilo ninaweza kuliacha. Lakini Ibara 24(d) kuna suala la uteuzi wa madiwani kama nilivyozungumza mwanzo ni sifa.

Mhe. Mwenyekiti, nikenda katika ukurasa 232 katika kifungu cha (p) inasema; "Kufanya kazi za ukataji wa miti, uwekaji wa matuta, upandaji na uondoaji wa miti pembezoni mwa barabara". Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa nilikuwa naomba tu kama itawezekana basi Mhe. waziri, tuongeze neno dogo baina ya matuta na upandaji tuongeze barabarani na kisomeke kwamba kufanya kazi za ukataji wa miti, uwekaji wa matuta barabarani, upandaji wa miti na uondoaji wa miti. Kwa hivyo, nilikuwa naomba liongezeke neno "barabarani" ili kuweka lugha nzuri katika hilo neno.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba nije katika suala jengine kabisa kwenye ukurasa wa 236, Ibara ya 38. Mimi hapa nimepata faraja kubwa sana na niwaombe wenzangu, sioni haja ya mswada huu kutokuupitisha na kuwa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kabla sijawa mwakilishi ila nimekuwa diwani kwa muda wa miaka 10, yaani vipindi viwili tofauti, nilikuwa naona kadhia na manyanyaso na mateso ya Waheshimiwa madiwani kufanya kazi katika mazingira magumu pasipo kujua mafao yake yako katika hali gani.

Mhe. Mwenyekiti, na hiki kimekuwa kilio cha muda mrefu, tumekuwa tukipiga kelele madiwani wapatiwe mishahara kutokana na majukumu yao kwa sababu wao ni wanasiasa kama sisi, wanaingia katika uchaguzi kama sisi, uchaguzi wetu unafanyika wakati mmoja, lakini tatizo lilikuwa kwamba wao wanashindwa kulipa mishahara na kwa sababu ambazo nyingi tu kwamba Serikali ilikuwa haina uwezo, sasa ninashukuru kwamba mswada huu umekuja angalau kuwatambua, pamoja na kwamba watakuwa si wafanyakazi wa kudumu, lakini maslahi ya madiwani yameonekana wazi kabisa.

Mimi niombe faraja nafikiri angalau hii itatoa unafuu kwa wale ambao madiwani kama sisi baada ya kuona kwamba mafao ya madiwani, sio mazuri tukaanza kukimbilia mafao mazuri kwa upande wa uwakilishi, sasa hivi labda wanaweza kubakia katika kazi zao za udiwani na kuwafanyia kazi wananchi wanaowachagua.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki cha 38 kinasema kwamba; Naibu Meya na madiwani wengine kabla kusoma hapa na naomba nisome hiki cha pili, kwanza ambacho cha pili ndio kitakuja katika suala hilo la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 37(2) kinasema kwamba;

"Meya atalipwa mshahara na stahiki nyengine kama itakavyopangwa muda kwa muda".

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 37(3) kinasema kwamba;

"Meya hatakuwa mtendaji mkuu wa Baraza, lakini atakuwa ni mshauri mkuu wa Baraza".

Sasa hii nafikiri inakwenda kama sheria, sasa hivi ndivyo ilivyo, ndivyo ilivyo mstahiki meya kwamba anapata mshahara kutokana na mafao yake. Lakini bado tulikuwa tuna kilio wakati hicho kipindi ambacho mimi ni diwani katika mantiki nzima ya Mhe. Naibu Meya, ambacho Mhe. Naibu Meya,

ametamkwa hapa katika kifungu cha 38, naomba nikisome Mhe. Mwenyekiti, kwamba;

"Naibu Meya na Madiwani wengine hawatakuwa wafanyakazi wa kudumu na watalipwa mishahara na stahiki nyengine kama itakavyopangwa kila baada ya muda na kuidhinishwa na waziri".

Mhe. Mwenyekiti, mashaka yangu yako kwa Naibu Meya na ukiangalia mswada huu namna unavyomzungumza Naibu Meya halafu Naibu Meya kwamba tumemuunganisha kwamba stahiki zake zitakuwa sawasawa na madiwani wakati *level* ya madaraka iko tofauti. Naibu Meya ni msaidizi wa Meya na katika mswada huu unazungumza hasa pale ambapo meya atakuwa hayupo kazi zake zitafanywa na Naibu Meya. Sasa ninakuwa napata mshangao kwamba leo huyu mtu humuajiri, hajaajiriwa, lakini meya ambaye kaajiriwa anapokuwa hayupo kazi zake zinafanywa na mtu ambaye si mwajiriwa.

Sasa mimi nilikuwa naomba Mhe. waziri, kama itakuwa inawezekana basi na huyu Naibu Meya naye tungemfanya ni mwajiriwa, hata kama itakuwa mshahara utakuwa sio mkubwa kama wa Meya au mafao yake, lakini tutampa nguvu ya kujisikia pale ambapo Meya anapokuwa hayupo basi Naibu Meya kufanya kazi zake kidogo inakuwa inaleta mustakbali mzuri, kuliko kwamba tumemuweka katika *level* ya madiwani wa kawaida katika sifa zake za kupata stahiki, lakini meya anapokuwa hayupo unampa kazi ende akakamate kazi za Meya.

Mhe. Mwenyekiti, kidogo nimuombe Mhe. waziri, aliangalie kwa udhati kabisa, aangalie *level* ya Mhe. Naibu Meya. Hili lilitukuta hata sisi katika Baraza la Wawakilishi, lilitukuta katika kuweka hadhi ya Mhe. Naibu Spika na Spika. Hadhi ya Spika unaikuta katika hali ya juu, lakini Naibu Spika, kidogo kulikuwa kuna mashaka mashaka, lakini nashukuru kwamba Baraza hili lilijaribu kurekebisha baadhi ya mambo na Naibu Spika hadhi yake ikaanza kukua. Kwa sababu huyu ndio msaidizi, sasa kama msaidizi unamuweka katika hali ya watu wa kawaida hili kidogo halileta taswira nzuri.

Nimuombe Mhe. Waziri, kwa dhati kabisa ili akipe hadhi cheo cha Naibu Meya angalau na yeye ajisikie kama ni msaidizi wa mstahiki meya na mafao yake basi yawe tofauti na madiwani wa kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niingie katika ukurasa wa 239, Ibara ya 45. Ibara hii inazungumza kwamba; "Kutakuwa na karani wa Baraza la Wadi ambaye ataajiriwa na mamlaka ya mtaa kufanya kazi za kila siku katika hiyo ngazi ya wadi". Sasa nilikuwa ninapata mashaka kwamba hii taasisi tusije tukaipa kazi

ya kuajiri, lakini ikafikia mahali ikaja ikashindwa kupata mafao ya kumlipa huyo mwajiriwa. Sasa nilitaka Mhe. waziri, atakapokuja aniambie kwamba hilo Baraza la Wadi litakapo mwajiri huyo karani atakuwa analipwa kupitia Baraza lenyewe au katika Taasisi ya Serikali kupitia Manispaa au Baraza la Mji, atakapokuja Mhe. waziri, atanisaidia ili kuona kwa sababu hofu yangu ni uwezo tusije tukafika mahali tukashindwa kuwa na uwezo wa kumlipa huyo karani.

**Mhe. Mwenyekiti:** Una dakika 5 za ziada.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Kwa sababu ni muda mkubwa wa Manispaa na nilikuwa diwani naomba niwatetee madiwani wangu. Utanipa za ziada kidogo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 240, Ibara ya 47(d) imetaja; "Kuanzisha muundo wa Kamati ya Ushauri wa shehia" na katika kifungu (d) hapa kinasema kwamba; "Miongoni mwa Wajumbe wake itakuwa kuna wataalamu wasiozidi watatu wanaoishi katika shehia kama itakavyopendekezwa na Kamati ya Ushauri". Mimi nilikuwa naomba tu Mhe. waziri, unisaidie kwamba sijaona hawa wataalamu maana yake hizo sifa zenyewe maana yake haukutajwa utaalamu wa fani gani au mtaalamu tu kwa sababu masuala ya wadi haya na Baraza inakuwa ni taaluma zake zaidi ni mambo ya kijamii. Sasa sijaona zile taaluma ambazo zimeainishwa katika masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, chengine ambacho nataka nikizungumzie nikidhi muda wako na wenzangu wapate kuchangia katika ukurasa wa 241, kifungu cha 49, kinasema;

“Mtu atastahiki kuwa Mjumbe wa Kamati ya Ushauri wa Shehia ikiwa:

(a) Mzanzibari mwenye umri wa miaka 21 sina mashaka; na

(b) Mkaazi wa Shehia husika; kidogo hapa ninapata mashaka."

Unapozungumza mkaazi wa shehia husika, mkaazi ana mamna mbili na mkaazi kama ni mkaazi wa kawaida, lakini kuna mkaazi pia ana mamlaka katika masuala ya upigaji wa kura kwamba lazima atimize miaka mitatu mfululizo, yaani miezi 36. Sasa napata mashaka isije hapa tukaweka mkaazi peke yake ikawa mtu amekuja juzi ana mwezi mmoja, lakini tukampa nguvu ya kuingia hapa wakati mtaa wenyewe hawauelewi, tabia zenyewe hawazijui, yaani ule uhalisia basi angalau tungeweka muda mkaazi ambaye asiyepungua muda fulani katika huo mtaa, ndio tunaweza tukamuingiza kuliko kuwa mtu

kaja jana lakini ana sifa nyengine akaja akagombania na kuna vitu ambavyo havimfungi kuingia katika chombo hiki. Sasa hili kidogo lilikuwa linanipa mashaka, lakini Mhe. waziri, nafikiri atakapokuja atanisaidia.

Lakini chengine ambacho kinanipa mashaka hiki kifungu cha (c) ambacho amehitimu angalau elimu ya kidato cha nne, ni kweli ulimwengu wetu ni wa sayansi na teknolojia na tunahitaji wasomi. Lakini katika baadhi ya maeneo usomi hauhitajiki na hususan katika ngazi hizi ya haya mabaraza ya shehia.

Mhe. Mwenyekiti, humu ukiangalia hata zile kazi ambazo zinatakiwa za hawa watu kufanya zile kazi zote ukiziangalia basi mara nyingi utakuta ni kuelimisha jamii katika masula ya sheria kuelimisha jamii umuhimu wa kutumia hadhi kuelimisha jamii kushiriki katika kazi za mikono yaani mambo yote ni kuelimisha jamii. Hawa watu wana-*deal* zaidi na jamii, sasa tukianza kuangalia watu wa *level* hii, kidogo tutaanza kupata mashaka na kuwapata wale wenye sifa.

Mhe. Mwenyekiti, na hususan tukiangalia mtu ambaye atakuwa amepata taaluma ya kidato cha nne kuja kumuweka katika haya mabaraza, sitegemei kama hawa watu tutakuja kuwapata. Kwa sababu watu wetu sasa hivi ni watu wa mahitaji, mtu akishakuwa na cheti anakimbilia katika kazi ambayo ina maslahi na yeye, sasa wasomi wote watakimbilia kwenye kazi ya maslahi, hapo tutakuja kuwakosa watu ambao tutawahitaji kuwaingiza katika haya mabaraza ya shehia.

Sasa ningeona labda tungeweka tu sifa zile za kibinaadamu ambazo zinaweza kumkuza mtu akaweza kuitumikia hii kazi kuliko kumuweka ambaye lazima awe na sifa awe amehitimu elimu ya *form IV*.

Mhe. Mwenyekiti, mtu anayehitimu elimu ya *form IV,* atataka ende jeshi, uhamiaji au polisi huko akapate ajira na mapesa yaliyokuwa mazuri, hutomuweka katika Baraza la Shehia akaanza kusikiliza matatizo na mambo ya kijamii katika katika muda ambao si mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kabisa katika mchango wangu huu wa leo katika ukurasa wa 241, kifungu cha 51 kinasema kwamba; "Kila Mjumbe wa Kamati ya Ushauri wa Shehia atafanya kazi kwa muda wa kipindi cha miaka mitano isipokuwa atakapokoma kuwa Mjumbe kwa kifo, kujiuzulu au kuondolewa". Mhe. waziri, nataka atakapokuja anisaidie kwa sababu kimeingia kitu atafanya kazi, sasa nilitaka kujua kwamba hao Wajumbe hawa watakuwa wameajiriwa au itakuwa vipi. Kwa sababu utakapozungumza mtu kufanya kazi tayari mtu itakuwa ameajiriwa angalau kama si mwajiriwa basi

ije lugha nyengine ambayo itakuwa haina mashaka iwe atatumikia kitu kama hiki kuliko kusema kwamba atafanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nikushukuru kwa dhati na nimshukuru tena kwa mara nyengine Mhe. waziri, kwa kuleta mswada huu, nasema kwamba kuna baadhi ya mambo mengi ambayo yaliyokuwa yakitukwaza kwa kipindi kirefu, lakini nina imani kwamba baada ya mswada huu kupitishwa na kuwa sheria basi yale matatizo ambayo yaliyokuwa yakiwagusa Waheshimiwa wenzetu madiwani na taasisi nyengine yanaweza kutatuka na kuweza kupatiwa ufumbuzi kwa kina.

Baada ya hayo kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani, naunga mkono mswada huu mia kwa mia. Ahsante sana nakushukuru.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikupongeze sana kwa ujasiri wako na asubuhi hii ya leo kuweza kunipa niweze kuchangia ili kufanikisha hali halisi ya sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba kidogo uniachie kama dakika mbili au tatu usinijumlishie katika sehemu moja ya kuchangia na hiyo ni lazima kutokana hali halisi, siri yangu ya mafanikio ili kuweza kuitoa hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. waziri, mkakamavu na shujaa sana na hasa kutuletea mswada huu ambao aliona kwa sababu kuna watu wengine wanakuwa na akili ya kuzaliwa, Mwenyezi Mungu kawajaalia lakini wengine tuna akili ya kuongezea katika kusoma. Sasa yeye kazaliwa na akili nzuri ameona jinsi gani aweke kumbukumbu katika wizara yake kwa sababu uzuri wa kiongozi siku zote ninasema akiondoka mahali aache kumbukumbu kila mara watu wapate kumsema kwa nia nzuri, atasema mtu Mhe. waziri, bwana, katuwachia kitu kizuri sana. Sasa hilo moja ninampa hongera kubwa sana shemegi yangu Mwenyezi Mungu amjaalie kila baraka na amzidishie yenye kheri na yeye, shari amuondolee.

Lakini pili, nina watu wangu wawili wazee wangu; mzee wangu mmoja Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharini alinisomesha sana alinambia maisha yote unapotaka kufanya jambo kwanza fanya *research*, chunguza jambo halafu liseme. Sasa namshukuru sana Mheshimiwa wangu huyo mzee wangu Maalim Abadalla Mwinyi, Mwenyezi Mungu na yeye ampe kila la kheri na shari amuondolee, azidi kumstawisha, kung'ara na kuwasaidia wananchi wa Mkoa Mjini Magharibi kwa furaha ambayo wanayoiona.

Pia, nimshukuru sana mzee wangu mzee Ali na yeye ni mmoja katika mtaalam ambaye kuna mambo anakuwa ananifahamisha za kumbukumbu, ananipa historia za kumbukumbu na yeye ninapata kuzisema hapa zinasaidia wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, naendelea kuchangia katika ukurasa 237 katika *research* yangu niliyoiona. Kifungu cha 39, kuna lugha na katika lugha hii kila mtu anakuwa na uonaji wake na tafsiri yake, hii yote inakuja kama alivyosema mwalimu wangu Abdallah Mwinyi anakupa jinsi gani ya kuweza kutafsiri lugha watu wakaifahamu. Lakini mimi nilivyoelewa hapa naomba ninukuu; "Kutakuwa na mkurugenzi katika kila Baraza la Jiji na Manispaa ambaye atateuliwa na Rais na Mkurugenzi wa Baraza la Miji, Halmashauri ya Wilaya ambaye atateuliwa na waziri kwa mujibu wa masharti ya sheria ya utumishi wa umma".

Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa kidogo nina utata, iweje Mheshimiwa huyu anateuliwa na Rais ana miguu mingapi? Iweje leo waziri anayeteua yeye wana miguu mingapi? Hapa nina utata, Mhe. mwanasheria, atazidi kunisaidia. Kifungu hiki mpaka macho yananiuma nimekwenda *laboratory* nimetafuta kile ambacho nimepewa na washauri wangu, sikupata jibu. Naomba sana ikiwa Rais anateua na hawa wapewe heshima ya kuteuliwa, kwa sababu hapa kutakuwa na viwango, sio Mhe. Rais, hawezi kuripuka tu kumchagua mtu mkurugenzi basi ndio hivyo tu mkurugenzi, mkurugenzi kwa kuwa jamaa yangu huyu mkurugenzi, hafanyi hivyo.

Sasa mimi nawashangaa sana hapa kuwa haiwezekani Mhe. waziri, awateua hawa tutawapunguzia heshima, tusiidharau hii sheria, kwa sababu sheria hii ndio hiyo inayoipa nguvu Halmashauri za Wilaya, sasa iweje leo tuweze kuikasimu mapema kuipunguza nguvu. Naomba sana iendelee kwa busara na hekima kabisa ridhia sana Mheshimiwa, yako mengi yakuteua, tuteue sisi Wajumbe wa Bodi, tuteue sisi washauri, hiyo nafasi hakuna tatizo. Lakini Mkurugenzi wa Halmashauri mimi naomba sana bado hiki kizingatiwe, kwa sababu leo kama ingekuwa si Ali Salim kuendelea kumteua wa mwanzo, mimi nilitaka niliahirishe Baraza, kwa sababu mimi mpaka sasa hivi *page* ya nane ndio kwanza nimefika kwa kuisoma.

Mhe. Mwenyekiti, huu mswada si mchezo mswada mkubwa sana huu, lakini watu wanauona kitu cha masihara, si kitu cha masihara kwa sababu kitu kinaundiwa sheria, sio masihara. Kwa hivyo, kwa kuwa umemuanzisha Ali Salim basi na mimi nakubaliana maana yake mpaka sasa hivi macho yananiuma niko kwenye *page* ya nane na hii ina 200, sijui na sitini na ngapi, ina 268 kama sikukosea, sio kitu cha mchezo. Kwa hivyo, naomba sana

nimeanzia hapa kwa makusudi kuona katika kitu kilichoniathiri ndani ya moyo wangu kuona kitu hicho.

Kwa hiyo, mimi naomba Mhe. waziri, msiwe na utata na kifungu hiki kabisa, mwanasheria wasiwe na utata na kifungu hiki kabisa, tutoe heshima iwe endelevu, tuwape heshima na wale makatibu wetu kwa sababu ndio maana tunawapunguzia nguvu kumbe kutokana na uteuzi wao unakuwa hauji-*engage* kwa mujibu wa sheria. Atangaze tu Rais asione tabu, mpeni heshima Mhe. Rais awamalize na wao kuweza kutangazia.

Mhe. Mwenyekiti, lakini niseme mswada huu nchi yetu ya Zanzibar ni masikini, hili nilikubali na niliseme wazi, bajeti yake siku zote inakuwa haikidhi haja na leo tunaleta mswada kama huu kwa sababu ni mswada mzuri sana wa kujenga hali halisi ya nchi ya kukasimu madaraka na hili neno kukasimu madaraka mimi naona halijapatiwa mkazio, kwa sababu tunakasimu madaraka, lakini baadae tunakuja kugeuka. Sasa kile kitu ambacho mimi kinanishitua sana ni jambo zuri sana hasa tukiangalia sasa hivi kumuona Mheshimiwa wangu mstahiki Mmeya atapunguzwa angalau kazi za kwenda kupokea wageni. Kwa sababu sasa hivi tunamuweka humu na kuna mambo lazima nitafanya humu kidogo apatiwe *promote* nzuri, humu bado kuna mambo ambayo yamekosekana ya kuzidi kumjenga meya wetu, sio acheze na kiti tu meya.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kutokana na sheria hii sasa Mheshimiwa wangu meya kidogo atakuwa na rungu jepesi, mimi nitalifanya liwe zito ikiwa tutakubaliana kwa mujibu wa taratibu. Naomba sana Mhe. waziri kwa kuwa msikivu utaweza kunisikiliza.

Mhe.Mwenyekiti, mwenzangu alizungumza Mheshimiwa aliyepita alikizungumzia kifungu cha 38, mimi sina tatizo nacho na kwa kuwa sasa hivi Waheshimiwa wetu huwa masikini, huwa na manung'uniko wanakuwa hawana hata ile *pocket money* angalau ya kuweza kujikimu na familia na marafiki zao na waliowapigia kura. Kwa sababu unapokuwa unapigiwa kura basi na mwananchi anajua ki-*percentage* nacho kile kinatoka na wao wanaweza kusaidiwa na wao. Sasa diwani wetu wanakuwa hawana *percentage* hiyo, leo sheria hii imeweka katika hali nzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, nawaombea kila la kheri na hii mimi sina wasi wasi, sijui nani hatowezesha kuipitisha, naamini hivi na hasa leo Sharifu mwenyewe wa Mchangani nimesimama hapa inatiririka tu wala usiwe na wasiwasi Mhe. Waziri, itakwenda *smooth* kabisa. Masawazisho lazima yawepo kuna mambo mengine sheria kwa sababu wana sheria wako wa aina nyingi, kila mwanasheria anajua alipofikia katika *level* ya kuweza kusoma. Sasa hayo

mambo huona *challenge* kule unapokuwepo Mahakamani wakabishana mmoja akashindwa, mmoja akafanikisha na ndio hali halisi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, hili suala nikiingia katika ukurasa wa 234 hapa zimeainishwa kazi za Mheshimiwa wangu mstahiki meya. Lakini kuna kifungu kimoja hapa cha (e), kuwa msimamizi wa maamuzi yote yanayoamuliwa na Baraza. Hii ni moja ya heshima kubwa sana, kwa tafsiri yangu mimi huko nyuma kulikuwa kuna maamuzi na yeye meya anakuwa hashirikishwi, masikini ya Mungu anakuta watu wameshaingiza mikataba wanayoitaka wao wenyewe, hiyo ndio imeisha.

Lakini sasa hivi hapa anasema kuwa atakuwa msimamizi katika yale maamuzi, ina maana atayasimamia na aweze utekelezaji. Hakuna tatizo lakini bado sheria hii nyepesi sana sijaona sehemu ambayo atakuwa na kauli maana yake unajua kusimamia unasimamia tu ndio, lakini sijaona kifungu ambacho kitaweza kumpa yeye kauli, sijaona humu nimejaribu kutafuta kama nilivyosema ndio kwanza niko *page* ya nane inanisumbua sana.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. waziri, ndio nadhiri yake hii aliona, dah, hapa niwapatie watu, maana yake *chemistry* huwezi kuisomesha wakati wa saa saba, lakini na yeye Mhe. waziri, aliona *time* ambayo ya mwisho mwisho atuletee ili watu tumalize malize. Kwa *study* hiyo nakupenda sana, si mara ya kwanza hii kutufanya kama hivi, nakushukuru kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini mimi nataka kuona kuwa pamoja na haya mambo yaliyoainishwa pale Kiongozi wa Baraza yeye wetu Mwenyekiti, Mwakilishi mambo mengi tu lakini naona bado Mheshimiwa wangu mstahiki kwa sababu ni mtu ambaye ana uwezo sana, kwa sababu ni mstahiki wa wenzetu tulipokwenda huko nje tunaona jinsi gani huyu maana yake, mimi nashangaa kweli, unajua mstahiki wa Zanzibar bado tunamvunja moyo kusema la ukweli.

Sheria hizi hazijamuwekeza vizuri mstahiki wa Zanzibar anakuwa peke yake hana hata yule msimamizi hana *board guard*, sijui *facility* nyingine kama anapatiwa. Kwa kweli bado hatujamtendea haki kabisa. Mimi ningeomba kabisa tujenge misingi ya sheria hasa ya kuweza kumuonesha kama ni mstahiki hasa wa Zanzibar, *otherwise*, pengine vyovyote kwa sababu Mheshimiwa anapokuwa tayari majadiliano ya kimaendeleo na Kamati yake, lakini inakuwa bado inatakiwa iende katika *stage* nyingine, ikifika kule akaambiwa *no*, ina maana mstahiki hana kauli tena imekwisha hiyo.

Mimi sijakubaliana nalo hata kidogo, naomba sana mwanasheria hili neno "kidogo" limo kwenye *bracket* hapa nalitafuta ili niweze kumpatia stahiki

ambayo itaweza kumsaidia, kwa sababu sasa hivi mji wetu wa Zanzibar unamuangalia meya na watu wake. Sio kama anashindwa kuutengeneza mji wetu, lakini na mazingira ya sheria inambana ya kuweza kujitanua kuweza kufanya kazi zake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana tutoe uwezo wa miradi ambayo wanayoiamua wao watu wa Manispaa, basi hata wizara isiweze kutia mkono, hiyo wazi waachiwe wenyewe waunde bodi yao wenyewe, watafute wakandarasi wao wenyewe ili waweze kuleta haiba ya mji wetu. Lakini mambo yenyewe yakiwa ukasema na hili jambo ambalo mimi linanisikitisha sana Zanzibar, tunakosa maendeleo kwa sababu tunakuwa mahodari wa kuingilia kazi. Tunatunga sheria na baadae tunaingilia katika sheria.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini na ndio maana harakati za mswada huu kuletwa, lakini umebanwa banwa, bado mpeni nafasi meya muone muda huu uliobakia, hebu muacheni tuone pale Darajani kama hajapageuza pakawa nusu ya London kwa sababu Zanzibar nayo inaweza ikaitwa London, kwani London ni kitu gani? London si katika kuleta maendeleo ya nchi.

Sasa mimi naomba kwanza tuwape heshima hiyo, mwanasheria kitafutwe kipengele cha kumuweza mstahiki kuamua miradi yao bila ya kupita katika Serikali Kuu. Wakipitisha kwenye Serikali Kuu hakuna kinachofanyika na ndio tabia yetu, *Wallahi* jamani mimi kinanisikitisha sana maana yake kinani-*confuse* kweli kweli hasa akili inaniuma wakati mwingine mpaka hufika mahali nikakaa na nikajifungua, nauliza ni sababu gani? Watu wamesoma lakini tunafika mahali kutoa uamuzi tu wa kuleta maendeleo kwa kuwasaidia wananchi tunachukua muda mrefu, hata mimi ingekuwa sikusoma basi nisingechukua muda mrefu, ninaweza nikachukua dakika mbili, tatu au nne nikasema *go*, wacha waletwe wafadhili wafanye kazi hapo vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli na hii kwa sababu mstahiki hana rungu, namuomba sana Mhe. waziri, tuachie bwana kabisa ili waweze kufanya kazi zao kwa uaminifu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sheria hii najiuliza sheha wangu ninavyofahamu mimi kuanzia Serikali inaanzia mkoa na wilaya mpaka kwenye shehia. Sheria hii inani-*confuse* kweli, kusema la ukweli na ndio maana nikasema nachangia nitaiunga mkono, *of course*, baadhi ya maeneo naunga mkono sina tatizo nayo hata kidogo. Lakini inanishangaza, Mwenyekiti anachaguliwa hatokuwa na bendera huyu ya kupepea, kwa sababu sheha wangu tayari yeye ana bendera inapepea, halafu sheha humu inavyoonesha na yeye atakuwa Mjumbe katika Mabaraza hayo.

Hapo mimi naomba sana Mheshimiwa nisaidie fikra kwa sababu kichwa kinaniuma sana, kwa sababu nina *experience* ya kuhusu Wenyeviti wenzetu wanakuwa na bendera na wao kwenye mitaa yao. Sasa huyu sijui nae itakuwaje, zisije zikagongana hizi bendera kwenye hizo wadi zetu au kwenye shehia zetu akawemo na Mwenyekiti na yeye akaja akaweka bendera yake.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana hili suala uje unitatulie hapa kwa sababu sheha anaingia halafu twende na wakati sasa hivi pamoja na kuchaguliwa Mwenyekiti basi tutafute Wenyeviti kidogo wenye ujuzi, uwezo na kuona angalau hata kidogo sheria za kudanganya danganya wawe nazo kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sheria hizi ziwepo ziweze kutusaidia na hali halisi kabisa. Mhe. Mwenyekiti, na katika hali nyingine hata na masheha wetu sasa hivi nao kidogo tuwape taaluma za sheria ili ziendane na wao tuwape taaluma za sheria. Mimi inanishangaza unamkuta sheha hajui kama ule muhuri ni sheria anaidhinisha kwa mujibu wa sheria zake yeye alizopewa yeye, hafahamu hivyo na anaingia matatani kinyume na utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, hapo mimi naomba sana tuwape semina, ni hatari hii. Naomba sana hili suala ambalo kuwa nalo hili tuwape taaluma za msingi kabisa za kuweza kufanikisha hali halisi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii sasa hivi tunakwenda kwa sababu inakasimu madaraka na neno "kukasimu madaraka" ni neno kubwa sana, kuwa tayari ikiwa kama wilaya inapunguza mzigo wa utendaji wa kazi, ninavyofahamu hivyo kama Halmashauri inajipunguzia sasa hivi madaraka ya kazi. Kwa sababu haya Mabaraza ni washauri wakuu, lakini je, watakubalika?

Mhe. Mwenyekiti, nazungumza jumla jumla kama nilivyokwambia maana yake *page* ya nane ndiyo kwanza nimefika katika kusoma sijaumaliza kabisa ni kitu ambacho sio cha mchezo. Kwa hivyo, nazungumza jumla jumla tu na unikubalie hivyo hivyo jumla jumla.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa, una dakika sita za ziada.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Watajitokeza wengine huko, mimi nakuvutieni hapa. Sawa, nataka niheshimu wakati wako, kama nilivyokueleza nikushukuru kwa kunipa muda huo, ninaamini kuwa utaweza kuniongezea.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona humu vianzio lakini najiuliza bado hizi Serikali zangu za Mitaa na wao *funds* zao watapata wapi pamoja na kodi? Naomba sana, kodi sasa hivi zinaingiliana; *ZRB* anamwambia Halmashauri anakusanya kodi kinyume na utaratibu, sasa mimi hujiuliza. Lakini vile vile, ni njia gani

kuu, tukisema wangojee fedha za bajeti, ndiyo maana nikakwambia mswada huu mgumu kwa sababu leo hiyo haki niseme kama wapo Wakuu wa Mikoa wengine wana fedha za kuwapelekea jamii mimi sijawaona, kama wako, *it is okay,* wamepeleka labda televisheni siku hiyo, mimi wakati umenipita. Kwa sababu hawana fedha za kuweza kushusha chini kwa kupeleka kwenye maendeleo kwa jamii na pia, Mkuu wa Wilaya siku zote naye analia hivyo hivyo fedha hana, tajiri nani Halmashauri?

Sasa Halmashauri kuna mambo ambayo sheria hii au sheria nyengine itakayokuja itawazibia mianya kwa sababu sheria nyingi sana Zanzibar kitu ambacho kinanishangaza katika dunia hii, peke yake Zanzibar ina kodi zaidi ya 100, tutafika mahali wananchi tutawakama, mwisho wa habari tutawauwa ni sawasawa na kumkama ng'ombe maziwa mwisho utamtoa damu.

Sasa mimi nafikiria kuwa Serikali katika sheria hii sasa hivi ifanye kila hali katika kuanzisha vianzio ambavyo vitaweza kuweka katika fedha ambazo zitakazotiwa kwa wingi na kuruhusika kwa mujibu wa sheria wakikubaliana na *ZRB*.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie na kama nilivyosema kwamba leo sitokuwa na hoja kubwa sana kwa sababu huu mswada nimekubaliana nao kwa asilimia mia moja, sina tatizo nao. Leo hii kama ulivyosema Mheshimiwa bado sijaweza kuzungumza sana kutokana na hali yangu ambayo karibuni nimekwenda operesheni wa *goiter*. Kwa hiyo, naomba nimshukuru sana Mhe. waziri, pamoja na katibu wake, wakurugenzi na watendaji ili sheria hii wasiweze kuikalia ndani ya *briefcase,* wawaachie wenyewe waliotungiwa sheria hii. Huo ndio uhodari wangu wa kusema kuwa sheria hii iwaruhusu watendaji ambao tuliwakasimu madaraka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo, kwa machache nakwenda tena kusema naiunga mkono asilimia mia moja mswada huu. Ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, sasa ni nafasi ya Mhe. Salma Mohammed Ali.

**Mhe. Salma Mohammed Ali:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha wazima na tukaweza kufika hapa kutekeleza majukumu yetu.

Pili nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mswada huu muhimu. Lakini vile vile naomba niipongeze serikali kwa kuuleta mswada huu ambao tulikuwa tunaihimiza sana serikali uulete hapa Barazani. Pia nataka niilaumu serikali kwa kuuleta mswada huu katika hati ya dharura.

Mhe. Mwenyekiti, huu mswada ni muhimu sana wa mageuzi ya mfumo wa Serikali za Mitaa, masikitiko yangu ni kwamba, Serikali za Mitaa ina wadau wengi miongoni mwa wananchi wetu, hivyo serikali kuleta mswada huu katika hati ya dharura umetunyima fursa ya kushauriana na wananchi wetu. Kwa hivyo, tunaujadili hapa Barazani kutokana na maoni yetu sio maelezo ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa namuomba Mhe. Waziri nimuulize ni sababu ipi iliyofanya mswada huu uletwe hapa kwa hati ya dharura ya Rais?

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 5(3) kinasema hivi, naomba ninukuu:

"Mamlaka ya kila Baraza la Serikali ya Mtaa yatafanywa kwa kufuata demokrasia na uwakilishi wa taasisi za serikali zilizoanzishwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii".

Mhe. Mwenyekiti, ninaomba ufafanuzi kutoka kwa Mhe. Waziri, nini maana ya kifungu hiki? Je, kutakuwa na uchaguzi wa kuchagua Mamlaka ya Serikali ya Mtaa husika au vipi? Mimi binafsi nadhani hilo ni jambo la msingi hasa tukizingatia jirani zetu tu hapo Bara, pamoja na ukubwa wa nchi yao huwa wanafanya uchaguzi wa kuchagua Serikali za Mitaa, Serikali za Vijiji na Serikali za Vitongoji.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa tunaleta sheria ya mageuzi ya Serikali za Mitaa msingi muhimu ni demokrasia ifuate mkondo wake kwa kuanzisha uchaguzi huru na wa haki.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 225 kifungu cha 10 pameelezwa ngazi tatu za utawala za Serikali za Mitaa nazo naomba nizitaje.

(a) Jiji, Manispaa, Baraza la Mji na Halmashauri za Wilaya;
(b) Mabaraza ya Wadi: na
(c) Baraza la Shehia.

Hapa naomba nimuulize Mhe. Waziri Sheha ni kiongozi wa Serikali Kuu au Serikali za Mitaa? Ninavyojua mimi Sheha ni mwakilishi wa Serikali Kuu na ndio maana katika ofisi yake nyumba yake pakapepea bendera. Ikiwa ni hivyo, Baraza la Shehia haliwezi kuwa Serikali ya Mtaa.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa serikali inataka kuimarisha mfumo wa Serikali za Mitaa basi ni lazima iwe wazi isichanganye Serikali za Mitaa na Serikali Kuu.

*(Hapa palitokea hitilafu ya umeme kwa sekunde chache)*

**Mhe. Salma Mohammed Ali:** Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 230 kifungu cha 22 naomba nipate ufafanuzi, kifungu hiki kinahusu Wajumbe watakaounda Baraza la Mji. Katika kifungu cha (d) naomba nikinukuu kinasema kwamba:

"Madiwani wasiopungua kumi (10) ambao wanateuliwa na waziri...". Mwisho wa kunukuu.

Mhe. Mwenyekiti, hapa panahitaji ufafanuzi, ikiwa Baraza la Mji lina Wadi saba na wananchi wamechagua Madiwani wao saba na hapa Mhe. Waziri ana uwezo wa kuteuwa Madiwani 10. Je, nini maana yake? Baraza hilo la Mawaziri si litakuwa la Mhe. Waziri. Kwa kweli hapa naomba nipate ufafanuzi kidogo na katika kifungu hiki mimi sikubali

Mhe. Mwenyekiti, hapa napendekeza waziri awekewe asilimia ya uteuzi na asilimia hiyo isizidi asilimia 40 ya Madiwani watakaounda Baraza hilo. Ninashauri sana mamlaka ya uteuzi wa Mhe. Waziri yaangaliwe upya, kwa sababu mimi sijawahi kuona kama wale wanaoteuliwa huwa wanakuwa wengi kuliko waliochaguliwa.

Katika ukurasa wa 336 kifungu cha 38 naomba niipongeze serikali kwa kukubali ombi la Waheshimiwa Wawakilishi, Madiwani walipwe mshahara. Haikuwa hali ya kuridhisha kuona wananchi wanachagua Rais, Mwakilishii na Diwani, lakini Diwani akawa halipwi mshahara. Kwa kweli mimi hapa naipongeza sana serikali kuzingatia ile dhana na dhamira nzuri ya haki sawa kwa wote. Hapa ni lazima serikali tuipongeze mana hata hawa Madiwani sasa watawajibika kwa wananchi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 239 kifungu cha 43 kinahusiana na muundo wa Wadi. Mhe. Mwenyekiti, hapa pia nahitaji ufafanuzi, kwa nini wananchi hawakupewa nafasi ya kuunda Baraza?

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe hebu naomba fanya *clarification* ya kitu kimoja, pamoja na mswada wako ulionao lakini kuna *paper* ambayo Kamati iliifanyia kazi, kuna *amendment*. Sasa naomba mwende nazo sambamba hizi ili wale wanaotusikiliza waweze kupata kitu kilichokuwa sahihi. Kwenye mswada kuna suala la mshahara katika kifungu cha 38. Lakini katika *amendment* katika kifungu cha 30 ndani yake kimo cha 38 pale panazungumziwa suala la posho. Kwa hiyo, mshahara umeondoka linakuja suala la posho.

Sasa ningependa nitoe maelekezo hayo ili wale wanaotusikiliza waweze kufahamu isije ikaleta *contradiction* katika uelewa wao. Tuendelee Mhe. Salma Mohammed Ali.

**Mhe. Salma Mohammed Ali:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante, lakini kwanza mimi hiyo karatasi ya marekebisho sijaipata kwa hiyo, nafuata huu mswada tulionao. Na ikiwa ni hivyo, malalamiko yatabakia pale pale Madiwani wanahitaji kupata mshahara. Kwa sababu hilo posho hapo nyuma tukiambiwa kuna posho, lakini hilo posho pia hawakulipata kikawaida.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hiki cha 43 kinachohusu muundo Wa wadi apa panahitaji ufafanuzi kwa nini wananchihawakupewa nafasi yakuunda Baraza lao la Wadi. Hapa Mhe. Mwenyekiti, demokrasi haijapewa uzito na vile vile naomba nimuulize Mhe. Waziri je, Baraza la Wadi litakuwa na ofisi au ni nyumba ya Diwani kama iliyo kwa Sheha.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 240 kuna kifungu cha 47, 48, 49 na 50. Vifungu hivi havipaswi kuwemo katika Sheria hii ya Serikali za Mitaa, Shehia ni ngazi ya Serikali Kuu tusichanganye mambo.

Vile vile naomba nije katika Jadweli la Kwanza Nam. 1(d) linasema kwamba, Mabaraza ya Mji lazima yenye idadi ya wakaazi kuanzia 75,000 mpaka 149,000. Hivi sasa Zanzibar ina Mabaraza ya Mji matatu, Baraza la Mji la Wete, Baraza la Mji la Chake Chake na Baraza la Mji la Mkoani. Katika Mabaraza hayo matatu hakuna hata moja lenye wakaazi 75,000. Je, kupitishwa kwa sheria hii maana yake ni kuyafuta Mabaraza ya Mji yalioko Pemba?

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa ni hivyo, mimi siungi mkono sheria hii. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa muda wako kutoa maoni yangu hayo.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Salma Mohammed Ali, sasa ni nafasi ya Mhe. Farida Amour Mohammed na baadae Mhe. Fatma Mbarouk Said. Mhe. Farida Amour.

**Mhe. Farida Amour Mohammed:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu japo mdogo katika mswada huu. Kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kunipa afya njema na kusimama mbele ya Baraza hili nikiwa mzima.

Pili naomba nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Waziri kwa kuamua kutuletea mswada huu, ingawaje huu mswada umechelewa kidogo kwa

sababu mswada huu au sheria hii ni muhimu na ilikuwa ikipigiwa kelele muda mrefu sana. Lakini pia nimshukuru Mhe. Waziri au serikali kwa jumla kuona ipo haja ya kuleta sheria hii hapa ingawaje imeletwa sheria hii kwa hati ya dharura.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii ya mageuzi ya Serikali za Mitaa ni muhimu sana na inagusa maisha ya watu wetu. Hivyo basi, kushirikisha wananchi wetu kwa kupata maoni na michango mbali mbali ingekuwa ni jambo jema sana na ingekuwa jambo la maana na ingeipa hadhi hii sheria, lakini kuileta haraka haraka inaweza kupitishwa kwenye Baraza hili bila ya kupata maoni ya wananchi wetu ambao ndio watekelezaji wakuu wa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 13(4)(b) kinaeleza kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa ina uwezo wa kushitaki na kushitakiwa. Hili ni jambo zuri, lakini wasiwasi wangu ni uwezo wa baadhi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika ngazi za Wadi. Sasa hapa naomba niulize swali. Je, Mhe. Waziri serikali imejipanga vipi kuziimarisha mamlaka hizi katika kuhimili dhima ya kushtakiwa?

Mhe. Mwenyekiti, hapa panahitaji mafunzo, uelewa mzuri, tena mkubwa, vyenginevyo viongozi wetu wa mamlaka hizi watakuja kujishitukia wako jela. Mhe. Mwenyekiti, nitoe mfano, kwa sababu kuna matatizo mengi au utaratibu mbaya wa uuzaji wa viwanja, mashamba yanayofanywa na mamlaka za mitaa hivi sasa. Je, kupitishwa kwa sheria hii nini hatma ya watendaji wa mamlaka hizo ambazo kuwa zinafanya mambo hayo?

Mhe. Mwenyekiti, katika vifungu vinavyohusiana na muundo wa Serikali za Mitaa na kifungu kidogo kinachompa waziri uwezo wa uteuzi wa Madiwani kuongeza nguvu muundo wa mamlaka hizi.

Kwa mfano katika kuanzishwa Mabaraza ya Jiji, waziri katika kifungu cha 18(2) kapewa mamlaka ya kuteuwa Madiwani wasiozidi watano, katika kuanzishwa Mabaraza ya Manispaa waziri katika kifungu cha 20(1)(b) kapewa mamlaka ya kuteuwa Madiwani wasiozidi 10 na katika kuanzisha Baraza la Mji na Halmashauri za Wilaya waziri katika kifungu cha 22(1)(d) na katika kifungu cha 24(1)(d) waziri amepewa uwezo wa kuongeza Madiwani 10 katika kila eneo.

Mimi kwanza hapa nina wasi wasi nataka Mhe. Waziri aniweke sawa. Kwanza Madiwani hawa watatoka miongoni mwa hawa hawa Madiwani waliopo au uteuzi huu atautoa katika eneo lipi. Sasa Mhe. Waziri namuomba anieleze nini maana ya kifungu hiki, kwa sababu kwenye eneo la jiji kapewa mamlaka ya kuongeza madiwani watano, kwenye eneo dogo la Baraza la Mji

na Halmashauri za Wilaya kapewa mamlaka ya kuongeza Madiwani 10 kila eneo. Je, hapa si kwamba waziri anataka kuongeza Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya kupitia wateule wake?

Mhe. Mwenyekiti, katika muundo wa Serikali za Mitaa kuna viongozi ambao wamegawika katika sehemu mbili, viongozi wa Serikali za Mitaa wa sehemu za Mijini, yaani viongozi wa jiji; kiongozi wa Manispaa na viongozi wa Mabaraza ya Miji, hawa wanaitwa Meya. Sasa viongozi wa Serikali za Mitaa wa sehemu za mashamba ambao viongozi wao wa Halmasauri huwa wanaitwa Wenyeviti wa Halmashauri na kwa kimtazamo nahisi utendaji wao wa kazi ni mmoja isipokuwa ni majina tu, yule ni Meya, yule ni Mwenyekiti wa Halmashauri.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hapa kuna jambo linanitia wasiwasi kwenye mambo ya maslahi, hapa katajwa Meya kuwa atapata mshahara na maposho lakini sikuona eneo linalomuona Mwenyekiti wa Halmashauri kupata maslahi hayo. Sasa hapa namuomba Mhe. Waziri anipe maelezo ya kina yatakayonifanya kushawishika kuunga mkono sehemu hii, vyenginevyo nitakuwa siwezi kuunga mkono.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu watendaji wetu hawa wanafanya kwa pahala pamoja na ukiangalia katika makusanyo na utekelezaji wa shughuli zote ni moja. Sasa hapa ukiona hawa wa mjini yaani Meya analipwa mshahara na maposho lakini Mwenyekiti wa Halmashauri kwa sababu anatoka vijijini, mashamba hapewi kitu wakati yule ndiye aliye na haki hasa ya kupewa. Kwa sababu yeye katika huduma zake zote mwisho wake kwanza anahangaika vijijini kupitia eneo hadi eneo kufuatilia maslahi, kufuatilia mapato ambayo ndio yanayoimarisha zile Halmashauri zenyewe. Sasa hapa kuonekana kama huyu hana haki aliyopewa pale wala hakuingiziwa chochote, hili kwa kweli Mhe. Mwenyekiti itakuwa ni uonevu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu malalamiko ya Madiwani nimeiona hii fomu, ingawaje wewe uliizungumza Mhe. Salma Mohammed kidogo kumrekebisha kutokana na muono wako. Lakini mimi katika kuangalia kwangu huu mswada sikuona pahala ambapo Madiwani watapewa mshahara. Sasa bado kilio chetu cha Madiwani kiko pale pale, inaonekana kuna watu wataopewa mishahara ambao wataajiriwa, sasa hawa Madiwani wetu ambao wamechaguliwa kama alivyozungumza msemaji wa mwanzo hapa Mhe. Ali Salum Haji tumefanya chaguzi tano, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar, Mbunge, Mwakilishi na Diwani na kampeni kubwa na gharama zilizotumika.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kuwatoa hawa wenzetu Madiwani katika fungu tukawawekea wao kazi yao ni kupata posho la kikao ambacho kuwa ndani ya

kikao hicho wengine wanapewa shilingi 30,000; wengine hazifiki, wilaya nyengine ni tofauti; hebu Mhe. Waziri hapa naomba akija anipe maelezo na ufafanuzi mzuri angalau hawa Madiwani kama hamkuwawekea huo mshahara sasa hayo maposho muyaboreshe na yawe katika hali moja isiwe wilaya hii au Halmashauri hii wanapewa hiki, hawa wanapewa hiki, wakati makusanyo yanaonekana kila sehemu inakusanya mapato mengi.

Kwa hiyo, nakuomba Mhe. Waziri ulisimamie hili kwa kuwaona Madiwani wetu ambao na wao wana haki ya kupata haki hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema machache haya naunga mkono asilimia 60, lakini baada ya majibu mazuri naweza nikaongeza ikawa asilimia mia moja. Nashukuru.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mheshimiwa Farida na asilimia yako sitini. Sasa tunamkaribisha Mhe. Fatma Mbarouk Said na baadae Mhe. Marina Joel Thomas. Mhe. Fatma.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia machache katika Mswada huu wa Sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake mbali mbali Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya pamoja na Maafisa wake mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi Miswada hii huwa na madhumuni na sababu. Mhe. Mwenyekiti, madhumuni ya Mswada huu ni mazuri na napenda ninukuu kwamba kama ilivyosema:-

"Madhumuni na sababu kwamba kwa mujibu wa kifungu cha 120 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 imeazimia kuanzisha ubora wa ufanisi wa Serikali za Mitaa pia imeamua kwamba kwa mfumo wa Serikali za Mitaa wenye ufanisi ni ule wa kuwashirikisha watu katika ngazi za chini na utakaozingatia misingi ya utoaji wa madaraka ambao ni uhamasishaji wa majukumu ya kiutawala kwa kazi maalum za ngazi za chini za Kitaifa".

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba madhumuni ya Mswada huu ni mazuri kabisa ili inataka sasa Serikali kugatua madaraka kwa Serikali hizi za Mitaa. Mhe. Mwenyekiti, kama kawaida niwaombe wenzangu tupitishe Mswada huu tukosowe na tuuboreshe na mimi nasema kabla ya kuingia kwenye Mswada wenyewe naunga mkono Mswada huu na naomba wenzangu vile vile wauunge mkono Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, nikianza ndani ya Mswada huu kwenye sehemu ya pili misingi inayoongoza. Kuna mamlaka ya Serikali ya Mitaa ambayo inasema kifungu cha 3 (1) Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni ngazi za chini ya Serikali ya Zanzibar iliyo na idadi ya Mabaraza ya Serikali za Mitaa zilizo huru na kuanzishwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ni kubwa na kama walivyosema wenzangu kwa kweli huu Mswada ni mkubwa ni muhimu na ulikuwa unahitaji muda wa kutosha. Mimi napata faraja kwa kugatua madaraka kwa Serikali za Mitaa kwa ngazi naamini kama kutakuwa na uwajibikaji na uwezo. Basi tunaweza kuharakisha maendeleo ya Serikali hizo za Mitaa, na mimi nimesema kwamba sisi sote ni wadau. Kwa sababu sisi tuko mitaani na kama kutakuwa na maendeleo mitaani kwetu hata na sisi Wawakilishi vile vile tutaondoka na yale malalamiko ya wananchi wetu na misaada mingi itakuwa iko huku kwenye Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye hiyo sehemu ya pili yenye misingi inayoongoza nikienda kwenye kifungu cha 5 (1) Asili ya Serikali za Mitaa inasema kwamba:

"Mamlaka ya Serikali ya Mitaa itaendeshwa na watu na itafanya kazi zake kwa kuzingatia matakwa ya watu kwa kuzingatia na kufuata taratibu zilizoanishwa katika Sheria hii na Sheria nyengine yoyote inayotumika".

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba hapa kuna neno "watu" naomba hii watu kwa sababu kila mahala nimeona watu, watu. Lakini ningependekeza kusema kwamba Mamlaka ya Serikali za Mitaa itaendeshwa na itafanya kazi zake kwa kuzingatia matakwa ya watu kwa kuzingatia na kufuata taratibu zilizoainishwa katika Sheria hii na Sheria nyengine yoyote inayotumika. Vile vile niende kwenye kifungu cha 6 (1) kwenye sura hiyo hiyo sehemu hiyo ya pili ambayo inasema:-

"Mamlaka ya Serikali ya Mitaa itaongozwa na watu na itatekelezwa kwa mujibu wa matarajio ya watu kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa katika Sheria hii na Sheria nyengine zozote zinazotumika".

Vile vile napendekeza kwamba, "Mamlaka ya Serikali za Mitaa itaongozwa na watu", hapa hii watu vile vile iondoke na iseme kwamba:

"Mamlaka ya Serikali za Mitaa itaongozwa na itatekelezwa kwa mujibu wa matarajio ya watu kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa katika Sheria hii na Sheria nyengine zozote zinazotumika"

Vile vile kwenye kifungu cha 7 Malengo ya Serikali za Mitaa yatakuwa kwenye *Marginal note* Malengo ya Mamlaka ya Serikali ya Mitaa. Vile vile ningeomba isomeke:-

"Kukuza uwezo binafsi na kuhakikishwa ushirikishwaji wa jamii baada ya kusema kwamba ni watu na jamii. Basi ieleze kwamba kukuza uwezo binafsi na kuhakikisha ushirikishwaji wa jamii katika kusimamia Sheria na amri ya kukuza Demokrasia, Uwazi na Uwajibikaji wa Serikali ya Mitaa".

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele kifungu cha 8 kuna Misingi ya Utawala wa Serikali za Mitaa na inasema kwamba misingi ifuatayo ya Utawala wa Mtaa itakuwa ni misingi ya Kukasimu na Utoaji wa Madaraka ya mfumo wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika Zanzibar. Hii ni misingi madhubuti kwani ndani yake mna uwajibikaji, haki, uwazi, utawala wa sheria na utawala wa demokrasia.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda na kifungu namba 10 Serikali ya Mitaa itakuwa na ngazi tatu za utawala zifuatazo:-

(1) Mabaraza ya Wadi
(2) Mabaraza ya Shehia

Nilikuwa naomba Mhe. Waziri anisaidie Wajumbe wake ni akina nani na watapatikana vipi. Pengine kama nilivyosema huko mbele iko lakini kwa haraka haraka niliona hapa baada ya kuiona hii basi naomba kwamba alivyosema mwenzangu hapa Mhe. Makame Mshimba kama huu Mswada kwa kweli una vifungu vingi na vifungu muhimu, kwa hivyo nilitaka kujua hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu ya tatu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Serikali ya Mtaa pamoja na mambo yanayohusiana na hayo. Kifungu cha 13(1) Kutaanzishwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kila mamlaka ya mijini na maeneo ya vijijini. Kwa hivyo, kuna kifungu cha 3(a) Orodha ya Ngazi za Serikali za Mtaa zilizoainishwa na kufutwa katika Zanzibar. Ningependa Mhe. Mwenyekiti, isomeke kwamba:-

"Orodha ya Ngazi za Serikali ya Mitaa ilizo ainishwa au kufuta. Sasa hii katika Zanzibar naona iishie hapo. Orodha ya Ngazi za Serikali ya Mtaa ilizoainishwa au kufutwa".

Mhe. Mwenyekiti, nikienda ukurasa huo huo wa 226, Vigezo vya Kuanzishwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Waziri kwa ajili ya utelekezaji bora wa shughuli za Serikali ya Mitaa atazigawa mamlaka ya Serikali ya Mitaa katika viwango vitakavyotegemea vifuatavyo:-

Ukubwa wa Eneo
Idadi ya Watu
Uchumi wa Eneo Husika
Maslahi ya Pamoja ya Jamii, pamoja na Ufanisi ya Urahisi wa Utelekezaji wa Shughuli za Kiutwala.

Nilikuwa naomuomba Mhe. Waziri akija aniambie ukubwa huo wa eneo ni ukubwa gani, idadi ya watu ni idadi gani na kama nilivyosema pengine mbele huko iko lakini hilo nililiona na nikasema nimuulize Mhe. Waziri. Sehemu hiyo hiyo ya tatu nikienda kwenye kifungu 16 kuna utaratibu wa Uanzishwaji wa Mamlaka za Mtaa.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 2 kidogo kinasema kwamba:-

"Pale itakapokusudiwa kuanzishwa Mamlaka ya Mtaa katika Eneo au Maeneo yoyote Waziri angalau miezi mitatu kabla ya kutoa amri ya kuanzisha chini ya kifungu cha 14 cha Sheria hii atawajibika kwa kutoa *notes* na inaonesha kwamba kuna mambo mengine yanayofuata mbali mbali kuweko, atazitaka mamlaka zote zenye maslahi au watu walioathirika na uamuzi huo kuwasilisha kwake kwa maandishi pingamizi yoyote au maelezo mengineyo kwa namna atakavyoeleza na ndani ya muda".

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kidogo ile "angalau" maana yake angalau kwa kweli hili neno kwa kweli iwe moja kwa moja inampa ruhusu yeye Mhe. Waziri kufanya basi isomeke:-

"Pale itakapokusudiwa kuanzishwa Mamlaka ya Mtaa katika eneo au maeneo yoyote Waziri kabla ya kutoa amri ya kuanzisha chini ya kifungu cha 14 cha Sheria atawajibika kufanya hayo maamuzi".

Mhe. Mwenyekiti, nikienda sehemu ya 4 Muundo wa Kazi na Uwezo wa Serikali za Mitaa. Mhe. Mwenyekiti, nikienda kifungu cha 20 Kuanzisha Baraza la Manispaa ambalo litaundwa na Wajumbe wafuatao:-

"Kuanzishwa Muundo wa Baraza la Manispaa".

Mhe. Mwenyekiti, wanawake tunaweza, wanawake tunaweza tunaomba iwiano iwapo Meya atakuwa mwanamme basi Naibu Meya awe mwanamke.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hili nasema nalitilia mkazo kwamba hata juzi tulipokuwepo Dodoma tulitaka nafasi hizi za Uwiano kwamba ziwepo kwamba mwanamme akichukuwa nafasi moja kubwa basi nyengine achukuwe mwanamke na huu ndio mkakati wetu sisi wanawake tunasema kwa sababu ukimtangaliza mbele mwanamke basi unaleta maendeleo zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika sehemu hiyo hiyo ya nne kifungu cha 24 (1) Halmashauri ya Wilaya itakuwa na Wajumbe wafuatao:-

Mwenyekiti ambaye anachaguliwa miongoni mwa Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya. Ningeomba kwa sababu hii nikisema kwenye kiengereza kuna *Present tense*, kuna *Continuous* na kuna *Past*. Kwa hivyo, hapa Mwenyekiti, ambaye anachaguliwa mimi ningependa hapa ibadilike. Mwenyekiti ambaye atachaguliwa miongoni mwa madiwani wa Halmashauri ya Wilaya. Vile vile Makamu Mwenyekiti, imeandikwa anachaguliwa miongoni mwa Madiwani.
Vile vile naomba Makamu Mwenyekiti atachaguliwa miongoni mwa Madiwani.

Vile vile kifungu (d) kinasema: "Madiwani wasiopungua 10 ambao wanateuliwa..." na yeye hapo hapo watateuliwa na waziri. Halafu kuna angalau asilimia 40 wawe wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hatutaki angalau, nasema moja kwa moja asilimia 40 wawe wanawake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 26, bila kuathiri kazi zilizoainishwa za kila Serikali za Mitaa, Mabaraza ya Serikali ya Mtaa kwa jumla wafanyakazi kwa mujibu wa kazi zilizopewa kwa mujibu wa sheria sekta ya miongozo katika eneo la mamlaka yake kama ifuatavyo. Lakini kuna kifungu hapa kuweka kumbukumbu za vyombo vya biashara binafsi, boti za uvuvi na vyombo vyengine vyovyote vinavyofanya shughuli za baharini. Hii inatokana na sura hii hii ambayo ni mwendo wa uwezo wa Serikali za Mitaa. Hapa vimetajwa vyombo vya moto, marikwama na gari za ng'ombe.

Mhe. Mwenyekiti, hivi vyombo vya moto afadhali lakini hizi gari za ng'ombe nazo pia zimo katika mitaa?

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwenye kifungu (k) hapa kinasema kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaosababisha maudhi kwa mtu binafsi na maudhi kwa jamii. Ningependa vile vile hapa niondoe haya maudhi, maudhi ni jambo jengine. Lakini iingie kwamba, kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaosababisha kero kwa jamii inatosha.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuyazungumza hayo niende bado maana yake Mhe. Farida Amour hapa ananitia ari, ananambia niendelee. Kwa hivyo, niende na sehemu ya saba masharti ya fedha. Hiki ni kitengo muhimu Mhe. Mwenyekiti.

Nikienda kwenye kifungu cha 70 kinasema, kwa sharti la kuidhinishwa kwa waziri anayehusika na fedha, Mamlaka ya Serikali ya Mtaa inaweza kujipatia mapato kutokana na vyanzo vifuatavyo: Kuna (a) kodi, halafu kuna kodi ya mali ya Baraza. Hapa nataka vile vile isomeke, kodi ya mali za Baraza haitakuwa na mali moja najua kutakuwa na mali nyingi. Kwa hivyo, hapa kuwe na kodi ya mali za Baraza. Viwango vya mtaa lakini vile vile kuweko na nyengine kama uuzaji wa mali vianzio vya mapato hivyo, pia mabango ya matangazo ya biashara.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda ukurasa wa 251 kuna hiyo mipango ya fedha kuna bajeti hapo imeonyeshwa kwamba kutakuwa na bajeti, vile vile kutakuwa na ukaguzi ni jambo la msingi hili lazima kwenye mapato ya serikali au kwenye matumizi na mapato na hasa Taasisi za Serikali lazima kuwe na udhibiti na ukaguzi. Lakini vile vile ni kwamba udhibiti na ukaguzi lakini kabla ya ukaguzi kwanza kufungwe mahesabu, bila kufunga mahesabu ukaguzi utakuwa sio mzuri. Kwa hivyo, kuwe na ufungaji wa mahesabu na baadae ipate ukaguzi.

Vile vile la mwisho nimeona kwenye kifungu cha 80 bajeti ya ziada, *supplementary hii* ni *supplementary budget*. Anasema endapo yatatokea mazingira mapya au jambo linalohusu umma ambalo halikuingizwa katika ya Kamati ya Mipango ya Fedha, Uchumi na Maendeleo Mkurugenzi atawasilisha bajeti ya ziada au utengaji wa fedha wa Baraza kwa ajili ya kupata idhini.

Mimi nimuulize Mhe. Waziri supplementary hii ni jambo zito inapofikia hali hii. Je, niulize *authorize* zitapatikana wapi. Ni nani atakaye-*authorize* hiyo *supplementary*.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono Mswada huu asilimia mia kwa mia. Ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi).*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Fatma Mbarouk Said. Sasa ni nafasi ya Mhe. Marina Joel Thomas na baadae Mhe. Shadya Mohammed Suleiman.

**Mhe. Marina Joel Thomas:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa nafasi hii kuchangia Mswada huu. Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Baraza la Manispaa ya Nam. 3 ya 1995 na Sheria za Halmashauri za Wilaya

na Mabaraza ya Mji Nam. 4 na kuanzisha upya Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar ya 2014.

Mhe. Mwenyekiti, pia ninapenda kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uamuzi wake wa busara na kwa kukubali Mswada huu kuletwa katika Baraza lako tukufu. Mhe. Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu Mswada huu wa dharura umeletwa wakati muafaka na Rais anayo mamlaka hayo kutokana na majukumu yake. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, pia ninampongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri na yenye busara pamoja na Mwenyekiti wa Kamati kwa kuwasilisha taarifa hii ambayo imeboresha vipengele mbali mbali ambavyo kwa upande wao wameona pengine vinahitaji maboresho. Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi nimefurahishwa sana na Mswada huu na kwa sababu mimi nimetokea kwenye Wizara hii, nimefanya kazi karibu miaka 25, changamoto ninazijua tunazozipata kwenye Mikoa na Wilaya. Kwa hivyo nimefurahishwa sana kuletwa Mswada huu kwa sababu utakuwa ukombozi katika ngazi za Mikoa na Wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia Mikoa na Wilaya huwa wanaandaa mipango mizuri tu; mipango kazi mizuri lakini wanashindwa kutekeleza kutokana na uhaba wa fedha na kwa vile Serikali ilikuwa haijakasimu madaraka katika ngazi za Mikoa na Wilaya, utekelezaji wao unakuwa sio mzuri kutokana na uhaba wa fedha. Mhe. Mwenyekiti, lakini kutokana na Mswada huu kwa kweli Mikoa watafanya kazi nzuri, wataisimamia miradi ya maendeleo vizuri wataetekeleza kwa fasaha kwa sababu hata zile fedha wataingiziwa moja kwa moja katika ngazi ya Mikoa na Wilaya. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, na ukiangalia Mikoa na Wilaya pia ni Serikali. Serikali Kuu kuna Mawaziri wa sekta mbali mbali, elimu, afya, kilimo, mifugo, uvuvi lakini ukiangalia katika ngazi ya Mikoa na Wilaya, zipo sekta mbali mbali ambazo kama Serikali Kuu zipo. Kuna Maafisa wa Elimu, Maafisa wa Kilimo, Maafisa wa Uvuvi na hawa ndio wanaoisaidia Serikali Kuu kutekeleza yale majukumu ambayo yamo katika sekta husika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo Mswada huu umeletwa katika wakati muafaka, ijapokuwa umechelewa lakini pia haujachelewa sana na unaweza ukasaidia kuleta mabadiliko katika wananchi, kwa sababu Wilaya na Mikoa ndio wenye wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda sura ya nne. Hapa ninapenda nimpongeze Waziri kwa kuangalia, nimeangalia kila miundo katika Mswada huu. Kuna

muundo wa Serikali za Mitaa, Baraza la Manispaa, Baraza la Mji na muundo wa Halmashauri. Mhe. Mwenyekiti, katika miundo hii hapa ninampongeza Mhe. Waziri katika muundo kaweka asilimia 40 ya wanawake. Hii ninampongeza kwa sababu kama tulivyopigania katika Katiba yetu tunataka asilimia 50, lakini kuweka asilimia 40 nayo ni hatua. Kwa hivyo ninampongeza sana kwa kutujali wanawake, anajua uwezo wanawake ambao waliokuwa nao. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda katika ibara ya 40, kifungu hichi cha (c). Hapa wanasema kifungu cha (b) Afisa Mwandamizi angalau awe na elimu ya shahada ya kwanza katika fani ya uongozi, sheria, sayansi, mipango, uandishi na inaendelea kama ilivyo. Hapa nilikuwa naomba kifungu hichi kifutwe kwa sababu ukiangalia katika Sheria ya Utumishi, Afisa Mwandamizi anaelezwa vizuri tu na Utumishi ndiyo inamteuwa Afisa Mwandamizi. Na katika Sheria ya Utumishi inaeleza Afisa Mwandamizi awe na uzoefu huu, awe na elimu hii. Kwa hivyo ninahisi kikaa hapa kitakuwa kama kinapingana na Sheria ya Utumishi. Kwa hivyo ni bora tuache kifungu hichi kibaki katika sheria ile ile mama ya Utumishi na hapa naomba kiondoshwe.

Mhe. Mwenyekiti, jengine Mswada huu utakuwa ni chachu ya maendeleo katika nchi yetu. Ninasema hivyo kwa sababu shughuli nyingi nyingi za maendeleo zinafanywa katika ngazi za Mikoa na Wilaya na Wilaya ndio zenye watu, ndio Wilaya ndio zenye kusimamia mipango mbali mbali. Lakini Mswada huu pia utaleta chachu ya maendeleo kwa sababu watakuwa wanasimamia kikamilifu shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mswada huu utakuwa kiungo baina ya Serikali Kuu na Serikali ya Wilaya na Serikali za Shehia. Pia nilikuwa naomba Sheria ya Mswada huu ukipita ninamuomba Mhe. Waziri kuna suala zima ngazi za Mikoa na Wilaya zinataka ziimarike, licha ya fedha ambazo watatiliwa na Serikali Kuu lakini waweze kubuni mbinu mbali mbali vyanzo vipya vya mapato ambavyo vitaweza kusaidia Wilaya na Mikoa kuweza kutekeleza kazi zao kwa ufanisi zaidi na vile vyanzo vya mapato vyengine ambavyo vipo, ninamuomba Mhe. Waziri viboreshwe ili viweze kuzisaidia sana hizi Wilaya na Mikoa.

Mhe. Mwenyekiti, pia hapo hapo vyanzoambato hivyo namuomba Mhe.Waziri mapato yadhibitiwe. Vyanzo vya mapato vizidhibitiwe, tupunguze mianya ambayo inaweza ikasababishwa fedha zitumike ambavyo kinyume na taratibu ambazo zinakusudiwa. Kwa sababu Manispaa ina sehemu nyingi tu za mapato, kuna *parking* za magari lakini hasa kama mapato hizi Mhe. Mwenyekiti, hazitokuwa na usimamizi mzuri, lile lengo ambalo limekusudiwa kutekelezwa kwa fedha hizi hazitofikiwa ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi, naomba niishie hapo lakini Mswada huu umefika muafaka haujachelewa na Rais hakukosea kuleta Mswada huu wa dharura, ni jukumu lake. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono asilimia mia.

Ahsante sana. *(Makofi).*

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman**: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kuweza kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia machache katika Mswada huu uliokuwepo mbele yetu. Kwa ruhusa yako naomba uniruhusu kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kutuchagulia Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba na Mkuu wa Wilaya; wote hawa wakiwa akinamama. Tunasema wanawake tunaweza bila ya kuwezeshwa. Mhe. Rais hongera. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri kwa kutuletea Mswada huu baada ya muda mrefu tulikuwa tukishuhudia matatizo mengi ya mipaka baina ya Mjini na Magharibi. Kwa mfano huko nyuma kulikuwa na sokomoko la Soko la Mwanakwerekwe ambalo huko nyuma kila mmoja anasema yeye ndio mmiliki wa soko hilo. Hadi hii leo tunashuhudia kutokuwa na taswira nzuri ya upanuzi wa soko hilo. Mhe. Mwenyekiti, sasa kuja kwa Mswada huu matatizo mengi madogo yataondoka. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, naomba tena nishukuru na kuwataka akinamama wenzangu kuunga mkono Mswada huu kwa kuupitisha, kwa sababu kila unapoangalia uteuzi wa Madiwani basi umetoa kipa umbele kwa akinamama. Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano kifungu cha 18 (2) (e) na chengine ni kifungu cha 20 (1) (d). Mhe. Mwenyekiti, mazingira ya utendaji wa kazi yanaonekana kuwa yanapata ufanisi kwa ushirikiano baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano haya tumeona kule kwa wenzetu Tanzania Bara. Mbunge anaingia kwenye Baraza la Halmashauri, lakini sijaona kwenye Mswada huu unaoonesha Mwakilishi kuingia katika Mabaraza hayo. Mhe. Mwenyekiti, ingawa kuna kauli inasema Manispaa zetu zina Wawakilishi wengi, zaidi ya mmoja. Lakini ni vyema Mhe. Mwenyekiti, tukatengeneza utaratibu wa kumchagua miongoni mwao kumpata Mwakilishi mmoja ambaye ataweza kutuwakilisha katika Baraza la Madiwani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano kama tulivyotumia utaratibu huu wa kuchagua Wawakilishi watano kutuwakilisha kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo kama nilivyosema awali mchango wangu mimi utakuwa sio mkubwa, baada ya hayo maneno machache, naomba

Waheshimiwa wenzangu wauchangie Mswada huu na kuuboresha na hatimaye kuupitisha.

Baada ya hayo kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba ninaunga mkono kwa asilimia mia Mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi).*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Shadya. Majadiliano na michango inaendelea. Mhe. Abdalla Mohammed Ali.

**Mhe. Abdalla Mohammed Ali:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nishukuru asubuhi hii kunipatia fursa ya kusema machache katika Mswada huu uliopo mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba tumekuwa mahodari sana wa kutunga sheria mbali mbali, lakini tumekuwa wapungufu sana wa kuzitekeleza sheria hizi. Mhe. Mwenyekiti, kumbukumbu zinaonesha kwamba katika kikao chetu cha bajeti mara hii tuliisakama sana na kulizungumza sana Baraza la Manispaa na tulifanya hivyo kwa kujua kwamba kuna ukweli usiofichika kwamba kazi za Baraza hili zimedorora. Kumbukumbu pia zinaonesha kwamba Baraza lako tukufu liliunda Tume Teule kwa ajili ya kuchunguza Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, sasa yote haya yanaonesha kwamba sheria zetu zina mapungufu makubwa. Sasa la kushangaza kwamba tunataka kuongeza mzigo mwengine kwamba hili Baraza ambapo hivi sasa tunalitegemea lifanye kazi zake kwa ufanisi, lakini limeshindwa, tunaongeza mambo mengine ambayo yanahisi yatakuwa ni mzigo na utekelezaji wake Mhe. Mwenyekiti, sifikirii kwamba kutakuwa na ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwa hili Baraza la Manispaa ambalo katika kifungu cha 21 limepewa kazi maalum na moja kati ya kazi hizo ni utoaji wa leseni. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tuna vitengo tofauti au tuna Idara tofauti ambazo zinasimamia utoaji wa leseni. Lakini kifungu hichi cha 21 Mhe. Mwenyekiti, hakikueleza kwa undani leseni hizi ambazo zitasimamiwa na Baraza la Manispaa ni leseni za aina gani. Sasa ningependa Mhe. Waziri atakapokuja labda akatwambia ili kuondosha huu mgongano ambao nina imani hivi sasa upo kwa kujua mapato haya yatakusanywa nani, Idara gani na mapato haya yatakusanywa na Idara gani. Sasa je, hawa Manispaa wao jukumu lao la kukusanya kodi kutokana na leseni ni leseni zipi zitakazokuwa chini ya Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimejenga wasi wasi kidogo na wasi wasi wangu unakuja hapa alipopewa Waziri wa kuteuliwa Madiwani kumi. Mhe. Mwenyekiti, sisi imani yangu ni kwamba tunataka kutanua demokrasia na kutanua demokrasia ni kuwapa wananchi maamuzi. Lakini hapa ninahisi kwamba maamuzi hayo wananchi watakuwa hawanayo. Leo kumpa Waziri mamlaka ya kusema yeye ateuwe Madiwani kumi. Mhe. Mwenyekiti, ninahisi kwamba sasa hapa tunasema kazi za Mabaraza, kazi za Halmashauri, kazi za hayo Mabaraza ya Vijiji yatakuwa wao ni kusikilia amri kutoka Serikali kuu, na wao hawatokuwa na mamlaka yoyote ile.

Mhe. Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba hakuna Baraza litakalokuwa na Madiwani wa kuteuliwa watakaozidi kumi, lakini hapa, wa kuchaguliwa samahani, lakini hapa amepewa fursa Waziri ya kuwazidi wale Madiwani ambao wamechaguliwa na wananchi, badala yake wa kuteuliwa na Waziri watakuwa ni wengi zaidi. Sasa sijui hasa nia hapa ni nini na hapa ndipo ninasema mimi siwezi kuunga mkono hoja hii. Kwa sababu undani wa suala hili mimi siufahamu. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze kwa kina ni sababu gani za msingi za kuwa na mamlaka haya ya kuteuwa watu kumi yeye wakasimamia wananchi huko wa kutoa maamuzi yao.

Mhe. Mwenyekiti, watu hawa mimi ninasema watakuwa ni watumwa kwa aliyewateuwa. Kwa hivyo hawatokuwa na nia yoyote ile ya kuwatumikia wananchi. Sasa mimi ninahisi angetupa maelezo ni kwa nini hapa tukaweka sheria hii wa kuteuwa watu hawa na sio kuchaguliwa na wananchi wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, labda niendelee kidogo tu kwenye makosa na adhabu. Sheria hii imekuja zaidi kwa ajili ya kuleta maendeleo ya kiuchumi na imetoa fursa kwa Mabaraza na Halmashauri kwa kukusanya kodi ndogo ndogo. Lakini leo imetoa fursa kwa adhabu ya mwananchi ambaye labda atashindwa kulipa kodi yake na adhabu yenyewe inakuwa ni kifungo kisichopungua labda mwezi mmoja. Mimi ninafikiri ikiwa lengo kubwa hasa ni kuwawezesha wananchi kukusanya mapato na kuweza kuyatumia katika maendeleo yao, hizi adhabu tungeziondosha.

Hivi sasa utaratibu uliopo wa *ZRB* ambacho ni chombo kikuu cha kukusanya kodi katika nchi hii, wao hufanya utaratibu wa kufunga maduka, wakiona yule ambaye wanamdai hayakamilisha taratibu zake. Sasa na sisi tungeliiga utaratibu huo, tusingeliweka adhabu ya kifungo, tungempa fursa huyu mwananchi ya kutafuta ili kesho alipe hii kodi. Lakini tukisema tunamfunga, ina maana na duka lake itabidi lifungwe asiwepo. Kwa hivyo halitokuwa na uwezo wa kuzalisha.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni kwamba Kamati za Ushauri za Sheha au Shehia, zimepewa fursa ya kuwa na wataalamu. Lakini je, wataalamu hawa hawakuelezwa watakuwa ni wataalamu wenye sifa gani. Kwa hivyo ningependa tu kumuomba Mhe. Waziri atakapokuja akanieleza ili huko katika uchaguzi au uteuzi kusije kukazuka malumbano baina ya wananchi wenyewe kwa wenyewe. Je, hawa wataalamu ambao wanatakiwa wawemo katika Shehia zetu ni wataalamu watakaokuwa na sifa gani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache mimi siungi mkono hoja hii mpaka Mhe. Waziri atakaponipa maelezo, kwa nini Madiwani hawa 10 awateuwe yeye na wasiteuliwe na wananchi. Nakushukuru.

**Mhe. Asha Bakar Makame:** Mhe. Mwenyekiti, kabla ya yote na mimi nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha tena siku ya leo kufika hapa katika Baraza lako tukufu hili tukiwa wenye afya njema.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Waziri, pamoja na watendaji wake wote ambao wametuandalia mswada huu. Pia nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambaye ameona kuna wajibu wa kuletwa mswada huu kwa dharura, ili kukamilisha malengo na matakwa ya mswada huu.

Lakini na mimi vile vile nichukuwe nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kututeulia wanawake ambaye mmoja ni Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Mwanajuma Majid na Hanuna Masoud ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake. Hii yote ni kuonesha kwamba wanawake tunaweza hatuwezeshwi. Tunaweza kwa sababu amewaweka wote wawili pahala pamoja. Kwa hivyo, nitowe tu pongezi za dhati na niwaombee dua ili waweze kufanyakazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, huu mswada ukiuangalia ni mzuri sana, lakini nitamuomba Mhe. Waziri, kwa sababu huwa tunaleta miswada mbali mbali hapa, lakini utekelezaji wake ndio matatizo. Sasa mswada huu ni wa roho ya wananchi, nathubutu kusema hivyo, kwa sababu ni mswada ambao utaleta maendeleo yao katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwanza wale wote ambao kwa mujibu wa mswada huu watateuliwa au watachaguliwa, naomba wawe na uwezo wa hali ya juu kabisa, ili tusije tena tukaona mambo yanakwenda shaghala baghala. Hilo moja.

Jengine hii asilimia 40 ya akina mama nimpongeze pia Mhe. Waziri. Lakini mimi naona bora tungeweka asilimia 50 ili tukaweza kufidia yale mambo ambayo huko mbele tunakwenda nayo. Sasa ili tuuweke mswada huu katika hali nzuri, sio mbaya asilimia 40, lakini ni vizuri asilimia 50 ikaanza kufanyakazi kwa sababu tunaupitisha hivi sasa huu mswada.

Pia niseme, sio wanawake tu, ni wanawake wenye uwezo. Tusichukuwe kwa sababu ni asilimia 40 tukachukua wanawake tu. Namuomba sana Mhe. Waziri, wanawake wenye upeo na uwezo wa kusaidia mswada huu, ili kurekebisha yale mambo madogo madogo ambayo yatajitokeza baadaye.

Nikimalizia hapo Mhe. Mwenyekiti, niseme kuwa utekelezaji na ufanisi ndiyo muhimu katika mswada huu. Nikija kwenye kifungu namba 21 cha mswada huu, kuanzia (a) mpaka (i) ni mambo muhimu sana yaliyotajwa katika mswada huu. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kwamba mambo haya kwa kweli yatekelezwe ipasavyo, hasa katika hizi *by laws* ambazo wamesema kwamba watatunga sheria ndogo ndogo. Sheria ndogo ndogo haina maana tukiziita sheria ndogo ndogo zisifanye kazi zake Mhe. Mwenyekiti. Sheria ndogo ndogo ndio zinazofanya ufanisi zaidi kuhakikisha kwamba hizi sheria ndogo ndogo ndio zinazoleta tija katika shughuli zetu zote.

Mhe. Mwenyekiti, naamuomba sana Mhe. Waziri kwamba hizi sheria ndogo ndogo ziwe na kiwango, na kiwango hicho kiweze kutosheleza mahitaji ya wale watu ambao wanatungiwa sheria ndogo ndogo. Lakini pia niseme tu sheria yoyote ile lazima impe mamlaka waziri. Kwa hivyo, mimi naunga mkono kwamba waziri anapata mamlaka ya kuchagua katika watendaji, wafanyakazi na kuchagua kama mswada huu unavyoeleza.

Mhe. Mwenyekiti, huko nyuma tulikuwa tunawaona Madiwani walikuwa wanachaguliwa na nani, katika wale wa kuteuliwa. Lakini na hapa mimi nimwambie tu Mhe. Waziri katika hao Madiwani 10 atakaowateuwa, aweke 50 kwa 50. Madiwani watano wawe wanaume na Madiwani watano wawe wanawake, ili twende sambamba na huko mbele tunakokwendea.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu wenzangu wamechangia sana mswada huu, na mimi niunge mkono mswada huu asilimia mia kwa mia ili tuweze kuupitisha na kuweza kutekeleza majukumu ya wananchi wa Zanzibar. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi niitumie fursa hii kufanya mambo yafuatayo. Mhe. Mwenyekiti, la kwanza nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika siku ya leo tukiwa hai na hatimaye kutujaalia nguvu na uwezo wa kutoka katika maeneo

yetu, wengine wanatoka Kijitoupele, wengine wanatoka Mwanyanya na wengine wapi. Tena wametoka katika maeneo hayo bila ya kushikiliwa mpaka katika jengo hili, hii ni hazina kubwa aliyotujaalia *Allah* na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Mhe. Mwenyekiti, mara baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nadhani sitaifanyia haki serikali kama nayo sikuishukuru kwa kuweza kuleta kitu kama hiki wakati huu. Kwa kweli mswada huu kuletwa hapa Barazani, serikali imesibu ile dhana ya utekelezaji wa utawala bora katika nchi yetu. Kwa hivyo, kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo langu la Wawi, nasema ahsante sana serikali kwa kuweza kutuletea kitu kama hiki.

Lakini kabla sijaingia katika mswada huu Mhe. Mwenyekiti, vile vile nitakuwa nimekunyima haki yako, kama sikutumia fursa hii kukushukuru. Tena nashukuru sana kwa sababu hata ki- *memo* sikuleta cha kukuomba kuchangia, wewe umenitaja. Kwa hivyo, nashukuru sana kwa mapenzi yako Mheshimiwa ya kuniteuwa mimi kuchangia hili. Kwa hivyo, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi Mhe. Mwenyekiti nasema ahsante sana. *(Makofi).*

**Mhe. Mwenyekiti:** Lakini Mhe. Mjumbe ulinyoosha mkono ndiyo maana nikakupa nafasi. Endelea. *(Kicheko)*

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nchi yoyote iliyosaini mkataba wa utawala bora kama tulivyo sisi Tanzania na hapa Zanzibar haina budi kuimarisha Serikali zake za Mitaa. Kwa kweli katika kipindi kirefu hiki, kwa masikitiko makubwa Serikali za Mitaa katika nchi yetu zilikuwa butu au zilikuwa hazipo kabisa Mheshimiwa, kwa sababu walikuwa wakifanyakazi huku wakiwa wananyooshewa msuli na hili jiserikali kuu, jambo ambalo kwa kiasi fulani sana Serikali za Mitaa zilikuwa dhaifu sana.

Sasa kuletwa kwa mswada huu Waheshimiwa na serikali, nina imani kwamba ni kuzifufua Serikali za Mitaa na kupanua demokrasia katika nchi yetu. Kwa hivyo, naipongeza serikali yetu hii inayoongozwa na Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa kuweza kuleta kitu hiki.

Mhe. Mwenyekiti, lengo la serikali kuleta mswada huu ni ku- *broaden democracy within the Islands.* Nakusudia ni kupanua demokrasia katika nchi. Ili serikali hizi ziwe madhubuti Mheshimiwa hapana budi watendaji na washiriki katika serikali hii wawe na uwezo wa kutosha katika kufanya shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, wakati naangalia hapa kwenye mswada huu niliona kwamba Madiwani wangelipwa mshahara, mswada huu bila ya mabadiliko. Lakini baada ya mabadiliko, yale mabadiliko sikuyapata nasikia watakuwa wanapata posho la vikao Madiwani wetu. Kama ni kweli nadhani waziri atakuja kunipa ufafanuzi hapa, ile *schedule of amendment* mimi sikuipata hapa. Lakini kama tuseme Madiwani wetu hawakupata mishahara basi hii ni kupunguza nguvu kwa kiasi kikubwa, kwa sababu hawa ni watendaji. Posho tu la shilingi 30,000 baada ya miezi miwili halisaidii kitu. Hawa wanahitaji walipwe mishahara tena mishahara ya kutosha kabisa, kwa sababu hawa ni wawakilishi wa wananchi.

Unapomdhalilisha Diwani mmoja katika nchi, basi umeidhalilisha Wadi nzima. Sasa hivi kuna Miji mingi imeingia *sister-ship* Waheshimiwa Wawakilishi nataka munifahamu kwamba kuna *sister-ship* baina ya Mji fulani na Mji fulani. Hivi sasa mimi Mji wangu wa Chake Chake ule unataka ku-*create sister-ship* na Mji kama ule wa Copenhagen, unataka ku-*create sister-ship* za Miji kama ile ya Deira pale Dubei. Unataka ku-*create sister-ship* za Miji kadhaa ya Ulaya. Sasa inasikitisha sana Mhe. Mwenyekiti, kwamba Diwani hana uwezo, hawezi ku-*afford* hata kupata suti ya kuingilia katika kikao cha kawaida cha Halmashauri. Unamkuta Diwani kavaa yebo yebo pamoja na shati hizi za kawaida anaingia katika vikao vikubwa sana, sio aibu ya Diwani ile ni aibu ya nchi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana serikali ifute aibu ya nchi kwa kuwapa maslahi mazuri Madiwani wetu ili watakaposhiriki katika ile *sister-ship meetings.* Kwa mfano, wale wanaokwenda Chake Chake pale wanakwenda Copenhagen karibuni hivi, basi waweze kula suti na kuuramba sawa sawa huku wakiwa na *mucus* na sio yebo yebo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea hivi sasa wakati yule Meya wa Copenhagen anakula suti pamoja na joho lililonakishiwa kwa mirinda ile ya dhahabu, lulu na yakuti. Basi Meya wetu wa Mji wa Chake Chake hata lile koti kama waliyokuwa wakivaa Wenyeviti wetu wa Afro Shiraz siku zile, akina Said Yakuti na Suleiman Rihami, hawamudu hawa Madiwani wetu. Sasa mimi nilikuwa naomba kwamba tuwafanye Madiwani wetu, wawe na wao. Sisi unaona hivi nilivyopendeza hapa angalau tunaezeshwa ndio sababu tunapata kununua suti. Wale wamechaguliwa ni sawa sawa na sisi Mhe. Waziri, tulisimama nao. Mimi naingia huku wakati nimekula suti safi hii, hata huku Kusini mwa Jangwa la Sahara haipatikani suti kama hii. Lakini Madiwani hawamudu hata kupata koti. Koti walilokuwa wakitumia Wenyeviti wao wale, wakiitwa ma-*chairmen* wa Afro Shiraz, hawawezi ku- *afford*.

Mhe. Mwenyekiti, huku ni kumdhalilisha Diwani wetu, mimi naomba kwamba katika ku-*strengthen* Halmashauri zetu hawa Madiwani waweze ku-*participate well,* sio katika vikao tu hivi vya hivi *local meetings,* lakini hata *International Meeting*. Hivi karibuni Mwenyekiti wangu wa Halmashauri ya Mji wa Chake Chake alikwenda Korea kutembelea, ikabidi tumuazime buti pamoja na kumfundisha kuvaa koti, kwa sababu tatizo, tujitahidini kuinua maslahi yao. Hata kufunga tai wanakuwa hawawezi kwa sababu hatuwawezeshi, tuwawezesheni waweze kupata tai, waweze kufunga tai, ile tai akiinunua hawezi kufunga basi wapewe semina za kuwa *smart.* Madiwani wetu wanapokwenda katika *International Community* ndio nchi yetu imekuwa *smart* jamani, msitudhalilishe huu ni mwaka wa ngapi, ni mwaka wa 50 tangu tupate uhuru. Kama ni mtoto aliyezaliwa mwaka wa 50 keshajukuu, haya jamani uwezo huo hatuna sisi, hatukui sisi serikali yetu haikui ni kokoto, kokoto ndio iliyokuwa haikui zaidi ya hapo hapo miaka yote. Serikali inakuwa na Madiwani wetu tuwawezeshe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya dibaji hiyo niendelee kwenye vyanzo vya mapato. Ili hizi Serikali za Mitaa ziwe makini, sio tu katika kuboresha na kuwaweka vizuri Madiwani wetu, kuna mambo mengine lazima tuwaachie. Kila chanzo kitachukuliwa na Serikali Kuu, Vyenzo vyengine ni lazima waachiwe hizi Serikali za Mitaa ili wajenge uwezo na wao wa kuweza kujisimamia mapato, sio kila jambo Serikali Kuu ikusanye yeye na hii isikusanye yeye. Serikali za Mitaa nazo ziachiwe Mhe. Mwenyekiti, baadhi ya vyanzo ili ku- *strengthen capacity.*

Mhe. Mwenyekiti, niende katika sehemu ya pili ya huu mswada. Katika kuimarisha demokrasia Mhe. Mwenyekiti na Utawala Bora ndiyo Serikali imeleta huu Mswada. Lakini sasa mimi napata tatizo katika kifungu nambari 4, eneo la Mamlaka ya Serikali za Mitaa nambari 4(1). Kwa masharti ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na vifungu vya sheria hii waziri atapopeleka kwa Rais kuigawa Zanzibar katika idadi ya Serikali za Mitaa. Ingekuwa tuko Saudi Arabia au ingekuwa tuko Uingereza basi haya maelezo ningeyaachia tu hivi hivi, kwa sababu wale wanafuata *monarchy,* sisi tunafuata demokrasia.

Sasa kumuacha tu waziri yeye mwenyewe akawa anapanga leo nataka nikate hivi na kesho nikate hivi, anataka amshauri Rais. Mimi nadhani waziri tusimuachie yote hayo, aweze kufanya *concurrence with* wale Madiwani ambao wamo katika Mabaraza ya Miji ile Manispaa, *a concurred* sio akae tu hivi afikirie au ashauriwe na mtaalamu. Mimi nadhani aidha, kwanza afanye *concurrence with* a hawa Madiwani wetu waliomo katika Manispaa au Mabaraza ya Miji au Halmashauri za Wilaya, ndio aweze kukatakata vipande kuweka sawa mipaka na kufanya nini, asiachiwe tu. Ikiwa hilo anaona tabu.

Mhe. Mwenyekiti, nakuomba unisikilize vizuri sana katika hili. Ikiwa waziri anaona tabu ku-*concur* na Mabaraza ya Miji katika kuweka mipaka na kuweka sawa hii, basi a-*make concurrence with leaders of political parties,* ambao wana Madiwani wao mule katika Baraza. Unaweza ukaniita mimi kama Katibu wa Wilaya pale wa CUF, ukamwita na Katibu wa Wilaya wa Chama cha Mapinduzi, sio tuliokuwa na Madiwani mule tukaja tukakaa na waziri tuka-*share mind* pale, halafu ndio akaenda kwa Rais. Asitoke tu moja kwa moja akaenda yeye. Hii itakuwa ana-*minimize democracy with the eyesless* na ile dhana ya utawala bora na demokrasia itakuwa tumeibana. Hayo ndio mawazo yangu katika hili.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nimeangalia kifungu cha 13(3)(a) mpaka (c). Kifungu 14(1) vile vile ni kwamba kuna uteuzi wa madiwani 10 watakaounda katika Halmashauri pamoja na Manispaa. Mhe. Mwenyekiti, hii ninapata tatizo sana katika hili, kwa sababu lengo letu ni ku-*broaden democracy* . Kwa mfano, Baraza la Mji wa Chakechake lina madiwani saba, ambao ni *elected*, yaani hawa *elected councils* saba waliochaguliwa na wananchi pia kuna wale *appointed*, ambao wamekuwa-*appointed according to the number of this within the council*.

Sasa unapopeleka madiwani 10 ukamuachia tu waziri ateue madiwani 10 hivi hivi, mwelekeo wetu tunaelekea wapi, hivi ni kupanua au kubana demokrasia katika nchi. Mhe. Mwenyekiti, ndio nikasema mambo kama yalikuwa yawemo kwenye *Monarchy System*, lakini katika *Democratic System* kama Zanzibar *it is unfair* kumpa waziri mamlaka ya kuteua watu 10.

Kwa hiyo, hii naona iondoshwe moja kwa moja haifai hii, isipokuwa patafutwe mpango mwengine. Kwa mfano, kama mimi nikiwa waziri naona kama mara hii hwenda nikawa waziri nitakayeshughulikia mambo haya, sasa nikija nikipewa hii nakwenda kumchukua baba yangu mdogo nampa, namchukua shemegi yangu mmoja nampa, namchukua na rafiki yangu pale mmoja nampa. Sasa hili ni tatizo *this is not a democracy*. *So what I'm saying* Mhe. Mwenyekiti katika hili, yaani hichi kiondoshe kabisa na hawa 10 waondoshwe.

Mhe. Waziri akiwa anataka hizi nafasi 10 azitoe kama *according to the number this political parties having within the council*, kama ilivyo humu kwenye Baraza hili, yaani itoke kwa *percentage* ya uwiano wa vyama vilivyomo katika *council* ile na wala asiachiwe kuchagua ndugu zake, baba zake wadogo, mama zake wadogo, mashangazi zake, ni tatizo. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Saleh Nassor Juma.

Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea. Mhe. Hamad Masoud Hamad.

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza kidogo kuhusu mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki nitafune maneno, lakini mswada huu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili wamegaiwa jana na umekuja kwa Hati ya Dharura, naweza nikatafsiri kwa nini umeletwa kwa Hati ya Dharura na umepatikana jana au juzi.

Mhe. Mwenyekiti, hakuna mswada mbaya kama huu na mimi ninaupinga kwa asilimia mia moja. Kwa mfano, amesema Mhe. Saleh Nassor Juma hapa kwamba madiwani saba wa kuchaguliwa katika uchaguzi wa papatu na halafu waziri analeta 10, maana yake ni kuwadhibiti wale saba ndio maana yake na hilo Baraza haliendi hata hatua moja kimaendeleo.

Kwa kweli, hao 10 watakaoletwa ni anaotaka waziri na wala hamna vigezo humu vya kuteua watu 10, Baraza hili lina Waheshimiwa Wajumbe 50 wa kuchaguliwa, kuna viti maalum sijui 20 au 25 kwa ujumla ni 70, lakini Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza wa kuteuliwa ni 10 tu na leo watu saba unakwenda kuwachanganya na watu 10 maana yake nini.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu naupinga kwa asilimia 100 na badala yake mswada huu urudishwe na tupewe muda wa kutosha wa Baraza lijalo tuje tujadili. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe.Hamad Masoud Hamad. Mhe. Mussa Ali Hassan na baadaye Mhe. Salmin Awadh Salmin.

**Mhe. Mussa Ali Hassan:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar ya mwaka 2014.

Kwa kweli, Mhe. Mwenyekiti sina budi nimshukuru Rais wa Zanzibar Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuweza kutuletea mswada huu kwa wakati, ili tujadili hali ya kuweza kuwa na Serikali za Mitaa kwa wakati ambao iko haja ya kuhakikisha kwamba tunapata madiwani katika sehemu hii ambayo ni nzuri zaidi, kuhakikisha kuipa nguvu Serikali ya Mitaa.

Vile vile kuhakikisha kwamba Serikali ya Mitaa inaweza kujitegemea katika sehemu zake ama shehia ambazo zinahitajika kuwa na madiwani wengi

kwenye Baraza la Manispaa, kuhakikisha kwamba sehemu zote ambazo zinaleta mapato basi zimetimia wahusika, ili kufanikisha kuwa nchi yetu inaleta maendeleo kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi kumpongeza Mhe. Waziri kwa kufanikisha kupanga ratiba hii ya kuhakikisha kwamba Manispaa zetu zinapata madiwani wengi, ambao wanaweza kukaa na wenzao ambao wamepangwa katika shehia, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mapato hayapenyi na kupelekea wizara zote au shehia zinaweza kujiletea maendeleo.

Kwa hivyo, sehemu nyingi ambazo shehia hazina madiwani wenye kutosha, basi mapato kwa sasa yanapenya na kupelekea nchi badala ya kusonga mbele utakuta kwamba nchi inazorota na mapato katika sehemu nyingi hatuwezi kupata maendeleo. Kwa mfano, utakuta jiji letu halina uhakika wa usafi wala masuala ya kuwa na maendeleo ya sehemu nyingi ambazo zinataka kuhakikishwa kwamba wananchi wengi wanapata huduma kupitia sehemu zao za Manispaa.

Kwa maana hiyo, Manispaa zetu utakuta hazijiwezeshi kujihakikisha kwamba zinaweka mji safi ama katika hali ya uzuri, yaani kufanana na mji ya wenzetu hasa katika nchi za Afrika ambazo nyingi zao zinategemea Manispaa. Manispaa zetu kwa kweli, zinashindwa kujiwezesha hata usafi wa barabara zetu ama kuhakikisha barabara zetu zinakuwa nzuri zinafafana na mji wenyewe kama hivi sasa zinavyoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, uwezo wa Manispaa kuweza kuwa na madiwani wengi ni kuhakikisha kuweka uzuri, usafi pamoja na mapato ya mji wetu. Kwa mfano, hivi sasa katika Mji wetu wa Darajani sasa unangara sana kutokana na mataa ya kisasa, kwa sababu serikali imeanzisha Serikali za Mitaa kuzipa nguvu na Serikali za Mitaa ndizo ambazo zina uwezo wa kuhakikisha kutengeneza mji wake. Sasa kama Serikali za Mitaa hazitokuwa na madiwani wengi kama walivyopangwa ni kudhorotesha Mji pamoja na Manispaa zisiwe na uwezo wa kujitegemea.

Kwa kweli, Mhe. Mwenyekiti nahakikisha kwamba kama tutapata Manispaa ambazo zitakuwa na madiwani wasiopungua 10 na wale saba ambao watakuwa wa shehia, basi Manispaa zetu tutahakikisha kwamba tutakuwa na uwezo na kuipunguzia mzigo Serikali Kuu kuweza kufanya kila kitu. *(Makofi)*

Hivyo, nampongeza Mhe. Waziri kwa kuhakikisha suala hili alilolipanga ni zuri na linaweza kutekelezeka, ili Mji wetu ikawezekana kuweza kuhakikisha kwamba Mji wetu unaendelea tukafananisha na Miji mingine katika Afrika.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tusiwe wa mwisho kwamba Mji wetu hauna Madiwani wa kutosha.

Kwa mfano, nchi nyengine zilizoendelea kila Manispaa zinahakikisha zinakua na madiwani wa kuteuliwa si chini ya 20. Kwa kweli, nchi yetu haijafikia lengo hasa kwa madiwani kama hawa 10 tukasema ni wengi, yaani hawa madiwani kwa kweli hawajatosha kuchaguliwa na waziri. Hivyo, nadhani iko haja hasa ya waziri aongeze angalau watano, tukahakikisha kwamba madiwani 15 na wale saba ikawa 22, ili kuona kwamba shehia inafanya wajibu wake pamoja na Mji wetu kuona unajiwezesha bila ya kutegemea Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kila shehia iko haja ikajitegemea wenyewe bila ya kuingiliwa katika maendeleo yake ya ndani ya kijiji hasa kwa ajili ya kuleta maendeleo ambayo yanatakiwa na wananchi wake, pia wakahakikisha kwamba shehia yao ndio wanayoitegemea kwa hukumu zote na isiwe wanategemea Serikali Kuu kuweza kutoa sheria ndogo ndogo za maamuzi, isipokuwa ziwepe Shehia za Vijiji ziweze kujitegemea, kuhakikisha wananchi wake wanapata maendeleo kama yalivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa leo naomba nisiwe na mengi sana kwa ajili ya kumpa nafasi zaidi Mhe. Waziri na kumhakikishia kwamba wajibu alioutekeleza ndio wajibu ambao tuliokuwa tunauhitaji katika shehia zetu, ili shehia ziweze kujitegemea kwa lengo la kuleta maendeleo ambayo yanahitajika. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mussa Ali Hassan na sasa ni nafasi ya Mhe. Salmin Awadh Salmin.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kutoa mchango wangu katika mswada huu muhimu sana ambao unakusudia kuanzisha Serikali za Mitaa na kufuta zile sheria zilizokuwa zikitumika mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitumie fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa kuamua kuwasilisha mswada huu kwa Hati ya Dharura. *(Makofi)*

Nadhani kwamba Hati hii ya Dharura au mswada huu kuwasilishwa kwa Hati ya Dharura imetokana na umuhimu wa jambo hili, ambapo sote ni mashahidi kila wakati tumekuwa tukiulizia juu ya Sera za Serikali za Mitaa, ambazo hatimaye zimezalisha sheria hii ya kusimamia au kutekeleza sera zenyewe. Kwa kweli, ni zaidi ya miaka 20 sasa awamu kwa awamu zimepita tumekuwa

tukizungumzia juu  ya Sera za Serikali za Mitaa na kuona namna gani serikali inakwenda na mabadiliko yale ya kidunia.

Kwa hiyo, nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kuwasilisha mswada huu kwa Hati ya Dharura, ili jambo hili Waheshimiwa Wajumbe wako wakapata nafasi ya kulijadili na kuliamua.

Vile vile nataka niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe, kwamba dharura ni dharura, tunaposema kitu ni dharura maana yake ni dharura na wala haiwi jambo la kawaida. Hivyo, ndio maana tumeweka taratibu za kawaida, lakini tumeweka pia taratibu za kidharura, kwa hiyo dharura inayokuja kwa lugha ya leo *emergency* imekuja. Kwa hivyo, nadhani tuupukee huu mswada tuujadili, tutoe mawazo yetu, ili sasa mawazo yale ambayo tutayatoa au yale ambayo tutakosoa, basi Mhe. Waziri naamini atayazingatia, kwa ajili ya kuwekwa sawa mswada huu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka kuwakumbusha Waheshimiwa Wajumbe, kwamba kazi ya kuandika sheria ni kazi yetu sisi na wala sio ya Mhe. Waziri, kwa sababu waziri yeye anatuonesha mwelekeo analeta *draft*.

Sasa sisi jukumu letu kuona yale maeneo yenye mapungufu ambayo tunahitaji yafanyiwe marekebisho basi tuseme kama wengine waliotangulia wakasema na waziri ataangalia pamoja na kuzingatia, kwamba sera au muuongozo unasemaje, ili sasa tuandike sheria iliyokuwa bora, ambayo inakudusiwa na hilo ndio lengo. Lakini tusiukatae moja kwa moja, isipokuwa tuseme yale mapungufu ambayo tunayaona yamo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naamini kwa kuwa Mhe. Rais ameweza kuwasilisha mswada huu kwa Hati ya Dharura, lakini pia ataweza kuwasilisha mswada ule wa Utawala wa Baraza kwa Hati ya Dharura katika kikao kijacho, kwa sababu jambo hili nalo tumekuwa tukilisema sana tunalihitaji.

Kwa hivyo, nalo linahitaji Hati ya Dharura, kuona kwamba kabla ya kumaliza Baraza hili basi tunakuwa na mswada ule wa sheria unaohusu masuala ya utawala wa chombo hiki, ili chombo hiki nacho kiweze kwenda kwa mujibu wa taratibu zile za kidunia, yaani taratibu za Mabunge ya *Commonwealth* kuliko ilivyo sasa. *(Makofi)*

Namuomba sana Mhe. Rais kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba kikao kijacho cha mwezi wa Januari atuletee ule mswada unaohusiana na masuala ya Baraza kwa Hati ya Dharura, ili tuujadili nao uweze kufanya kazi zake. *(Makofi)*

Baada ya kumshukuru Mhe. Rais, pia nitumie nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri. Kwa kweli, Mhe. Waziri amefanya kazi kubwa ni muda mfupi ambao amekuwepo katika wizara hii lakini ameweza kumudu kutuletea kitu hiki, kwa kweli hatuwezi kusema kwamba kimetimia asilimia mia juu ya mia hapana, inaweza kuwa kina mapungufu, lakini mawazo yao wenzetu ni hayo, kwa hivyo na sisi tuchanganye mawazo yetu, ili tupate kitu kilichobora. Hivyo, Mhe. Waziri tunakupongeza sana kwa kuwasilisha jambo hili. *(Makofi)*

Kimsingi naukubali mswada huu na yale mambo ambayo yamekusudiwa. Lakini ninalotaka kusema ni kwamba lengo na madhumuni ya kuanzisha Serikali hizi za Mitaa kwa hao wenzetu ambao wametangulia na sisi tukafuata tukaiga ni kugatua yale mamlaka ya Serikali Kuu na kuyaleta chini kwenye Serikali za Mitaa na hayo ndio madhumuni makubwa. Kwa maana hiyo, Serikali Kuu kukasimu nafasi ya mamlaka yake kwa Serikali za Mitaa, yaani kupeleka chini. Sasa Mhe. Waziri kama sheria yako imeelekeza huko mbona sisi hatuna matatizo. *(Makofi)*

Lakini naona bado kuna baadhi ya maeneo yana mapungufu katika jambo hili na mapungufu haya nadhani bado serikali inahitaji kuyaona kwa ujumla na wala sio katika eneo hili tu la Serikali za Mitaa, isipokuwa ni katika maeneo yote yale ambayo bado serikali inayasimamia kuona yanatoa nafasi kwa vyombo vile kufanya shughuli zake.

Mhe. Mwenyekiti, narudia kule nyuma ambako tulikotoka kunakohitaji kuwa na sheria, ambayo hata *separation of power*, mihimili hii bado serikali au dola ising'ang'anie kuchukua madaraka yote kwa pamoja. Kwa kweli, bado kuna nafasi serikali kutoa nafasi kwa chombo kama baraza la Wawakilishi kama ni muhimili pamoja na Mahakama pia, yaani kutoa ile *separation of power*, ili kila mmoja aweze kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, si vyema kuendelea kung'ang'ana na kushikilia, nadhani huo utakuwa sio mfumo mzuri ambao unaendana na wakati. Kwa hivyo, na hili naamini kwamba sheria hii itakuwa inatoa fursa zaidi kwa Serikali au Mamlaka za Mitaa kuweza kufanya shughuli zake.

Vyombo hivi ambavyo vimeanzishwa ambapo wakati ule vilikuwa kila kimoja kina sheria yake sasa hivi tumeweka sheria moja, tumeweka sheria moja ambayo itaongoza masuala yanayohusu jiji, manispaa na halmashauri zile pamoja na taratibu zitakapokuwa. Lakini inavyoonekana kwa mujibu wa sheria hii mambo mengi yatatungiwa kanuni lakini yapo masuala hasa ya msingi yalikuwa bado yanahitaji kuwemo kwenye sheria kuliko ilivyo sasa, bado yalikuwa yanahitaji maamuzi ya chombo hiki, lakini inaonekana mambo

mengi yamewekwa kwenye kanuni ambayo kanuni inatungwa peke yake na Mheshimiwa Waziri. Kwa hivyo naona kuna haja ya kuliangalia jambo hili kwamba yapo maeneo ambayo yanahitaji kuwemo hasa kwenye sheria hii badala ya kuwemo kwenye kanuni na zile *by laws* kuna haja hiyo ili kutoa fursa zaidi.

Lakini jengine Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalotaka kusema katika mfumo huu wa uanzishaji wa Serikali za Mitaa lazima Serikali ifahamu Mhe. Waziri kwamba unapozungumza Serikali ya Mtaa maana yake ni serikali kamili, ni serikali kamili yenye maamuzi kamili. Si vyema vyombo hivi vikawa sasa havina mamlaka juu ya shughuli ile nadhani tutakuwa tunarudi nyuma, kwa hivyo tuvipe mamlaka kamili ya kufanya maamuzi kamili ili yanapotokea matatizo basi tuweze kujua nani wa kumlaumu.

Mwenzangu hapa Mheshimiwa Mshimba alisema mwanzo kwamba kuna mambo mengi ambayo yangetaka yatekelezwe na Serikali za Mitaa lakini unakuta Serikali kuu inaingiza mkono wake, na hatimaye mambo yale unayakuta hayana ufanisi. Mimi nitazungumzia suala moja, kuna mradi huu wa *ZUSK* ambao unasimamiwa na Baraza la Manispaa la Zanzibar lakini taratibu zilizopo mradi ule wa *ZUSK*, hatukuwaachia wenyewe watu wa Tawala za Mikoa unakuta mradi ule una mikono mingi, Wizara ya Fedha haiachii na kila mtu, na matokeo yake mradi ule unakuta hakuna ufanisi. Mimi nataka kusema kwamba mradi ule hauna ufanisi, na hauoneshi mwelekeo kwa sababu yale mambo ya msingi ambayo yapo kwenye mradi ule yameshindwa kutekelezwa.

Mimi naamini kama mradi ule tungewaachia wenyewe wenye *local government* zile wakasimamia wakatekeleza naamini mradi ule sasa hivi tungakuwa tunazungumzia lugha nyengine, na tungepata nafasi ya kujua nani wa kumlaumu katika lile, mimi kwa kweli Mheshimiwa Mwenyekiti katika bajeti ijayo patakuwa na kazi si ndogo juu ya mradi ule. Kwa sababu mradi ule sasa tunamaliza miaka mitano bajeti ijayo itakuwa ndio bajeti ya mwisho mradi ule tumeanza kuuzungumza tokea bajeti ya kwanza, mradi ule umezungumzwa tokea awamu ya tano, mradi ule Dokta Ali Mohammed Shein amekuwa akiuzungumza kwenye kampeni zake za uchaguzi tokea kipindi kile, inasikitisha kuona mradi ule mpaka hivi leo ninavyozungumza hatujaona chochote kinachoendelea. Wananchi hawajaona chochote tumetumia mradi ule hasa kwa utengenezaji hasa wa michirizi katika kampeni ile kwa wananchi wetu nilikuwepo mimi kwa sababu mradi ule umegusa sana katika maeneo yangu ya jimbo langu juu ya kuondosha maji machafu katika maeneo ya Sebleni, Sogea pamoja na maeneo mengine lakini mpaka leo huoni dalili yoyote, huoni chochote kwa kweli inasikitisha na bajeti ijayo itabidi tupate maelezo ya kutosha juu ya jambo hili.

Haya yote yanatokana na kwamba hatujazipa Serikali za Mitaa mamlaka yake na maamuzi yake juu ya kusimamia mambo haya, kwa hivyo ni matumaini yetu kwamba sheria hii badala ya kututoa hapa tulipo na kutupeleka mbele, kama haikuwekwa vizuri inaweza ikaturudisha nyuma, kuna kitu humu kimeandikwa sana Sekretarieti ya Mkoa, kuna maeneo yameandikwa Sekretarieti ya Mkoa, Halmashauri zinapeleka maelezo yao kwenye Sekretarieti ya Mkoa *why Mkoa? why secretariat* ya Mkoa wakati vyombo hivi ni vyombo vyenye maamuzi. Kwa hivyo hili nadhani tuliangalie sana kwa makini tutakuwa hatwendi kule mbele tunakokwenda matokeo yake tutakuwa tunarudi nyuma, kwa kweli hili nimesema nilizungumze sana juu ya dhana hii.

Lakini jengine hili ambalo Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wamekuwa wakilizungumzia suala la Mheshimiwa Waziri kuchagua wajumbe kumi, kwa kweli nadhani hili Mheshimiwa Waziri anahitaji kuliangalia sana lina mantiki, linazungumzika kwa sababu sheria ile iliyopita ya Baraza la Manispaa si kwamba mambo yake yote yaliyokuwemo yalikuwa mabaya la hasha, mengine yalikuwa ni mazuri lakini tumekwenda katika kuboresha. Sheria ile ilimpa Mheshimiwa Waziri mamlaka ya kuteua wajumbe watatu lakini haikusema kama mwanamke mmoja zilikuwa ni hekima za Mheshimiwa Waziri mwenyewe wajumbe watatu, lakini hii inatoa nafasi kwa wajumbe kumi Mhe. Waziri hebu liangalie kwa makini jambo hili nadhani linahitaji marekebisho na linazungumzika.

Kwa kweli kiwango hicho ni kikubwa mno linaweza kuzungumzika kuona nafasi hizi tunaziangalia vizuri na ndio wajibu wetu chombo hiki, wajibu wetu ni kutengeneza kama nilivyosema si kulaumu na kusema hiki kitu kibaya hapana, pale ambapo tunahisi hapakukaa sawa tuseme ili paweze kuwekwa sawa kwa sababu sote ni binaadamu tuna akili na tunavyoambizana basi tuna haki ya kuangalia uzito wa jambo hili. Kwa hivyo Mheshimiwa Waziri utakapofanya majumuisho hebu angalia uzito wa jambo hili, hili jambo linazungumzika.

Jengine Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utendaji katika taasisi zetu hizi, kwa kweli taasisi hizi zimekuwa na matatizo katika utendaji, hata wakati mwengine Baraza lako hili la Wawakilishi liliwahi kuunda kamati teule nadhani mnakumbuka, tuliunda kamati teule kuchunguza Baraza la Manispaa juu ya utendaji wa Mkurugenzi na mambo mengine baada ya kuona shughuli kule haziendi vizuri. Na Baraza hili likatoa ripoti mimi bahati nzuri kwenye kamati ile nilikuwa ndio Mwenyekiti wa kamati, kuna mambo ambayo tumeyaeleza pale ambayo matatizo tuliyoyaona na chombo hiki Baraza lako likatoa *terms of reference* juu ya yale mambo, kwa mfano kuangalia Mkurugenzi namna anavyoendesha na anavyofuata sheria, kwa hivyo

nilidhani wakati wa uandishi wa sheria hii ungeelekeza kuona matatizo yale yaliyojitokeza katika utendaji na katika utekelezaji basi yanatatuliwa, lakini nilipopitia haraka haraka basi nimeona yameongeza matatizo zaidi badala ya kupunguzwa matatizo zaidi.

Kwa mfano Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sheria ile namba tatu ya mwaka 1995 ilikuwa inamtaja Mkurugenzi wa Manispaa kwamba atakuwa ndio mtendaji mkuu lakini atawajibika kwa Baraza, lakini pamoja na statement iliyokuwemo kwenye sheria alikuwa anashindwa kuwajibika kwa Baraza, akawa anafanya mambo yake mwenyewe anavyoona yanafaa kama vile ni kampuni yake, hayo Kamati teule iliyaona. Alikuwa anaitisha tenda, anapitisha miradi, anafanya mambo chungu nzima hata dira ya kupitishiwa kwenye *council* yale na ilihali sheria ile ilikuwa inataja moja kwa moja.

Lakini ukiangalia sheria hii wala haizungumzii hivyo imemtoa kabisa Mkurugenzi, sasa haya ni hatari, kwa sababu ukiangalia hapa katika sheria hii eneo hili la uteuzi wa Mkurugenzi imesema tu kwamba atakuwa mtendaji mkuu, lakini ibara ya pili inataja kwamba atawajibika kwa majukumu yake mwenyewe na shughuli zake mwenyewe, hii siyo sahihi. Kama wakati ule Sheria ilikuwa inamtaja awajibike kwa Baraza na akawa anashindwa kuwajibika kwa Baraza, leo unaondosha kifungu kile unaandika vyengine, ukumbuke ile ni *council* sio serikali kile ni chombo cha kisiasa kilichotolewa na wananchi na ndicho chenye maamuzi juu ya kusimamia sera na mambo mengine. Kwa hivyo haiwezekani kabisa kuondosha mambo kama yale ya msingi, mimi nilidhani itatoa *statement* kabisa itakayomuonesha moja kwa moja Mkurugenzi kwamba yeye anawajibika kutekeleza majukumu yake katika vyombo vile, hawezi sasa kufanya vyenginevyo vyovyote pamoja na kwamba kuna ibara moja ndogo inayosema atekeleze juu ya maamuzi, ile ni *statement* ndogo na anaweza kutekeleza maamuzi ya *council* lakini anaweza kufanya na yake mengine aliyokuwa nayo sasa utamfanyaje.

Lakini Mkurugenzi wa Manispaa au Mkurugenzi wa Halmashauri yeye anatakiwa afanye na utekelezaji wake kwa mujibu wa yale ambayo yamepitishwa pale, ananionyesha kifungu hiki ibara ya 39 (2) inasema, Mkurugenzi atakuwa mtendaji mkuu na afisa basi, uhuru wa mamlaka za Mitaa na hatakuwa na majukumu ya kazi za kila siku za mtaa. Lakini mtu aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi atalamzimika kuwajibika katika kazi na majukumu yake basi!

Lakini ibara ya 41(1)(a) inasema atawajibika na kutekeleza maamuzi yote yaliyofanywa na Baraza, haya ni mambo mawili tofauti kuwajibika katika chombo kile, lakini kuhakikisha kwa yale yale yaliyopitishwa pale, huyu Mkurugenzi lazima tukumbuke anateuliwa na Mheshimiwa Rais kwa mujibu

wa sheria hii. Kwa maana hiyo atawajibika kwa Rais aliyemteua, kwa maana hiyo kwa mujibu wa sheria hii atakuwa sasa yeye pale hana uwajibikaji isipokuwa juu ya yale maamuzi yaliyotolewa na *council* tu atayafuata, lakini mwenyewe atakuwa anawajibika kwa majukumu yake mwenyewe jambo ambalo litaleta migogoro mikubwa, na tutakuja kuunda tume hapa na tume nyengine na tume nyengine matatizo haya hayaondoki, mimi nina *experience* juu ya masuala haya, juu ya masuala mbali mbali. Kwa hivyo Sheria hii ingeliweka wazi Mkurugenzi ajue kwamba mimi nawajibika hapa juu ya wanasiasa, sio ilivyo hivi sasa imewekwa kwenye lugha nyepesi.

Kwa hivyo Mheshimiwa Waziri nadhani kuna haja ya kuiangalia sheria ile iliyopita ile kwa sababu sio kama yote ilikuwa na matatizo, kuna vifungu vingine vilikuwa vizuri na vinakwenda kwa mujibu wa zile taratibu ziliopo, kwa hivyo eneo hili nalo Mheshimiwa Waziri nadhani uliangalie kwa sababu ni eneo ambalo linatuletea matatizo sana. Kuna kuwa na mivutano mkubwa sana kati ya wakurugenzi ambao watendaji lakini pamoja na zile Halmashauri wanafika pahala Wakurugenzi wale wanawadharau kabisa wale Madiwani ambao wameteuliwa ambao wao ndio *council* ile ndio *Council* yenye bila ya kuwa na Madiwani huna *council* pale wale wengine wote ni watendaji. Kwa hivyo wao ndio wenye maamuzi juu ya chombo chao.

Eneo jengine Mheshimiwa Mwenyekiti, ambalo nishukuru kwamba sheria hii inakusudia kuanzisha kamati za maendeleo katika mamlaka ya mitaa, ambapo Serikali inakusudia kutenga fedha kwa ajili ya kuzipeleka kwa ajili ya masuala ya maendeleo katika mitaa, mimi Mheshimiwa Mwenyekiti nadhani hii ni hatua kubwa ambako huko nyuma kwenye taratibu zetu zile za kizamani hapakuwepo na jambo hilo. Zamani ilikuwa fedha zile wenyewe Manispaa wanazikusanya basi kama zinakuwa zinakidhi mahitaji yao basi sehemu tu ya fedha zile wanajaribu kuzipitishaia kwa Waheshimiwa Madiwani kwa ajili ya maendeleo, na wakati mwengine pesa zile zinakuwa hazitoshi kwa sababu kama tunvyojua Halmsahauri hizi au Manispaa wana majukumu makubwa ya huduma nyengine sio masuala ya maendeleo tu, tumewapa majukumu ya usafi katika mji na kuangalia mambo mbali mbali ya bustani na mambo mengine, kwa hivyo wanakuwa na majukumu makubwa kutoa *service* ile kutokana na kile kipato kidogo wanachokisanya. Wakati mwengine wanatenga fedha kidogo kwa ajili ya maendeleo katika sehemu lakini sasa hivi sheria hii inakusudia Serikali kuu basi kutenga fedha kwa ajili ya maendeleo, wameanzisha kamati ya maendeleo ambayo itakuwa inaratibu maendeleo mimi nadhani hilo jambo zuri nafasi hii tuitumie vizuri na hata zile kamati za wodi ambazo zimetajwa humu na wajumbe wake ambazo zitakuwa zinaangalia ni maeneo gani katika wadi ambayo yanahitaji kupata msukumo.

Kwa bahati nzuri fedha zile zitakuwepo na yule Mwenyekiti wa wadi ambaye atakuwa ndio mjumbe katika kamati ile ya maendeleo ya serikali ya Mtaa basi atapata fursa ya kuchukua yale maeneo ambayo wananchi katika wadi ile wanahitaji , ikiwa masuala ya maji, barabara, afya na miundo mbinu na hata katika muundo pale wamewekwa wajumbe watano katika wodi ambao watachukuliwa katika miongoni mwa wale wataalam waliopo katika eneo lile katika fani ile katika kusaidia kuleta maendeleo. Nadhani hii ni hatua kubwa ni fursa kubwa ambayo itawezesha sasa fedha zile za Serikali kwenda kwa wananchi moja kwa moja kwa ajili ya kutatua matatizo yao katika miradi midogo midogo, hizi zitakuwa ni mbali ya fedha zile ambazo zinapitishiwa kwenye Kamati za maendeleo za waheshimiwa hizi nadhani ziko mbali.

Kwa hivyo maendeleo katika maeneo yetu yatakuwa yanapatikana kwa fedha kutoka katika Serikali kuu kwa kupitia kamati zile za maendeleo ambazo wenyeviti wao ni Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, lakini hata kupitia kamati hizi za wadi ambazo zitakuwa fedha zake zinapelekwa kwenye Serikali ya Mtaa katika kila Halmashauri na Manispaa, nadhani eneo hili ni zuri.

Kubwa zaidi Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nasisitiza juu ya umuhimu huu wa vyombo hivi kuwa na maamuzi ndio sera ya kidunia, si vyema tukawa sisi Serikali kuu tunaingiza mikono yetu tunaandaa sheria ambazo bado zinawarejesha nyuma, hili Mheshimiwa Waziri hata utakapokuja kuandika kanuni zako juzi tulipokuwa kwenye kamati nilizungumzia sana juu ya uandishi wa barua zile ambazo zinasema barua hizi lazima zipite Sekretarieti ya Mkoa, jambo ambalo mimi sikuafiki na tukakubaliana kwamba utaandaa kanuni ambazo utaelekeza ni maeneo gani. Mimi kwa masuala yale ya fedha za maendeleo sina tatizo, kwa sababu sasa hivi Manispaa zinashughulikia masuala ya maendeleo. Lakini tukumbuke pia wana mashughuli yao na wao yale ya kila siku ya kushughulikia masuala yao ya kimanispaa ambayo nayo wanahitaji kuwasiliana katika vyombo mbali mbali, katika taasisi mbali mbali.

Mhe. Waziri kwa mujibu wa taratibu hizi hivi vyombo viko chini yako, taasisi hizi haziko chini kwa sababu hizi taasisi ni za kisiasa zaidi watu hawa wanachaguliwa na wananchi, hawa wako chini ya mwanasiasa mwenzao hawako chini ya utendaji kwa nini tuwe tunawasukuma kwenye utendaji, tunawatumia kwenye utendaji hawa maamuzi yao mengi yanategemea na maamuzi yako na Waziri anakuwa yeye ni mtu wa karibu sana katika vyombo hivi, kwa sababu ni vyombo vya kisiasa zaidi si vyombo vya utendaji.

Kwa hivyo Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa muda huu nimetoa mchango wangu naukubali mswada huu upite kwa asilimia mia juu

ya mia, uende ili uwe sheria kwa sababu itakuwa sio vyema tukiendelea kuukwamisha sisi wenyewe, tumeutaka na tumeuomba siku zote tunapiga kelele halafu leo wametuletea wenzetu tena kwa hati ya dharura, halafu leo tuwaambie warudi nao. Tunajua itakuwa kasoro zipo tuzisawazishe kasoro zilizopo ili mswada huu wa sheria uanze kutumika kwa manufaa ya watu wetu. Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana (*Makofi*).

**Mhe. Mwenyekiti:** Huku nimebakiwa na mchangiaji mmoja ambaye ni Mheshimiwa Hijja Hassan Hija kwa hivyo atakuja kumalizia jioni baadae tutamkaribisha Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu achangie na baadae atamalizia Mheshimiwa Waziri.

Lakini kabla ya kufunga kuna tangazo hapa, WaheshimiwaWajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwamba mazoezi ya Timu ya Baraza la Wawakilishi yanaendelea katika uwanja wa Mao Tse Tung kila siku kuanzia saa 12.00 asubuhi, kwa ajili ya maandalizi ya mchezo kati ya timu ya Baraza la Wawakilishi na Benki ya NMB kutoka Dar es Salaam, mchezo huo unatarajiwa kufanyika siku Jumamosi tarehe 8/11/2014 katika uwanja wa Amani saa moja usiku. Hivyo basi Waheshimiwa wote mnaombwa mushiriki kwenye mazoezi na hatimae mufike katika mechi pamoja na washangiriaji wote. Naomba kuwasilisha.

Baada ya maelekezo hayo sasa nasitisha kikao hichi hadi Saa 11.00 za jioni ya leo, ahsante.

*(Saa 12.58 Mchana Baraza liliahirishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, napenda nikushukuru kunipa nafasi jioni hii na naomba nitoe mchango wangu kwa ufupi kwa kile ambacho nimekiona, ingawa mswada huo nimechelewa kuupata kama kawaida yetu, lakini napenda niseme kwamba, mswada huu unajibu matakwa ya wananchi wa Zanzibar, ikiwa ni matakwa pia ya sehemu ya wawakilishi ambayo mara kadhaa tumekuwa tukiomba Serikali kuleta mswada wa marekebisho ya Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, duniani kote nguvu ya utendaji wa maslahi ya umma uzalishaji na usimamizi wa maendeleo basi umeletwa kwenye Serikali za Mitaa. Kwa hivyo sio rahisi kupinga nadharia hii iwapo na dhana hii

imekwenda sambamba na vigezo vya kimataifa na vigezo vya nchi nyengine ambazo wamefanikisha ufanisi mzuri wa mfumo huu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano wa karibu wenzetu Tanzania Bara wamewezesha Serikali za Mitaa kuleta maendeleo ya wananchi tofauti na Zanzibar. Zanzibar Serikali za Mitaa zimekuwa ni kero. Kwa wenzetu ni kimbilio la nchi kimaendeleo kiasi ya elimu, miundombinu maji na kadhalika.

Wananchi wa nchi za wenzetu wamekuwa na manufaa makubwa kwenye Serikali za Mitaa. Kwa hivyo mswada huu kama umetungwa kwa ajili ya kujibu masuala hayo ni lazima wawakilishi waunge mkono. Lakini kama una dosari hakijafikia kiwango hicho, basi ni lazima tuoneshe zile dosari, ili Waziri atukubalie na hatimaye twende sambamba kwa vigezo vya kimataifa. Tuangalie majirani zetu wanafanyaje, ili lengo la kuleta ufanisi kwa wananchi liweze kufikiawa.

Mhe. Mwenyekiti, ni tegemeo letu kwamba Waziri kwa sababu yeye amekuwa ni shahidi mara zote wawakilishi wake wakidai marekebisho ya Serikali za Mitaa nadhani hatakuwa mbishi, hatukubali pale ambapo wawakilishi wake watamshauri ili kuleta ufanisi wa sheria hii kwa lengo la kuleta maendeleo ya wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo sasa nianze kwenye ukurasa wa 225 kifungu cha 11 naomba ninukuu aina ya mabaraza ya Serikali za Mitaa yanaweza kuwea kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nashauri neno yanaweza lifutwe na badala yake liandikwe yatakuwa, maana yake yanaweza ni hiari ya mtu akitaka lakini tuweke yatakuwa, ili kama ni wajibu wa kufanya. Ukisema yanaweza maana yake unamfanya mtu akipenda afanye na asipopenda aliwache, kwa hivyo madam ni wajibu wa mabaraza haya Mhe. Mwenyekiti, ni muundo mpya kwa hivyo neno yanaweza liondoke na badala yake liwe yatakuwa.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu nyengine ambayo nataka nizungumze kwa ujumla wake kwenye muundo wa mabaraza yenyewe, kifungu cha 18, 21, 22 na 24 vyote kwa pamoja mswada huu vinaeleza kwamba Waziri atateua wajumbe kwa maana ya Madiwani, ziko sehemu madiwani 10 na Waziri atateua ziko sehemu atateua madiwani watano. Hoja yangu kwa ujumla Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba hawa ni wanasiasa waliochaguliwa, hapa Zanzibar sisi kama Wazanzibari Katiba yetu iko wazi kwamba mfano wawakilishi wanapochaguliwa na wananchi asilimia 30 kwa sasa ndio wawakilishi wanaopata nafasi za kuteuliwa.

Kwa hivyo uteuzi huu wa Madiwani Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri si busara kutuwekea nambari kwamba ateue madiwani 10 kwa mfano. Halmashauri ya Wilaya Mkoani ina madiwani 11akiteua kwa kiwango kile cha madiwani 10 maana yake itakuwa na madiwani 21. Wale 10 ambao wameteuliwa na kwa sisi Wazanzibari wengi wa nidhamu ya woga unapomteua anakutii hata kama sio matakwa ya sheria. Kwa hivyo ukiteua 10 maana yake unawafanya watu 10 watii matakwa ya Waziri hata kama ni kinyume na sheria.

Kwa hivyo ninashauri kwamba tusikiuke Katiba, tuweke asilimia maalum kama ilivyo kwenye Katiba kwa upande wa wawakilishi na madiwani kuchaguliwa. Na kwa sasa kabla ya Katiba mpya ambayo kwangu mimi sijaamini kama itakuwa na ufanisi ni asilimia 30 nafasi za uteuzi kwa mabaraza ya kuchaguliwa. Kwa hivyo Mhe. Waziri hili nikuombe sana kwa heshima zote usijiamulie tu kwamba utateua madiwani 10 kwa Halmashauri, madiwani 10 kwa Baraza la Mji, madiwani 10 kwa jiji lazima tuweke asilimia. Asilimia ngapi kwa kila Baraza ya Madiwani waliochaguliwa ndio itakuwa asilimia ya uteuzi wa Waziri.

Hii Mhe. Mwenyekiti itawapa fursa wale madiwani waliochaguliwa kutambua wajibu wao na kwamba watakuwa hawana hofu juu ya wale watu walioteuliwa, ambao tukiacha sheria kama ilivyo Mhe. Waziri atakuwa na nguvu kubwa ya kuteua watu, na kwa uzoefu wa Zanzibar ninasisitiza Wazanzibari wengi wanakuwa na nidhamu ya wote, atafuata matakwa ya aliyemteua.

Kwa hivyo hii si busara sheria na nadhani Mhe. Waziri naomba uwe msikivu kwa hili kwakifungu cha 18 (1)(e), 21(1)(d), 22(1)(d), 24(1)(d) zote Mhe. Waziri usiteue kwa idadi ya namba badala yake uteue kwa asilimia ya wajumbe waliochaguliwa.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye kifungu cha 21(i) naomba ninukuu:

“Kusimamia uchimbaji wa mawe, mchanga na uvunaji wa mbao au rasilimali nyengine za asili kama zitakavyodhibitiwa na Waziri mwenye dhamana ya raslimali za asili”.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni kazi ya Manispaa, ninapata tabu kuona kwamba manispaa zetu kweli zina masuala ya mawe maana Halmashauri mjini huko *coastal area* kote huku kuna machimbo ya mawe. Ninapata mashaka kwamba pale Mkoani pengine au Wete, Chake au Zanzibar mjini kwamba hii kazi ya usimamizi wa machimbo ya mawe itakuwa ni kazi yao. Kwa hivyo nadhani kwa ushauri wangu Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki Waziri angenikubalia kikasomeka kama ifuatavyo kwamba ni uvunaji wa raslimali mbali mbali. Ili

kama itabahatika kuna mawe, ikibahatika kuna mafuta, gesi iwe ni *general* zaidi kuliko kuwaambia mpaka kazi ya mawe. Ukiwapa kazi watu wa mjini waje wadhibiti raslimali mawe wakati hata hawajawahi kuyaona wengine.

Kaka yangu Mhe. Gavu anayekaa mjini sidhani kama jiwe analijua, lakini mimi ninayeka Muambe na mwenzangu wa Micheweni na Matemwe ndio hasa wenye mali ya jiwe. Kwa hivyo nadhani Manispaa hii si kazi yao na badala yake iandikwe kwamba ni uvunaji wa raslimali mbali mbali pale ambapo zitajitokeza, ikiwemo mawe pengine mafuta, gesi na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 32 Meya atakuwa na uwezo wa kazi zifuatazo:

(a) Kiongozi wa Baraza la Mji au Manispaa.

Naomba isiwe kiongozi iwe kuongoza Baraza la Mji au Manispaa, maana yeye Meya ni kiongozi kwa hivyo tuseme kuongoza na hivyo hivyo 33(1)(a) neno kiongozi liondoke liwe kuongoza ili ile sifa ya Meya basi iwe kazi yake ni kuongoza sio yeye ni kiongozi halafu kiongozi tena basi tuweke sifa ya kuongoza.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 237 kifungu cha 39(1) Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna uteuzi wa wakurugenzi, wakurugenzi wa manispaa jiji hawa watateuliwa na Rais lakini wakurugenzi wa Mabaraza ya Mji na Halmashauri watateuliwa na Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, sipingani na mfumo huu lakini ninachotaka kusema wazi kwamba Zanzibar imekuwepo tabia sifa za kiwango cha elimu ni zile zile, *degree* ya kwanza au *masters* au *diploma*. Lakini madam mimi nimeteuliwa na Rais ninakuwa na mshahara mkubwa kwa sababu mimi nimeteuliwa na Rais, mwenzangu Mhe. Haji ambaye na yeye ana *degree* ile ile ameteuliwa na Waziri anakuwa na mshahara laki nne, sifa zile zile, majukumu yale yale uzoeefu ule ule.

Kwa hivyo mimi tumekubaliana kifungu hicho Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu wakurugenzi hawa wote watakuwa na sifa moja; *degree* ya kwanza naomba Mhe. Waziri atwambie maslahi yao yatakuwa vipi. Kwa uzoefu hapa Zanzibar kwamba kila ambaye Rais amemteua yeye ndio VIP anakuwa na mshahara mkubwa. Huyu wa chini ambaye hana uteuzi wa Rais yeye anapewa laki tatu na nusu, laki nne na hatimaye unatayarisha mazingira ya wizi.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki lazima Mhe. Waziri tukubaliane kwamba maslahi ya wakurugenzi hawa wale ambao Rais atawateua wakiwa wana *degree* ya kwanza na wale Mhe. Wziri ambao atawateua wana sifa ile ile ya *degree* ya kwanza basi maslahi yao yaende sambamba, isionekane kwamba

uteuzi wa Rais kwa elimu ile ile yeye ni bora zaidi na mteuzi wa Waziri kwa elimu ile ile awe ni mtu wa chini.

Mhe. Mwenyekiti, hili na Mhe. Waziri tukubaliane na ajue kwamba wakurugenzi hawa ndio watakaokuwa na majukumu ya kuendesha taasisi hizi wakiwa na elimu sawa na uzoefu sawa, kwa hivyo maslahi yao lazima yawe sawa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme jengine kwamba uwajibikaji wa wakurugenzi kaka yangu Mhe. Salmini amezungumza asubuhi hapa kwamba mabaraza duniani kote, mabaraza husika ndio yenye kuchukua dhima ya kuwajibisha Wakurugenzi. Kwa hivyo huyu ambaye Rais amemteua ni wazi kwamba atakuwa na kibri kwamba hatakuwa na uwezo wa kuajibishwa na Baraza husika. Na huyu ambaye Waziri amemteua kwa tabia yetu ya Zanzibar itakuwa hakuna uwezo wa kuaibishwa na Baraza.

Kwa hivyo kifungu cha uajibikaji wa wakurugenzi hawa naomba tuwe wazi kwamba mabaraza husika yana uwezo wa kutoa mapendekezo ya uajibikaji na kuwaajibisha Wakurugenzi wao na kwa hawa wawili ambao Rais anawateua baada ya mashauriano ya Baraza husika Rais azingatie busara zake na aweze kuchukua hatua. Lakini tukiacha hivi hivi tu kwamba wao kwa sababu wameteuliwa na hakuna nguvu ya Baraza husika Mhe. Mwenyekiti, Mabaraza yetu yatakuwa hayana nguvu yoyote na yatadharauliwa na itakuwa hakuna maana yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka niseme kwamba maslahi ya madiwani wetu. Mhe. Mwenyekiti, kwa miaka kumi mfululizo nimekuwa nikisikia kwamba wawakilishi wengi wanatetea maslahi ya madiwani wetu. Hoja ya Serikali madiwani hawa ni wengi uwezo hawana, Mhe. Mwenyekiti, nachukua Baraza la Madiwani ambalo liko Wilaya ya Kaskazini “B”. Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wanakusanya zaidi ya milioni mia tatu lakini Serikali inashindwa kuweka mshahara mdogo angalau laki moja kwa mwezi, jambo ambalo kwa mwaka lisingezidi milioni hamsini. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mantiki ya Serikali iko wapi, kwamba watu wanazalisha fedha nyingi lakini posho wanaopewa madiwani wetu hawa ni posho ndogo.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali inaandaa mazingira ya wizi, ni nani ambaye anakusanya milioni mia tatu, mshahara wa Katibu wa Halmashauri ni shilingi laki mbili, posho ya diwani shilingi elfu thalathini, halafu umwambie nani asiibe. Kwa hivyo kama lengo ni kudhibiti wizi na kudhibiti utendaji wa Halmashauri zetu maslahi ya watendaji na maslahi ya madiwani wetu yaongezwe. Haitowezekana Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya

Magharibi sasa hivi inakusanya karibu bilioni moja, lakini maslahi ya madiwani na watendaji wetu ni mshahara mdogo sana.

Sasa nadhani Mhe. Mwenyekiti, kila ambaye anakusanya basi afaidike na utaratibu uangaliwe kwa maslahi ya madiwani, lugha ya mshahara pengine haipendezi lakini hilo posho Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri lazima kuwe na kanuni madhubuti ambalo posho lao litaongezeka, ili kulinda maslahi madiwani wetu wachape kazi vizuri kwa ajili ya kuleta ufanisi kwenye Halmashauri na Mabaraza ya Mji mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 47(d) kifungu hiki kina muundo wa Kamati ya Ushauri ya Shehia, kifungu (b) Wajumbe wasiozidi watano kutoka katika kijiji au mtaa ndani ya shehia hiyo. Mhe. Mwenyekiti, nashauri kwamba kazi ya Kamati ya Ushauri wa Shehia ni kazi kubwa ni kazi nyengine za kitaalamu nashauri kwamba badala ya kuwateua wajumbe hawa watano Mhe. Mwenyekiti, lazima wajumbe hawa watano wachaguliwe kwa ridhaa ya wananchi husika. Tusiwaachie masheha na watu fulani kuteua watu hawa, wako watu katika mitaa yetu Mhe. Mwenyekiti, wana sifa kubwa za uchumi, za elimu na mambo mengine. Kwa hivyo tukiwaachia wananchi wachague watu wao wanaowataka Mhe. Mwenyekiti, watu watano hawa watachagua watu wenye sifa nzuri ili watasaidia Kamati ya Ushauri ya Kijiji au Shehia.

Mhe. Mwenyekiti, nashauri kwamba kamati hii ichaguliwe na ukiangalia kazi ya kifungu cha 48 Mhe. Mwenyekiti, kifungu (b) moja kati ya kazi yao ni kusimamia mipango ya ajira ndani ya shehia. Sasa kama kusimamia mipango ya ajira unachagua watu ambao hawana uelewa Mhe. Mwenyekiti, wimbi la migogoro katika shehia zetu litakuwa kubwa.

Kwa hivyo wachaguliwe watu wenye uwezo wa kielimu, ili wanapoamua kuajiri mtu waajiri kwa kiwango na vigezo vya kielimu ili kuondosha upendeleo. Kwa mfumo wa sasa tukiwaachia watu hivi hivi kuchaguana tu maendeleo yanayohitajika ya Serikali ya kupatikana ufanisi hayatopatikana. Watateuliwa watu ambao hawana uwezo wa taaluma na hatimaye matatizo ya shehia zetu yatakuwa makubwa. Nashauri kwamba watu hawa wachaguliwe ili wapatikane watu wenye uwezo, ili matakwa ya kazi ya kifungu cha 48 ya kusimamia maendeleo ya shehia yaweze kupatikana.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu pia umeeleza mambo mengi ya kuhusu fedha lakini nimekosa kuona maeneo ambayo juu ya akaunti ya mabaraza mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, naomba kifungu hiki cha akaunti ziongezwe kwamba mabaraza yote iwe ni matakwa ya sheria kufungua akaunti kwa mabaraza yao. Hivi ilivyo Mhe. Mwenyekiti, siajabu kuja kuambiwa kwamba akaunti ya Baraza fulani imeingia kwenye akaunti ya fulani. Kwa hivyo mbali

tu ya kukaguliwa na CAG na ripoti za fedha kupelekwa Serikalini Mhe. Mwenyekiti, naomba kwamba sheria iseme wazi kwamba lazima Mabaraza haya yafungue akaunti, ili fedha za umma katika mabaraza husika basi ziende kwenye akaunti maalum ili ziweze kuwa salama na kusimamiwa na watu husika.

Mhe. Mwenyekiti, mambo ya jumla ambayo napenda niyaseme ningeshauri sana Mhe. Waziri akazingatia umuhimu wa Wabunge wetu na Wawakilishi kuwa wajumbe wa Mabaraza husika. Mhe. Mwenyekiti, hili si ajabu wala sio kikwazo, wenzetu Tanzania Bara hapo Wabunge ni wajumbe wa Halmashauri wanaoanisha mipango ya Serikali ndani ya Bunge, wanaangalia maendeleo ya Halmashauri zao hatimaye ushauriano wa mabaraza haya yanakuwa na ufanisi.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, na Zanzibar naomba tuanzie hapo, Wabunge wetu na Wawakilishi wetu waungane na madiwani kama sehemu ya wajumbe wa mabaraza ya Halmashauri, Mabaraza ya Miji na Manispaa ili waweze kutoa mchango wa maendeleo kwenye maeneo yetu muhimu haya haya.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile nishauri kwamba mswada huu pia umeeleza maslahi ya Meya lakini maslahi ya Mwenyekiti sikufurahi nayo. Mhe. Mwenyekiti...

**Mhe. Mwenyekiti:** Umebakia na dakika tano ya ziada.

Mhe. Mwenyekiti, nashauri kwamba ni kweli Meya wetu apewe maslahi mazuri na katika hili Mhe. Mwenyekiti, lazima Kanuni ya Upangaji Matumizi ya Fedha izingatie vyeo vya Meya wetu. Mabaraza haya Mhe. Mwenyekiti lazima yazingatie uwezo unaostahiki kwa Meya wetu ili kuwa na maslahi mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile tuangalie Wenyeviti wetu wa Halmashauri, Mabaraza ya Mji na wao hata kama hawatomfikia Meya kimaslahi, lakini wawe na uwezo kidogo sambamba ili wajenge ari ya kutenda kazi na kusimamia maendeleo ya Mabaraza yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla niseme kwamba mswada huu kama utatekelezwa kwa nia ile ile ambayo Waziri ameieleza na kama kutakuwa hakuna tatizo la kudanganyana na kufanyiwa hadaa basi unaweza kuwagomboa Wazanzibari. Na kwa kuanzia kuwagomboa Wazanzibari Mhe. Mwenyekiti lazima Wakurugenzi wetu waangalie mazingira ambayo hayatasababisha wizi. Huwezi Mkurugenzi (a) ukampa mshahara mkubwa, Mkurugenzi (b) ukampa mshahara mdogo baadae ukamwambia afanye

uadilifu, hatoweza. Kwa hiyo, uteuzi wa Wakurugenzi Mhe. Mwenyekiti, lazima uzingatie maslahi ya Wakurugenzi wetu wote wale ambao Rais amewateua na wale ambao Waziri utawateua maslahi yao yalingane, ili sasa Mabaraza yanapoamua kuwasimamia basi wawe hawana sababu ya kulalamika.

Mhe. Mwenyekiti, leo Wakurugenzi wetu ni aibu kusema mshahara wao, lakini wanalipwa mshahara ambao lazima unamwambia mtu kaibe. Ni mshahara ambao haustahiki, ni mshahara mdogo kwa hiyo Mhe. Waziri hili lizingatie sana na naomba kwa kweli ulifanyie kazi kwa moyo thabiti ili sababu ya uzembe katika Mabaraza yetu, sasa tuweze kuondosha.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa nikwambie tu kwamba mswada huu ukipita usiwe mvivu na Mabaraza basi yapate nguvu ya kupeleka vijana wetu katika kusoma elimu ya masuala haya. Nimetembelea kule Dodoma Chuo cha Serikali za Mitaa kule Hombolo Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari hakuna. Wanafunzi mia tatu unakuta Wazanzibari wawili. Mhe. Mwenyekiti, nadhani uwezeshaji wa Mabaraza haya ndio yatawapa nguvu watu wetu kupata elimu na kujiendeleza katika maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya masuala hayo Mhe. Waziri akikubali hoja zangu nitaunga mkono mswada huu. Ahsante sana.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa fursa hii angalau kuchangia mswada huu wa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wameyazungumza mengi tokea asubuhi na mengi ambayo wameyazungumza ni ya msingi na nadhani Mhe. Waziri kama ambavyo wamemtaja ni msikivu na mengi atayafanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nichukue fursa hii kuwapongeza Mhe. Waziri na watendaji wake, mimi mswada huu naujua na nilianza kufanya nao kazi tokea nilipokuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Na tumefanya kazi kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu kwa muda mrefu tukienda, tukirudi lakini nawapongeza watendaji wa wizara hii kwamba kwa kipindi chote hawakuvunjika moyo. Kila pale ambapo tukijaribu kuwafahamisha na kuwapa maelekezo wamekuwa wakienda wakirudi na kurekebisha yale ambayo yalikuwa yanahitajika na leo hii mswada huu kufikishwa hapa kujadiliwa. Kwa hiyo, nawapongeza sana Mhe. Mwenyekiti kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia baada ya kusoma mswada huu nitambue kwamba ile dhana ambayo imekusudia ya kupeleka mamlaka kwa wananchi

ukisoma vifungu vya sheria hii utaikuta sasa imetimizwa vizuri. Ile *devolution* sasa iliyokuwa imekusudiwa kwa mujibu wa mswada huu sasa imetimizwa kwa kupeleka madaraka haya ya Serikali huko chini huko. Lakini pia kwa kutoa uwezo sasa kwa Serikali hizi za Mitaa kujiimarisha kiuchumi, kimaendeleo na kupanga mipango yao Mhe. Mwenyekiti ya maendeleo.

Sasa ukisoma Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 8 cha mswada huu utaona kwamba ile dhana ya utawala iliyokusudiwa imeoneshwa wazi wazi. Kuna karibu maeneo tisa ambayo mswada huu imeyafafanua na kuyaeleza kwa uzuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia ukisoma kazi ya kila Baraza utatambua kwamba kazi kubwa ambayo imepewa Mabaraza haya ukiacha ile ya kutunga sheria, lakini ni ya kuimarisha uchumi na mapato na maendeleo ya Mabaraza yao M kule wanakotoka. Sasa hii ni moja ya kazi ambayo nadhani na maeneo mengi ambayo Waheshimiwa Wajumbe wamechangia ni hili, na mimi Mhe. Mwenyekiti, naomba kuungana nao kwa kumuomba pia Mhe. Waziri kwamba inabidi na kuna haja ya kuwajengea uwezo hawa Madiwani wetu ambao sasa ndio watatekeleza kazi hii. Kwa sababu bila ya kuwajengea uwezo haya yote ambayo tumewapa kisheria hawatoweza kuyatimiza.

Kwa hiyo, nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba kupitia Mabaraza haya yatakapoundwa upya ni vyema sasa kuweka utaratibu maalum wa kutoa mafunzo kwa hawa Madiwani wetu, ili sasa ile dhana ambayo imekusidiwa ya kutimiza malengo haya iweze kutimia Mhe. Mwenyekiti. Natambua ukitizama *structure* yetu ya sasa hivi ilivyo imekuwa *centralized* mambo yote yako Serikalini huku juu, kwa hiyo huku chini utakuta kuna mapungufu makubwa.

Sasa *of course* wenzetu wengi na ukisoma mifumo ya wenzetu wengi duniani wao wameanza kujijenga huku chini, wamejiimarisha chini vizuri lakini baadae sasa ndio wakaamua kwenda juu kujiunga. Sasa sisi tunaanza juu tunashuka chini, kwa hiyo utakuta kuna hisia hapa kwamba je, kweli Serikali ina azma ya kwenda huko chini. Lakini kama nilivyosema ukisoma masharti ya vifungu vya mswada huu utaona sasa ile dhana ambayo imebebwa ya *devolution*, imetimia moja kwa moja. Kwa hiyo, niungane na mimi na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kuunga mkono hoja hii ya Mhe. Waziri, ili sasa kazi hii ya utekelezaji ianze mara moja.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia wengi wa Wajumbe tokea asubuhi walikuwa wamezungumzia eneo hili na kutoa fursa na uwezo kwa Mhe. Waziri kuteua Madiwani, idadi na wawe wangapi hilo nitamuachia yeye mwenyewe Mhe. Waziri. Lakini mimi nataka kuzungumzia ile dhana kwamba kwa nini Serikali

imekuja na ile dhana ya kutoa uwezo kwa Mhe. Waziri ya kuteua Madiwani kwa idadi ambayo yeye mwenyewe Mhe. Waziri atakubali kwa mujibu wa mapendekezo ya Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti, ukitizama miundo ya Mabaraza yetu haya na ukitizama kazi ambazo zimepewa unapata msingi kwamba unahitaji kuwe na Wajumbe ambao wataingia wenye utaalamu, wenye ujuzi na wenye kutekeleza zile kazi ambazo zimeelezwa kwenye sheria. Sasa kazi ambayo amepewa Mhe. Waziri ya kuteua hawa Wajumbe ni kwa kuzingatia misingi hiyo.

Kwanza kuhakikisha kwamba wale ambao wanawateua wana sifa za vigezo, na ujuzi wa kwenda kusaidia kwenye Mabaraza yale. Inawezekana Mhe. Mwenyekiti ukapata Madiwani wote ambao hawana ujuzi au wengine wanapishana kwenye ujuzi, sasa *of course* utahitaji utaalamu wa uchumi, utahitaji mtaalamu wa sheria, utahitaji mtaalamu wa *local development*. Sasa haya ndio ambayo Mhe. Waziri ameachiwa kwa sheria hii kuweza kuteua watu hao ili sasa iweze kusaidia zile kazi ambazo Mabaraza haya yamepewa.

Sasa naamini Mhe. Waziri amesikia vizuri kama hii hoja ya Wajumbe, kama huu uwezo aliopewa nadhani na yeye atautekeleza vizuri kwa kuteua wale Wajumbe ambao wana sifa hizi ambazo zitakidhi haja ya wao kuteuliwa kama ni Wajumbe Mhe. Mwenyekiti.

Jengine ni hili la kuleta huu mswada wa dharura na kama Mhe. Waziri alivyosema alipowasilisha hoja hii kwanza ni kutimiza masharti ya kifungu cha 80 cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, kwamba Kanuni za Baraza zinatoa uwezo kwa Mhe. Waziri kwa kuleta mswada wa dharura pale ambapo ataona kuna haja ya kufanya hivyo. Lakini sababu yake nini?

Mhe. Mwenyekiti, kwanza utakapokuwa tayari na sheria hii inabidi sasa utenge bajeti maalum ya kuweza sasa kuzisaidia hizi Serikali za Mitaa, na kama tunavyojua siku hizi matayarisho ya bajeti yanaanza mapema. Utaratibu tuliouzoea wa kuanza *June* mpaka mwisho wa *July* au *early Augost*, lakini sasa hivi utaratibu na ambao ulianza mwaka jana ni wa kuanza Baraza hili la Bajeti katika mwezi wa *Mei*. Sasa ukileta hii miswada kuisoma mara ya kwanza, mara ya pili na ule muda ambao unatumia inawezekana dhahiri kwamba usitoe fursa nzuri kwa Wizara ya Fedha kujipanga na kuweza kutenga bajeti maalum inayohitajika katika kutekeleza hizi kazi za Serikali ya Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, pili ni kwamba kwa kupitishwa sheria hii *of course* inaweza kutoa fursa kwa zile sheria nyingine sasa nazo kuzitizama na kuweza kufanya mabadiliko, ili sasa yaendane na matakwa ya sheria hii. Wajumbe

wengi asubuhi hapa wamezungumzia kugongana kwa baadhi ya sheria za Manispaa na Mji Mkongwe, sheria ya utalii na sheria nyingi nyinginezo, tumekuwa kukipokea haya malalamiko ya kwamba taasisi moja na nyingine zinapokea na kukusanya kodi hizo hizo. Sasa kupita kwa sheria hii Mhe. Mwenyekiti, sasa kutaanzisha kazi ya kuzifanyia kazi zile sheria nyingine, ili sasa ziendane na matakwa ya sheria Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, pia niwapongeze Kamati kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Nadhani Kamati yangu hii ya Katiba na Sheria imefanya kazi nzuri sana na mengi ambayo wameyapendekeza Waheshimiwa Wajumbe yalishafanyiwa kazi na Kamati hii. Sasa mimi niwaombe sana Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kwamba tupitishe hoja hii ya Mhe. Waziri, ili sasa tumpe uwezo wa kwenda kuwapa nguvu huko *local government* kama ambavyo Baraza hili kwa muda mrefu lilikuwa likisisitiza. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, kwa wale ambao wako nje naomba sasa warejee ndani, ili waweze kusikia zile hoja zao ambazo walikuwa wanahitaji kupata ufafanuzi. Mhe. Waziri tafadhali.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, kwa mara nyingine tena kunipa fursa ya kuja hapa na kuweza kutoa ufafanuzi kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutokana michango ambayo wameweza kuitoa kuchangia mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu wote kwa kushiriki katika mjadala huu wa kuchangia Mswada wa Kufuta Sheria mbali mbali na Kuweka Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2014.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe waliopata kuchangia mswada huu ni 16 jumla yao, na naomba niwataje;

1. Mhe. Ussi Jecha Simai, mwakilishi wa wananchi Jimbo la Chaani ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala;
2. Mhe. Ali Salim Haji, mwakilishi wa wananchi jimbo la Kwahani;
3. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, mwakilishi wa wananchi Jimbo la Kitope;
4. Mhe. Salma Mohammed Ali, viti maalum;
5. Mhe. Farida Mohammed, viti maalum;

6. Mhe. Fatma Mbarouk Said, mwakilishi wa wananchi Jimbo la Amani;
7. Mhe. Marina Joel Thomas, mteule wa Mhe. Rais;
8. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman, viti maalum;
9. Mhe. Abdallah Mohammed Ali, mwakilishi wa wananchi Jimbo la Mkoani;
10. Mhe. Asha Bakari Makame, viti maalum ambaye pia ni Mwenyekiti wa wake zetu wa Jumuiya ya Wanawake wa CCM kwa hapa Zanzibar;
11. Mhe. Saleh Nassor Juma, mwakilishi wa wananchi Jimbo la Wawi;
12. Mhe. Hamad Masoud Hamad, mwakilishi wa wananchi Jimbo la Ole;
13. Mhe. Salmin Awadh Salmin, mwakilishi wa wananchi Jimbo la Magomeni na mnadhimu wetu Mkuu kwa upande wa Chama cha Mapinduzi;
14. Mhe. Hija Hassan Hija, mwakilishi wa wananchi Jimbo la Kiwani, mdogo wangu;
15. Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa, huyu alichangia kwa maandishi, mwakilishi wa wananchi Jimbo la Kikwajuni; na
16. Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar ndugu yangu Said Hassan.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niishukuru sana Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kwa mchango wao mzuri sana ambao waliutoa kwenye Kamati na kwa yale marekebisho ambayo waliyafanya wakishirikiana na baadhi ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, ukiacha wale waliodharurika wamenisaidia sana katika kuiweka vizuri sheria hii na kufanya mabadiliko na marekebisho ya msingi kabisa, ambayo yataifanya sheria hii iweze kutumika vizuri. Umahiri wao, ujasiri wao na ushauri wao umenisaidia sana katika kupata marekebisho yanayohusiana na sheria hii na mimi nathamini marekebisho hayo na sisi kama Wizara na Serikali tumeyazingatia na yote yale tuliyoyafanya kama ni marekebisho kwenye Kamati basi yatakuwa ni sehemu ya mswada huu. Ijapokuwa baadhi ya Wajumbe wamesema hawajapokea yale marekebisho lakini yale marekebisho yaligaiwa toka jana na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi na ni imani yangu kwamba Waheshimiwa watajiridhisha kwa yale marekebisho na sisi tumeridhika nayo.

Mhe. Mwenyekiti, nitatoa ufafanuzi kwa Wajumbe kwa mambo ya jumla, sitasema mtu fulani kasema nini lakini mchango mwingi uliotolewa na Waheshimiwa Wajumbe ulikuwa unafanana. Kwa hiyo, nitatoa ufafanuzi kwa mujibu wa michango ilivyokuwa inatolewa na ikibidi nitaweza kutoa ufafanuzi kwa yale maeneo mengineyo. Mimi nimeyaita mengineyo kwamba hili pengine atakuwa kalizungumza mtu mmoja wengine hawakuyazungumza.

Lakini yako mambo ya jumla ambayo yamezungumzwa, mimi hayo ndio nitakayoyatolea ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, la kwanza na naomba nisije kwa mtiririko ule ulivyotoka lakini nijibu zile hoja zenyewe au nitoe ufafanuzi kuhusu zile hoja zenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza ilikuwa hoja inaulizwa ni kwa nini mswada huu umewasilishwa kwa hati ya dharura? Mwanasheria Mkuu ameeleza kwa urefu kwa nini mswada huu umewasilishwa kwa hati ya dharura. Kwa mujibu wa Kanuni zetu za Baraza la Wawakilishi kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu kabla sijauwasilisha mswada huu nilisoma hati ya Mhe. Rais ambayo ameiandika kwa madhumuni ya utekelezaji wa kifungu cha 80 cha Kanuni ya Baraza la Wawakilishi kama alivyoeleza Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Halikadhalika Waheshimiwa Wajumbe kama mtakumbuka wakati nikihitimisha mjadala wa bajeti katika Kikao cha Bajeti cha mwaka 2014/2015, mlihimiza sana sheria hizi na mimi nikaliomba Baraza hili chini ya usimamizi wa Mhe. Spika, kwamba tutajitahidi kipindi cha mwaka huu wa bajeti tulete miswada hii kwa hati ya dharura. Sasa tujikumbushe huko na hiyo inatokana na nini, kutokana na umuhimu wa miswada hii katika kuwapelekea wananchi mamlaka ya kujipangia maendeleo yao wao wenyewe.

Sasa zile sababu ambazo Mwanasheria Mkuu amezinukuu sitazirejea, lakini tukumbushane kwamba hata Baraza lenyewe lilidai hilo. Pia tukumbuke tu kwamba, kabla ya sheria hizi vile vile mlihimiza suala la sera na sera hii hapa tayari baada ya kupitisha sera, maana yake kinachofuata sasa ni kuitafsiri sera kwenye sheria hii.

Suala la pili lilikuwa ni uwezo wa waziri kuteuwa Wajumbe kumi (10) katika Baraza la Jiji na Mabaraza mengine. Kwanza nataka niseme kwamba nimesikiliza kwa makini sana maoni ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na mimi na wenzangu wizarani ni wasikivu tena wasikivu sana. Kwa hiyo, baada ya kuyasikiliza maoni ya Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba nataka niseme kwa mujibu wa kifungu cha Mswada huu cha 18, 20, 22 na 24 pametajwa aina ya Mabaraza. Kuna Baraza la Jiji, kuna Baraza la Manispaa, kuna Baraza la Mji na kuna Baraza la Halmashauri. Wajumbe wake wanapatikana vipi? Vigezo vya Jiji ni nini?

Vigezo vya Jiji kuwe na Manispaa zisizopungua mbili kwa hiyo zinaweza zikawa tatu, zinaweza zikawa nne inategemea ukubwa wa jiji lenyewe. Lakini tukianza na hicho kigezo cha mwanzo cha kuwa na Manispaa zisizopungua mbili, kila manispaa inatakiwa iwe na Wajumbe wa kuchaguliwa wasiopungua 15 kwa maana kila Manispaa inatakiwa iwe na Wadi

zisizopungua 15. Kwa maana hiyo, katika ngazi ya jiji kutakuwa na Manispaa mbili kwa mfano, kwa hiyo kukiwa na Manispaa mbili kwa kuanzia maana yake kutakuwa na Wajumbe wa kuchaguliwa 30 kwenye hizi Manispaa mbili.

Sasa katika wale Wajumbe 30 yaani 15 katika kila Manispaa wakishachaguliwa Wajumbe 15 kutoka kwenye Wadi ni wale Wajumbe 15 watakaochaguana miongoni mwao kutoa Wajumbe 10 kuja kwenye jiji. Kwa hiyo, kila Manispaa itatoa Madiwani 10 kuunda jiji. Ukishapata hao Wajumbe 20 sasa wa Baraza la Jiji, waziri amepewa mamlaka ya kuteuwa Wajumbe watano. Kwa hiyo, jiji litakuwa na Wajumbe 25 na hawawezi kuwa wao ndio wenye maamuzi ya wale Wajumbe 20 ambao watatoka kwenye Mabaraza yale ya Manispaa kuunda Baraza la Jiji.

Katika Baraza la Manispaa kutakuwa na Wajumbe 15 wa kuchaguliwa yaani Wadi zisizopungua 15 zinaweza zikazidi, lakini kwa kuanzia angalau 15, hivyo hivyo katika Baraza la Mji, na hivyo hivyo katika Halmashauri ya Wilaya.

Kwa hiyo, miongoni mwa hao 15 wa kuchaguliwa katika kila Baraza sasa hapa nimeamua kusikia kilio cha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi badala ya kuteuwa 10 nitateuwa Wajumbe wasiozidi asilimia 50 ya wale Wajumbe ambao wametoka kwenye Wadi. Kwa hiyo, tutegemee kwamba katika Wajumbe 15 naweza nikateuwa Wajumbe saba na hawa Wajumbe saba nitakaowateuwa watazingatia hivyo vigezo kwamba wawe na sifa mbali mbali ambazo za busara, lakini na uhalisia itabidi niufanye kwa mujibu wa sheria hii na Kanuni ambazo nitazitunga baadae za sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo hili nimekubali kusikia kilio cha Waheshimiwa na kwamba sasa nitateuwa asilimia isiyozidi 50 ya Wajumbe hao. Katika hao nitakaowateuwa asilimia 40 itakuwa ni wanawake. Kwa nini tumefanya hivi, tungeweza kwenda kama Wajumbe wengine walivyopendekeza twende kwenye 50, 50, lakini Katiba yetu bado inazungumzia asilimia 40. Kwa hiyo, lazima tufuate masharti ya Katiba ya Zanzibar. Sasa Katiba utakapokuja kuirekebisha ikiwa na masharti ya asilimia 50 inakuwa rahisi sasa kuja kufanya marekebisho kuongeza idadi ya asilimia ya wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo limezungumzwa sana na Wajumbe ni kuhusu suala la uteuzi wa Wakurugenzi kwamba baadhi yao wanateuliwa na Mhe. Rais na baadhi yao wanateuliwa na waziri. Nataka niseme kwamba, Wakurugenzi wa Jiji watateuliwa na Rais, Wakurugenzi wa Baraza la Manispaa watateuliwa na Rais, Wakurugenzi wa Baraza la Mji na Halmashauri watateuliwa na waziri. Huu mfumo sio mgeni kwa hivi sasa, tuna ngazi ya Baraza la Manispaa Mkurugenzi anateuliwa na Rais,

tutakapokwenda kwenye ngazi ya juu ya jiji bado heshima hii inabaki kwa Mhe. Rais. Lakini kwa *practice* iliyopo sasa Makatibu wa Mabaraza ya Miji anateuwa waziri na Makatibu wa Halmashauri anateuwa waziri.

Kwa hiyo, tunaendelea na *practice* hii kutokana na *standard* ya vile vyombo vyenyewe. Kwa hiyo, naomba Wajumbe waendelee kuamini kwamba huu uteuzi unafanyika katika *category* hizo ambazo tumezitaja, zile mbili anateuwa Rais na zile mbili nateuwa mimi. Hii inatokana na uwezo na majukumu ya zile taasisi ambazo tunazianzisha, huko usoni tutakapokuja kuona kwamba tushafikia *standard* sasa hata haya Mabaraza ya Halmashauri na Mabaraza ya Mji nao wateuliwe na Rais au tunaweza tukaja tukaamua vyenginevyo, hilo ni suala la baadae. Lakini kwa hivi sasa tungeomba tubaki na utaratibu huu ambao tumeuainisha kwenye sheria yetu hii. Hii inatokana na hadhi ya taasisi hizo na pia kumsaidia Mhe. Rais kuteuwa baadhi ya majukumu.

Suala la nne lilikuwa ni malipo ya mishahara na maposho kwa Waheshimiwa Madiwani, hii ndiyo ilikuwa hoja. Kama tulivyosema kwenye kamati hili jambo limefanyiwa marekebisho, tunajua kwamba kilio chetu na kilio cha Madiwani na pengine katika kilio hicho na mimi nilikuwemo kuwaombea kwamba wapate maslahi Waheshimiwa Madiwani wetu.

Nakiri kwamba malipo ya mshahara kwa Waheshimiwa Madiwani imeingia kimakosa katika sheria hii, Madiwani watalipwa posho kutokana na kwamba wao si watendaji wa kudumu. Hivyo watalipwa posho na marupurupu mbali mbali kulingana na hali ya mapato ya taasisi husika na hii Ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija umeizungumza sana, umeimalizia kwa kusema lakini Waheshimiwa Wajumbe wengi wamesema.

Mhe. Hija Hassan Hija wewe katika kuichangia hii umetoa mfano wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B'. Utaratibu wetu wa hivi sasa kuna posho ambayo wanalipwa kwenye vikao nisingependa kuitaja hapa, lakini kuna marupurupu ambayo wanalipwa kila mwezi. Nataka niseme katika Baraza la Manispaa na Halmashauri zote za Unguja na Pemba utaratibu huu tumeuweka baada ya kusikia kilio cha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Waheshimiwa Madiwani wenyewe baada ya kuonana nao mimi mwenyewe, kwamba tunawalipa posho za vikao. Tunawalipa marupurupu ya kujikimu kwa mwezi na tunalipa stahiki nyengine inategemeana na hali ya Halmashauri.

Kwa hiyo, nataka nikubaliane na Mhe. Hija Hassan Hija kwamba anayefanya vizuri ni vizuri kumuangalia, tumefanya hivyo si kwa utashi tu, baada ya kuzipitia Halmashauri na tukawapa vigezo vya kuongeza viwango vya

makusanyo yao na baada ya kuona kwamba viwango hivyo wamevifikia basi tumeamua kuwatengenezea na wao maslahi yao.

Lengo la serikali kufanya *devolution* kwa maana ya kukasimu madaraka kupeleka kwenye Halmashauri, huko mbele kuna hoja nitakuja kuizungumza ni kuzipa uwezo Halmashauri kifedha ili ziweze kutimiza na yale mambo mengine.

Mhe. Saleh Nassor Juma alisema hapa, kwamba ni aibu kwa Waheshimiwa wetu wanaposafiri nje ya nchi hadhi yao na hali yao. Mimi najua kwamba ziko Halmashauri ambazo zinawashonea mpaka suti Madiwani hivi sasa, tunataka hilo sasa liwe kwa Halmashauri zote ni moja kati ya hizo stahiki nyengine ambazo wanazipata. Lakini wanapokwenda kwenye vikao vyao Halmashauri nyingi wana nguo zao maalum majoho, unajua katika vyombo hivi kama Mabaraza na chombo kama hiki cha Baraza la Wawakilishi kuna mavazi maalum, kuna vazi maalum kwa Madiwani na Meya.

Kwa hiyo, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, Mabaraza mengi yanazo nguo maalum kwa ajili ya kushiriki kwenye vikao vyao na kuweka utambulisho wao pale wanapoalikwa kwenye shughuli mbali mbali za kitaifa, *time* gani Mhe. Diwani anavaa na *time* gani Mstahiki Meya anavaa au Mwenyekiti hili ni suala lao wao wenyewe kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Lakini tunajitahidi na tutaendelea kuimarisha suala hili ili tusiendelee kupata fedheha, tutajaribu kuwapa stahiki mbali mbali ili wanapokwenda nje ya nchi waweze kupata stahiki zao. Wengine unaweza ukawapa stahiki lakini wasishone nguo wakafanya mambo mengine. Kwa hiyo, pia tutaweka utaratibu wa kuweza kuweka sawa.

Meya kuwa na uwezo wa kufanya mawasiliano ya kiofisi na taasisi yoyote. Kwenye sheria yetu katika mjadala wetu tulikubaliana kwamba, kutakuwa na kifungu ndani ya mswada kinachoonesha taratibu za mawasiliano. Kwanza Meya na Madiwani ni watunga sera katika vyombo vyao na ni watu ambao wanafanya maamuzi na maamuzi yao mtu ambaye wanatakiwa wampelekee ni waziri.

Kwa hiyo, kutakuwa na *link* kati ya waziri na Mabaraza ya Madiwani kupitia Meya au Mwenyekiti kwa yale mambo yanayohusu maamuzi ya Mabaraza na yale mambo yanayohusu usimamizi na yale mambo yanayohusu sera na shughuli mbali mbali ambazo zinafanywa na Madiwani. Kwa hiyo, utaratibu huo utawekwa na tutaufafanua zaidi kwenye Kanuni ambazo nitazitunga mimi kama waziri.

Waziri na masuala yanayohusu shughuli za kiutendaji. Mkurugenzi kama mtendaji mkuu atahusika na atawekewa utaraibu mkuu. Hata hii sheria yetu imesema, watu walikuwa na hofu kwamba Mkurugenzi anawajibika kwa Rais. Lakini ukiangalia katika kazi za Mkurugenzi kwenye *category* zote Jiji, Baraza la Manispaa, Baraza la Mji na Baraza la Halmashauri pale kwenye kifungu kidogo cha (a) katika mtiririko Mkurugenzi atawajibika kwa Baraza, Baraza maana yake ni wale Madiwani.

Sasa uwajibikaji mwengine ni ule ambao upo kwa mujibu wa sheria ya utumishi na pengine Katiba inavyoeleza, kwamba anayekuteuwa ndiye unayewajibika kwake. Lakini haiondoshi yale majukumu ya msingi na maamuzi ya msingi ambayo yamewekwa kwa mujibu wa sheria hii ya kuwajibika kwa Baraza la Madiwani. Sasa pale ambapo Mkurugenzi anakwepa kuwajibika kwa Madiwani na kwa sababu tumesema kuna kifungu maalum ambacho kinaweka utaratibu wa mawasiliano kati ya Baraza na waziri, waziri wajibu wao yaani Baraza wajibu wake ni kuniarifu waziri, ili waziri na mimi nichukue hatua ya kumuarifu mteuzi aweze kuchukuwa hatua za nidhamu. Kwa wale ambao nimeteuwa mimi maana yake nitachukuwa hatua za nidhamu kwa sababu watakuwa hawafuati masharti ya Sheria hii.

Lakini hata hivyo indhari ya Waheshimiwa Wajumbe ambayo imetolewa hapa naikubali na nitaizingatia na nitajitahidi sana kwenye Kanuni nitakazotunga kuweka uwazi kwa baadhi ya maeneo kama Waheshimiwa Wajumbe walivyonishauri.

Eneo jengine la 6 Sheha kuwa Mjumbe katika Baraza la Serikali za Mitaa wakati yeye ni sehemu ya Serikali Kuu. Kwa utaratibu wetu sasa Zanzibar ngazi ya chini ya Serikali ni katika ngazi ya Sheha. Kwa hiyo, Sheha kuwa Mwenyekiti, kwa vile Serikali Kuu inagatua madaraka baadhi ya madaraka kwa Serikali za Mitaa, ni vizuri Sheha kuhusishwa katika Mabaraza ya Wadi na Shehia, ili kuweza kuelewa na kusimamia utekelezaji wa shughuli za kiutendaji.

Pia Sheha ndio chanzo cha Utawala kwa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa na atakapokuwa anatekeleza majukumu yake katika chombo hiki, atatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria hizi atafuata miongozo na maelekezo inayotoka kwenye Baraza la Madiwani juu ya mipango na mambo mengine yote, na atakapokuwa kwenye Sekta nyengine ya Serikali za Mitaa kule sasa atafata ile Sheria ya Serikali za Mitaa.

Kwa madhumuni ya Sheria hii atafuata Sheria hii na yeye atakuwa Mwenyekiti na wale Wajumbe wa lile Baraza kama nilivyosema watakuwa ni Wajumbe ambao wanatokana na wananchi wenyewe na hata wale wataalamu

nimeulizwa hapa wataalamu wenyewe ni wepi. Tutazingatia zaidi ule ugatuzi katika jaduweli la 3 ambapo kuna mambo karibu 81 hayo ndiyo tutakayoanza kuyapeleka kwenye mamlaka ya Mabaraza ya Miji, Mabaraza ya Manispaa na Mabaraza ya Halmashauri.

Kwa hiyo, tutajitahidi kuona Wataalamu wa Sekta zile wanaoishi katika maeneo yale ndio wanakuwa wataalamu katika Mabaraza ya Shehia na Baraza la Wadi. Kwa hiyo, kwa sababu hatujawa na utaratibu wa kuwa na viongozi wa kuchaguliwa katika ngazi ya chini ya Shehia tumesema huyu anaweza akafanya kazi hizo kama Mwenyekiti na pahala pengine mkisoma hii Sheria mtaona kwamba yeye akeshatoka na maoni ya wananchi kwa sababu maoni haya yanapatikana vipi. Yanapatikana kwenye ile Kamati lakini pia atakuwa na uwezo wa kuitisha mikutano ya hadhara kuzungumzia maendeleo ya wananchi wa Shehia ile, na wakeshakuyapata yale mambo sasa wao wanayachukuwa wanayapeleka kwenye Baraza la Wadi.

Wanapokwenda kwenye Baraza la Wadi Mwenyekiti pale ni Diwani sio Sheha na yeye pale kwenye Baraza la Wadi Sheha anakuwa hata haruhusiwi kupiga kura pale, mwenye nguvu ni Diwani anaangalia ile mipango ambayo imeteremshwa kwenye Shehia ndivyo ilivyo halafu Diwani anaichukuwa pale kuipeleka kwenye Baraza la Halmshauri ya Wilaya kwenye Baraza la Mji kwenye Manispaa au kwenye jiji.

Kwa hivyo, nadhani tuaminiane tu kuwa hili jambo najua kwa sababu ya upya wake Wajumbe wengi wamekuwa na khofu lakini Sheha hapa atatekeleza Masharti ya Sheria hii na Kanuni zile ambazo nitazitunga kwa mujibu wa Sheria hii. Hatatekeleza masharti ya Sheria ya Serikali za Mitaa.

Mamlaka ya Kutoza Kodi na kutoa leseni, Wajumbe pia wamelizungumza jambo hili najua upendo wao kwa vyombo hivi wangependa mambo haya yawe wazi wazi. Lakini tunachokusudia hapa ukisoma tena lile jaduweli utakutia kwamba kuna mambo ambayo Mabaraza haya yatakuwa yamepewa mamlaka. Lakini Serikali za Mitaa zinatekeleza majukumu yake kwa kufuata Sheria yake na Sheria nyengine ya Sekta husika za Serikali.

Kwa mfano, kuna Sheria ya Leseni, mwenye Sheria hii ni Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na katika hili nataka nimpongeze sana Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kwa utaratibu mzuri ambao ameuweka na Baraza la Manispaa kwa kushirikiana kuitekeleza ile Sheria ya Leseni. Watakachotakiwa Baraza la Manispaa kufuata muongozo wa Sheria ile katika kutoa leseni ambazo wao watakuwa na mamlaka nazo.

Hivyo hivyo, katika Sheria nyengine zote za nchi za fedha ikumbuke kwamba katika ugatuzi huu wa Madaraka na niseme katika mambo ambayo yako kwenye jaduweli ijapokuwa Mhe. Hamad Masoud amesema hakubaliani na Mswada huu. Lakini kama nilivyosema Mswada huu kuna mambo yasiyopungua 81 kwa kuanzia Serikali Kuu ina kasimu kwa mamlaka ya Mabaraza haya. Kwenye eneo la Fedha na Maendeleo ya Kiuchumi kuna mambo 13 mkisoma jaduweli mtayaona; kwenye Mambo ya Sheria na mambo yasiyohusiana nayo kuna mambo 4 yanakasimiwa hizi Halmashauri na Mabaraza.

Kwenye kazi za Jamii kuna mambo 8 yanakasimiwa. Kwenye Sekta ya Afya kuna 14 yanakasimiwa. Kwenye Elimu kuna mambo 8 yanakasimiwa, kwenye Kilimo, Maliasili na Utajiri wa Wanyama mambo 12 yanakasimiwa kwa vyombo hivi.

Kwenye masuala la Kijamii na Kiutamaduni mambo 13 yanakasimiwa. Kwenye Mambo ya Ulinzi na Usalama wa Jamii mambo 6 yanakasimiwa na kwenye Kazi nyenginezo yanakasimiwa. Jumla yake ni mambo 81 ambayo Serikali imeamuwa kuyakasimu kwenye vyombo hivi vya mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Kwa hiyo, katika kuyatekeleza mambo haya Serikali za Mitaa kazi kubwa ya Serikali Kuu ni Sheria, Sera, Miongozo na mambo mengine. Mambo mengine Serikali itayakasimu yafanywe na hivi vyombo na hizi Taasisi za Mamlaka na hapa ndipo tutakapoweza kukasimu madaraka kwa vyombo hivi. Tusipofanya hivyo nataka nitumie nafasi hii kusema kwamba kwa madhumuni ya jaduweli hili la tatu maana yake Sheria hii haitakaa kwenye makabati.

Serikali tumeamua na lazima tufanye hivyo na ndio maana moja kati ya sababu iliyotufanya tulete Miswada hii kwa hati za dharura kwa sababu tunataka, kama mnakumbuka Waheshimiwa Wajumbe kwamba baada ya mkutano huu tutakuwa na mkutano mwengine wa Januari tayari maandalizi ya Bajeti yatakuwa tayari yameshaanza. Kwa hiyo, tukileta Mswada huu kwenye Kikao chengine maana yake Serikali vile ilivyokusudia haitaweza kufanikiwa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mengineyo niseme kwa haraka haraka kuna suala la kutakiwa kwamba wizara tuwe makini wakati wa kugawa mipaka ya Shehia ili kuepuka changamoto za muingiliano wa mipaka. Nasema jambo hili tumelizingatia na kulichukuwa na tutahakikisha tunakuwa makini, ili muingiliano usitokee.

Sifa za Madiwani nadhani hii ibakie ukiacha wale ambao tutawateuwa kwa utaalam wao. Lakini wale wengine wabakie kwa mujibu wa Katiba yetu ya Zanzibar ilivyo. Uwekaji wa Matuta barabarani liengezwe kama ni jukumu. Nadhani hili jambo kwa sababu Mabaraza haya zaidi njia zao ni zile *Fida Roads*. Kwa hivyo, mimi nadhani hili jukumu bado tungeliacha kwenye Sekta husika, lakini tutaweka kwenye utaratibu wa Kanuni ikibidi tutashauriana na Sekta inayohusika.

Hadhi ya Meya apewe msaidizi naweza kumwita msaidizi au mlinzi. Vyombo hivi havikatazwi vinapoona kwamba kuna haja ya kumpa kiongozi wao msaidizi au mlinzi na kwa sababu vyombo hivi sasa ndani ya Sheria tunaanzisha rasmi Polisi wa Mabaraza, kwa hiyo kuhusu ulinzi hakuna tatizo kumteuwa mmoja ambaye pengine ame-*qualify* vizuri kuwa mlinzi wa Meya au Mwenyekiti, au kumteuwa msaidizi miongoni mwa maafisa wale walioko pale. Kwa hiyo, sisi hatuna matatizo nalo.

Ufungaji na Ukaguzi wa Hesabu umo kwenye Sheria kwamba litakaloanza ni ufungaji kwanza wa hesabu halafu Waheshimiwa wote utafata baadae kwa mujibu wa Sheria za Zanzibar. Mabaraza bado ni Taasisi za Serikali na bado watawajibika kufata Sheria ile ile ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na watafuata Sheria ya Fedha na Manunuzi ya Zanzibar, na kama watafanya hivyo lazima suala la ufungaji wa Hesabu litangulie halafu suala la Ukaguzi lifatie.

Wawakilishi kuingia katika Baraza la Madiwani limezungumzwa na Wajumbe wawili. Lakini Serikali bado inashawishika dhana ile ile ya Wajumbe mlioisema kwa nguvu zote kwamba tusije tukateuwa Wajumbe wengi zaidi kumpa nafasi waziri wakawazidi wale waliochaguliwa na wananchi, bado khofu ipo kwamba unapowateuwa Wawakilishi na Wabunge kuwa Madiwani wanaweza wakawa na nguvu kubwa zaidi kwenye Mabaraza yale kuliko wale Madiwani waliochaguliwa na wananchi, na kwa sababu mipango yao ya maendeleo yote ambayo inakuja kwa sababu kwa utaratibu wa sasa Serikali Kuu Tume ya Mipango itapokea mipango ya Maendeleo ambayo itaanzia kuanzia kwenye zile Kamati za Shehia, Mabaraza ya Wadi, Mabaraza ya Halmashauri, Mabaraza ya Mji, Manispa na Jiji. Yakitoka hapo mipango ile na mambo yote yale yatakwenda kwenye Kamati ya Maendeleo ya Mkoa, na Kamati ya Maendeleo ya Mkoa tupo Wabunge wote wa Mkoa ule, tupo Wawakilishi wote wa Mkoa ule na tupo kwa mujibu wa Sheria ambayo nitaiwakilisha kesho.

Kwa msingi huo bado Serikali tunaona kule tuwaachie Waheshimiwa Madiwani na huku kwenye Mkoa Meya au Mwenyekiti anakuwa Mjumbe kwenye Kamati anawasilisha ule mpango wake, basi huku sisi kama tuna

maoni na michango tutaitoa huku kwenye Kamati ya Maendeleo ya Mkoa kuliko sisi kutaka twende tukawe Madiwani.

Kumetolewa mfano wa Bara; Bara tofauti na kwetu, Bara Wilaya inaweza ikawa na Mbunge mmoja. Lakini kwetu tofauti kwa mfano huku Mjini tuangalie idadi ya Wabunge na Wawakilishi 20 na huku umeshasema kwamba kwenye Baraza la Manispaa kutakuwa na Wadi kwa kuanzia 15. Kwa hiyo, hao ndio watakaokuwa wamechaguliwa. Sasa ukiwachukuwa hawa 20 Mbunge na Muwakilishi ukawapeleka kwenye Baraza la Wadi maana yake unakwenda kuwazidi wale. Kwa hivyo, tumeona sio busara kufanya hilo.

Limezungumzwa suala la mamlaka ya waziri baada ya kupata idhini ya Rais kugawa maeneo tungewashirikisha wenyewe kule. Lakini tuelewe kwamba hizi mamlaka zinashughulikia mambo tofauti na pengine tuondokane na ule utaratibu wa ki- *Monarch*. Lakini tuelewe kwamba katika nchi zinafata utaratibu ule kwa *Monarch* Waziri Mkuu ndio anakuwa kila kitu, kwa mfano Uingereza Bajeti ya Serikali nzima inawasilishwa na Waziri Mkuu ndiye mwenye Wizara, Mawaziri wengine *Secretary of State* na Makatibu ni *Clack* na Meya hafuati utaratibu wetu wa kuchaguliwa kwamba pengine anachaguliwa na Madiwani au Mwenyekiti; anachaguliwa na wananchi wote katika eneo lile.

Sasa mimi nadhani huko tusiende bado tubaki na utaratibu huo muda ukifika tukiona sasa Meya akachaguliwe na wananchi wote basi Sheria inaweza ikatungwa na baadae ikarekebishwa. Lakini kwa sasa tunahisi utaratibu huu wa kumpa mamlaka waziri kufanya hizi kazi zilizoelezwa bado unafaa kuwepo.

Suala la kuzingatia mamlaka kwenda kwa wananchi ndio lengo ndio lengo la *Devolution* la kuweza kupeleka madaraka kwa wananchi wote na kama nilivyosema ukiisoma hii Sheria kwenye jaduweli kuna mambo 81 ambayo Serikali inabidi lazima ifuate utaratibu huu uliopo kwa mujibu wa Sheria tuyapeleke kwa wananchi ndio lengo kuu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri anamaliza kwa hiyo tumstahamilie kidogo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:**...Mhe. Mwenyekiti, yale mengine yote ambayo ameyasema Mhe. Hija Hassan Hija mengine mimi nimeyatolea ufafanuzi.

Mswada huu hauna chembe ya hadaa Mswada huu, tunauleta Serikalini ili tuyatekeleze haya yaliomo ndani ya Sheria. Kwa hiyo, niwatoe wasi wasi

Waheshimiwa Wajumbe msimamizi wa shughuli za Serikali ni Baraza hili Tukufu. Kwa hiyo, Serikali haina chembe ya hadaa ndani ya Mswada huu uliyoyaleta, inayaleta kwa dhati kabisa kwa lengo lile lile la kupeleka au la kusogeza maendeleo kwa wananchi yawe karibu ziadi.

Utaratibu wa kuwajibishwa Mkurgenzi nadhani nimeshayaeleza, suala la Rasilimali limezungumzwa uvunaji au uchimbaji. Mimi nadhani hapa zaidi kwa sababu sisi tunasimamia tutakuwa tunatoza ada kwa hizi shughuli zitakazofanyika. Kwa hivyo lugha gani ya kuweka kama uvunaji wa rasilimali mbali mbali nalo pia linaweza likawa ni tatizo, kwa sababu ukisema mamlaka iwe na uwezo wa uvunaji wa mafuta na gesi asilia.

Mimi tukubali tu kwamba ile *Municipal Service levy* itakayotozwa kutokana na rasilimali hizi, iwe ndio wajibu wa Mabaraza haya ya Manispaa na Halmashauri. Kwa hivyo mimi nidhani kama nilivyosema Kanuni zitawekwa vizuri na haya yote kama nilivyosema sekta husika ndizo zitakazoweka sheria, sera na miongozo ya kuweza kuifanyia kazi.

Na tukubali kwamba utaratibu tulionao sasa utabadilika. Asubuhi nimesikia hapa wakiulizwa waandishi wa habari waliopo Mikoani. Lakini tukishaweka utaratibu huu na sheria nikishakuitangaza kwenye gazeti rasmi, mtu yule sasa Waziri kazi yake ni kutoa miongozo na sheria na sera, anakuwa chini ya mamlaka husika ambayo ipo kule katika Baraza la Manispaa au Baraza la Halmashauri au Baraza la Mji au *City Council.*

Kwa hivyo mimi ninadhani tukubali kwamba kwa sababu ya mazoea tunaweza kidogo tukapata taabu lakini itabidi tusivunjike moyo. Kuwajengea uwezo Madiwani, hiyo kazi tutaifanya lakini vile vile watumishi wetu kuwapeleka kwenye Chuo cha Halmashauri kilichopo Hombolo Dodoma, wameanza kwenda wachache na kadri ya hali ya fedha za Halmashauri tutaweza, hii ni ile tu ambayo ilizoeleka kwamba tunawaajiri wafanyakazi *direct* kutoka kwenye vyuo ambao wamesomea fani mbali mbali. Lakini kwa msisitizo ambao hasa Ndugu yangu pale Mhe. Hija Hassan Hija ameusema wa kuwapeleka Hombolo, hili jambo ni zuri tutalifanya. Kwa sababu mtu anaweza akawa amepata taaluma ya sekta yake lakini kwa madhumuni ya kufanya kwenye Mabaraza haya, basi tutawapeleka ili waende waka-*specialise* kwenye mambo ya Mabaraza na Halmashauri, ili waweze kuwa kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa maoni ambayo ametupa juu ya kuimarisha au kufanya marekebisho ya sheria hii. Kwa hakika pia ninataka vile vile nimshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kazi nzuri ambayo

ameifanya ya kuweza kutoa ufafanuzi wa baadhi ya vifungu mbali mbali, kuhusu utekelezaji wa Mswada na Sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja imetolewa iamuliwe)*

*(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia Mswada huu kifungu baada ya kifungu. Naomba kutoa hoja.

## KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

### Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar ya mwaka 2014

### Sehemu ya Kwanza
### Masharti ya Utangulizi

| | |
|---|---|
| Kifungu 1 | Jina fupi na kuanza kutumika |
| Kifungu 2 | Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake |

### Sehemu ya Pili
### Misingi inayoongoza

| | |
|---|---|
| Kifungu 3 | Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 4 | Eneo na Mamlaka ya Serikali ya Mitaa pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 5 | |

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia kwenye kifungu hichi nilikisoma na ninapenda nikinukuu tena. Kifungu hiki kilisema kwamba "Mamlaka ya Serikali za Mitaa itaendeshwa na watu na itafanya kazi zake kwa kuzingatia matakwa ya watu, kwa kuzingatia na kufuata taratibu

zilizoainishwa katika sheria hii na sheria nyengine yoyote". Pamoja na kifungu chengine lakini nianze na hichi.

Nikasema kwamba ili kuwa sheria hii ni ya watu inajulikana hakuna labda sheria hii inatungiwa wanyama au jambo jengine lolote. Nikasema hapa ingesomeka vizuri na nikasema isomeke hivi, "Mamlaka ya Serikali za Mitaa itaendeshwa na itafanya kazi zake", tuondoe hii watu kwa sababu ninaiona kwenye sheria kuna watu. Sasa nikasema iwe hivyo kwamba itaendeshwa na itafanya kazi zake kwa kuzingatia matakwa ya watu na kufuata taratibu zilizoainishwa katika sheria hii na sheri nyengine yoyote itakayotumika.

**Mhe. Mwenyekiti:** Hoja yake anataka hii watu, watu ipunguzwe. Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, hivyo ndivyo *devolution* ilivyo, lazima utaje watu, tunakusudia watu. Mamlaka tunazipeleka kwa watu. Hazikukusudiwa kwa mambo mengine. Kwa hivyo sijui tatizo lako wewe kutaja hii watu nini.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Mhe. Mwenyekiti, ninasema kwamba hii sheria ni kwa ajili ya watu ili kwamba hii watu imejirejea na kwa sababu kuwa isomeke vizuri, nikasema kwamba hii sheria ni watu tokea hapo hawakutungiwa mbuzi wala ng'ombe. Kwa hivyo mimi nikasema hapa ili isomeke vizuri na hapa kwenye sheria hizi zimekwenda watu, watu hata na kifungu chengine ambacho kwenye sehemu hii hii, kifungu cha 6 vile vile, "Mamlaka ya Serikali ya Mitaa itaongozwa na watu".

Hii vile vile nikasema kwamba iondoke na ili isomeke vizuri vile vile, "Mamlaka ya Serikali ya Mitaa itaongozwa na itatekelezwa kwa mujibu wa matarajio kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa katika sheria hii na sheria nyengine zozote zinazotumika". Ile watu, watu maana yake imetawala humu kwenye hii sheria na tunajua kwamba sheria hizi zimetungiwa watu. Kwa hivyo ili isomeke vizuri nilisema hivyo Mhe. Waziri hakujibu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niliomba kwamba hii sheria, haya maneno ambayo yamejirejea rejea yaweze kusomeka hivi ambavyo nimependekeza.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mjumbe hata mimi nimekuelewa lakini kama ambavyo Mhe. Waziri amesema labda nikusaidia tu, kwa sababu katika kifungu cha 5 (1) inasema, "Mamlaka ya Serikali ya Mitaa itaendeshwa na watu". Hapa watu watakuwa ni waendeshaji, sawa kifungu cha (1) lakini nasaba ya (2) inakuja na itafanya kazi zake kwa kuzingatia matakwa ya watu.

Sasa hapa ni yale mahitaji au matakwa ya watu ndio yanayosababishia kufanyika hivyo. Sasa hata na mimi sijafahamu bado, *logic* yako ni kitu gani katika hili. Kwa sababu ninahisi hii sentesi ipo sawa. Kwa sababu nimejaribu kuiangalia hata hii ya Kiingereza naona ipo hivyo hivyo na inajitosheleza. Sasa sifahamu, labda utusaidie zaidi. *(Makofi)*

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Mhe. Mwenyekiti, hizi sheria huwa na mabadiliko kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri anijibu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri tusaidie.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, utaratibu, mimi sio kwamba ninaogopa swali. Mhe. Fatma siogopi swali ulilouliza na hoja uliyoitoa. Nimekuelekeza namna ya kifungu kinavyosema. Kifungu cha 5 (1) "Mamlaka ya Serikali ya Mitaa itaendeshwa na watu", *management* ni ya watu na itafanya kazi zake kwa kuzingatia matakwa ya watu.

Sasa hapa kila sehemu ina maana yake kwa sababu ni vitu viwili tofauti. Kwa hivyo mimi ninadhani sioni kama kuna tatizo. Sasa ukitaka lazima tuseme zaidi au kimoja tukitoe, mimi ninadhani sisi tumeona ibakie hivi. Sasa kama unataka hivyo, sisi tunaona bado ibakie hivi imeandikika vizuri ikiwa inasema hivi kuliko vyenginevyo.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Mwenyekiti, ili kumfurahisha Mhe. Fatma katika hiki kifungu cha 5, naomba kisomeke hivi, "Mamlaka ya Serikali ya Mitaa itaendeshwa na watu na itafanya kazi zake kwa kuzingatia matakwa yao", ya watu tuitoe hapa. Kwa hivyo, hiyo ita-*refer* hawa watu matakwa yao. Kwa hivyo tuweke matakwa yao kwa kuzingatia na kufuata taratibu zilizoainishwa moja kwa moja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Eeh! unataka kuongeza zaidi Mwanasheria Mkuu.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, *of course* ukisoma kifungu hiki inabidi pia usome sasa na kifungu cha 9 cha Katiba. Kifungu cha 9 (2) (a) ndicho ambacho sasa kinatoa mamlaka ya wananchi kwenda huko na kinasomeka hivi, "Mamlaka ya kuendesha nchi ni ya watu wenyewe ambapo nguvu na uwezo wote wa Serikali kufuatana na Katiba unatokana na wananchi wenyewe". *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Kwa hivyo kimuongozo tunakwendaje.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Kwa hivyo kifungu hiki ninashauri kibakie kama kilivyo, kipo sawa. *(Makofi)*

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu na Mwanasheria Mkuu nimemfahamu vizuri, basi naomba tuendelee.

| | |
|---|---|
| Kifungu 5 | Asili ya Serikali za Mitaa pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 6 | Vyanzo vya Sheria ya Serikali ya Mtaa |
| Kifungu 7 | Malengo ya Mamlaka ya Serikali ya Mtaa |
| Kifungu 8 | Misingi ya utawala wa Serikali ya Mtaa |
| Kifungu 9 | Kukasimu mamlaka ya Serikali ya Mtaa |
| Kifungu 10 | Ngazi ya Serikali za Mtaa |
| Kifungu 11 | |

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia kifungu hichi nilisema sentesi ya 11 (1) kwamba aina ya Mabaraza ya Serikali ya Mtaa yanaweza kuwa kama ifuatavyo; nikasema kwamba badala yanaweza tuseme yatakuwa, kwa sababu hivi ndivyo ninavyoona lugha ilivyo sahihi. Naomba maelezo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, ninakubaliana na hoja yake.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa tuendelee.

| | |
|---|---|
| Kifungu 11 | Aina ya Mabaraza ya Serikali za Mtaa pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 12 | Utoaji wa mamlaka |

## Sehemu ya Tatu

## Kuanzishwa kwa Mamlaka za Serikali ya Mtaa Pamoja na Mambo Yanayohusiana na hayo

| | |
|---|---|
| Kifungu 13 | Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Serikali ya Mtaa pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 14 | Vigezo vya kuanzisha mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 15 | Yaliyomo katika Amri ya kuanzisha |
| Kifungu 16 | Utaratibu wa kuanzisha mamlaka za mtaa pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 17 | Hati ya uanzishwaji |

## Sehemu ya Nne

## Muundo, Kazi na Uwezo wa Serikali za Mtaa

Kifungu 18

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Mhe. Mwenyekiti, wakati ninachangia kifungu hiki cha 18 (2) (e) Madiwani wanaoteuliwa wote watakaoteuliwa wasiozidi watano watateuliwa na Mhe. Waziri, wawili miongoni mwao angalau wawe wanawake.

Mimi nilizungumza sio hapa tu kila panapo uteuzi wa Mhe. Waziri nikasema tuweke sifa, nikanukuu hata sheria ya sasa hivi. Pia imetaja sifa ya Madiwani watakaoteuliwa. Ninashukuru wakati Mhe. Mwanasheria Mkuu anajaribu kutoa ufafanuzi hili alilizungumzia namna ya sifa ya Madiwani, akasema imani kwamba Mhe. Waziri atalizingatia. Mimi nilitaka liwekwe ndani ya sheria, suala la kuzingatia linanikosesha imani kwa sababu za msingi.

Mhe. Mwenyekiti, vipindi viwili mimi nilikuwa Diwani, kipindi cha tatu ndio hiki nimeondoka. Mhe. Mwenyekiti, katika vipindi vyote pamoja na kwamba sheria imetamka kwamba Madiwani wanakuwa na sifa maalum, kunakuwa kuna mchumi, *engineer* pamoja na mtu wa mipango kama sikosei. Lakini vipindi vyote viwili ambavyo mimi nimekaa Diwani Mhe. Waziri hakuitekeleza sheria na tulikuwa hatuna mahali pa kuweza kumbana. Leo tunaye Mhe. Waziri Mhe. Omar Haji Kheri, tunamjua uadilifu wake anaweza kuteuwa watu kutokana na sifa ambazo yeye anahisi zinaweza kusaidia Mabaraza, lakini kesho kaja mwengine ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, kukosa watu wenye sifa katika vyombo hivi, vimepelekea Mabaraza kutokuwa na uwezo wa kufanya kazi zake ipasavyo hata kutengeneza mikataba iliyokuwa haipo makini na kushitakiwa katika Mahakama. Mhe. Mwenyekiti, ninataka ufafanuzi zaidi.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:**Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Ali Salum Haji alisema hivyo na Mhe. Mwanasheria Mkuu alipokuwa akichangia amesema hivyo, na mimi nilivyokuwa nikifanya majumuisho nimesema hivyo.

Lakini sasa ukishaweka sifa za elimu kwa hawa watano tu ambao ninaowateuwa mimi, lakini wale wengine ni kusoma na kuandika, hatuoni hapo tutakuwa *bias*. Lakini mimi au waziri mwenye mamlaka hii ni lazima ayazingatie haya kwa sababu ya hali ile ambayo itakuwepo, kama kuna wataalamu ambao tunawahitaji, tunahisi katika Baraza la Madiwani hawamo.

Tunaweza tukaweka mtu mwenye fani ya uchumi. Lakini katika waliochaguliwa kukawa na watu watatu wenye fani ya uchumi.

Kwa hivyo, tuaminiane tu kwamba wanaweza waliochaguliwa wakawemo watatu wa uchumi, akawemo mmoja wa afya, lakini ukawa kuna fani ambayo huna, kwa hivyo, ni lazima uzingatie zile fani ambazo huna ndani ya kile chombo.

Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Ali Salum atukubalie tu kwamba sisi tutahakikisha kwamba tunazingatia hilo na kwenye Kanuni kama ilivyosema sheria hii tutazingatia hayo. Ahsante sana.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu Mhe. Waziri, mimi sina *objection* na nimesema mimi ni mdau wa Baraza la Manispaa kwa muda wa miaka 10, nina-*gain* uzoefu. Nasema awamu zote mbili tulipata mchumi mmoja tu katika mwaka 2000, kama sikosei Mhe. Mwalimu Haji Ameir. Kutoka tangu miaka hiyo mpaka sasa hivi hakuna sifa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Naomba uende kwenye hoja Mheshimiwa.

**Mhe. Ali Salum Haji**: Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, ndiyo nakuja katika huo wasi wasi. Sasa ningeomba Mhe. Waziri labda tuweke hivi, kama atanifahamu vizuri. Ningeomba kutokana na maelezo ya Mhe. Waziri kwamba inawezekana tukaweka sifa za watu ambao wanahitaji kuteuliwa, lakini sifa hizo Mhe. Diwani wakaingia nazo, basi angalau tuweke katika hii sheria katika huu mswada. Basi kwamba atateuwa kutokana na mahitaji ya mapungufu ya sifa zinazohitajika.

Lakini lazima hiki kitu angalau kiwepo, kuliko kuiwacha wazi. Watafute angalau kitu kwamba Mhe. Waziri atateuwa kutokana na mapungufu au kutokana na mahitaji ya taasisi pale ambapo panahitajika. Lakini hicho kitu angalau kinampa uzito katika ule uteuzi wake. Vyenginevyo hali itakuwa kama hii ya sasa hivi Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ**: Sina tatizo nitaliweka tu vizuri.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 18, naomba hoja yangu niitowe moja kwa moja, 18, 20, 22, na 24 kabisa kwa vile ni hoja zinazofanana kuhusu uteuzi wa Madiwani.

Mhe. Mwenyekiti, nilijenga hoja hapa kwa Mhe. Waziri kwamba vifungu hivyo 18(1)(e), 21(d), 22(1)(d), 24(1)(d) kwamba Mhe. Waziri alitaja nambari za Madiwani, nashukuru sana kwamba amekubali kuonesha nambari. Lakini amesema sasa badala ya nambari atawateuwa Madiwani hawa kwa asilimia isiyopungua 50, inaweza kuwa 65, 99, mpaka 100 haipungui 50. Hii hesabu ni *wrong*.

Sasa namuomba Mhe. Waziri akubaliane na mimi kwamba hii asilimia iwe 40 tu, kwa sababu kama haipungui 50 maana yake unaweza ukenda mpaka 100, jambo ambalo ni ile ile ni kutoa huku ukatia huku. Kwa hivyo, namuomba iwe asilimia 40.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ**: Mhe. Mwenyekiti, kwanza asilimia isiyozidi 50, siyo isiyopungua, isiyozidi 50 na msingi wake wa hapa nilisema kwamba kwa kule kwenye Jiji inabakia na tano, kwenye Mabaraza Wadi za kuanzia kigezo cha awali ni 15, lakini zinaweza zikawa Wadi 20, zikawa 25 inategemea na ukubwa wa Wadi.

Kwa hivyo, kwa mfano kwa hizi Wadi wambazo tunaanza nazo 15 sisi tutawateuwa watu wasiozidi asilimia 50 maana yake ni 7, kile kipande hakiwezi kukatika. Katika hao 7 katika watu 15 maana yake watafanya kuwa na watu 22. Kwa hivyo hawawezi kuzidi wingi wa wale waliochaguliwa na wananchi, msingi wake ni wale waliochaguliwa na wananchi. Katika hao 7 asilimia 40 itakuwa wanawake. Ndiyo nilivyosema, namuomba sana Mhe. Hija Hassan aelewe kwamba Hansard zirekebishwe ziseme hivyo na tutafuata utaratibu huo, ahsante sana.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, asilimia isiyozidi 50 naomba tuendelee.

| | |
|---|---|
| Kifungu 18 | Uanzishwaji na Muundo wa Baraza la Jiji pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 19 | Kazi za Baraza la Jiji pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 20 | Kuanzishwa na Muundo wa Baraza la Manispaa pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 21 | Kazi za Baraza la Manispaa. |
| Kifungu 22 | Muundo wa Baraza la Mji pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 23 | Kazi za Baraza la Mji pamoja na marekebisho yake. |

Kifungu 24 Muundo wa Halmashauri ya Wilaya

**Mhe. Fatma Mohammed Said:** Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia kwenye kifungu hiki nilipousoma Muundo wa Halmashauri ya Wilaya. Unajua Mhe. Mwenyekiti kwa kweli Kiswahili mimi kinanipa shida, na nilipokuwa skuli nilikuwa napata tabu hivyo hivyo, kwa sababu maksi zangu zilikuwa ndogo kwenye Kiswahili kuliko Kiingereza. Kwa hivyo, napata tabu.

Nilisema hapa pafanywe usahihisho wa maneno, kwa sababu inasema kwamba Mwenyekiti ambaye anachaguliwa. Ina maana kwa wakati wetu huu tuliokuwa nao. Kwa hivyo, mimi nikapendekeza isomeke kwamba Mwenyekiti ambaye atachaguliwa miongoni mwa Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya.

Vile vile vifungu vyengine hivyo hivyo nilipendekeza kwamba baada "ana" iwe "ata" na hapa Makamu Mwenyekiti atachaguliwa miongoni mwa Madiwani na kwa sababu Madiwani, sio wa kudumu kama alivyosema Mhe. Waziri, kwa hivyo nilipendekeza hivyo.

Halafu na hapa vile vile na (c) nilisema hivyo hivyo kwamba Madiwani wote watakao chaguliwa na wananchi na wananchi kutoka katika Wadi husika. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hakunijibu hilo na kwa sababu kulikuwa na masahihisho haya ambayo nilisema kwamba Kiingereza, vile vile kina- *tenses* zake, kwa wakati wa sasa na wakati mwengine na akisema kwamba wanachaguliwa na kwa sababu itakuwa hawa sio wa kudumu. Ndiyo nikasema kufanywe masahihisho hayo. Mhe. Waziri hakunijibu hayo.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ**: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Fatma Mohammed, lakini hayo marekebisho yote tumeyafanya tulipokuwa kwenye Kamati tuliyagundua ambayo anayasema.

Tatizo ni kwamba sasa anasoma mswada hasomi na yale marekebisho. Sasa mimi nadhani mtu anapotafuta kumbukumbu achukuwe na yale marekebisho ambayo tumeyafanya kwenye Kamati, maana kuna vitu vyengine vidogo vidogo ambavyo tulikwisha vifanya kwenye Kamati. Kwa hivyo, hayo marekebisho tumeyafanya kwenye Kamati.

**Mhe. Fatma Mohammed Said:** Mhe. Mwenyekiti, lakini hili ni tatizo lao wenyewe, kwa sababu jana tulipewa mswada huu, sijui kama ni wa dharura basi hayo mengine hatukuwahi kuyaona na kama ulivyosemwa kwamba mswada huu ni mkubwa sana.

Kwa hivyo, nikubaliane na waziri na nachukua huo ushauri wake tuendelee.

| | |
|---|---|
| Kifungu 24 | Muundo wa Halmashauri ya Wilaya pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 25 | Kazi za Halmashauri za Wilaya. |
| Kifungu 26 | Kazi za jumla za Mabaraza Serikali za Mitaa pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 27 | Uwezo wa Jumla wa Mabaraza Serikali za Mitaa pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 28 | Mialiko katika Baraza. |
| Kifungu 29 | Kiapo cha Madiwani. |
| Kifungu 30 | Muundo, Muda wa Meya, Naibu Meya, Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti. |
| Kifungu 31 | Nafasi ya Wazi ya Afisa Meya pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 32 | Kazi na Uwezo wa Meya. |
| Kifungu 33 | Kazi na Uwezo wa Mwenyekiti. |
| Kifungu 34 | Kuondoshwa kwa Meya na Mwenyekiti pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 35 | Utaratibu wa kumuondoa Meya au Mwenyekiti pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 36 | Kujiuzulu kwa Mjumbe. |
| Kifungu 37 | Maslahi na posho za Meya pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 38 | Kazi na Uwezo wa Meya. |

**Mhe. Ali Salum Haji:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Wakati nilipokuwa nachangia kifungu hiki ndani ya mswada nilinukuu kama ilivyo, baada kufika hapa sijaona marekebisho na nikapata faraja na nilishukuru kwamba zile mbio za Madiwani kuja katika nafasi zetu kutunyang'anya huku angalau

zitapungua. Lakini kumbe katika marekebisho neno "mshahara" limeondoka linafutwa na limewekwa neno "posho".

Sasa mimi nataka Mhe. Waziri atusaidie, kwa sababu bado naona ile kadhia kwa Madiwani bado itakuwepo na ule unyonge bado hautoondoka, kwa sababu posho ndiyo kitu ambacho kiko sasa hivi na ndiyo kitu ambacho kinaleta mgogoro.

Sasa ninachotaka kusaidiwa kwa Mhe. Waziri, kwa sababu katika ufafanuzi wake yeye, alisema kwamba watakuwa Madiwani wamepewa fursa hiyo kisheria maana yake, kujiongezea maposho kadiri ya mapato yao yatakavyokuwa yanaongezeka.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kutokana na Madiwani kuwa na njaa kali katika utendaji wa kazi na kutafuta namna ya kujiongezea maposho. Natoa mfano wa Manispaa ya Zanzibar, ambayo sasa hivi imefikia kwamba wanabana wafanyakazi, yaani kulikuwa kuna wafanyakazi wa kulipwa kwa siku wale, walifikia pahala wakawaondosha wote wakabakia na waajiriwa na wale walipwaji kwa siku ndio walikuwa wakifanya zile kazi za mitaani, sasa hivi wamebana nafasi za watu wengine.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe twende kwenye hoja moja kwa moja.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Nitakapomfahamisha ndio atakaponifahamu Mhe. Mwenyekiti. Hoja yangu inakuja kwamba sasa hivi mapato yanaongezeka, yanaongezeka kwa sababu ya kuwabana wafanyakazi, yaani wafanyakazi wanakuwa kidogo mitaani. Hivi sasa katika Jimbo langu halina mfanyakazi wa mitaro na nina mitaro karibuni sita, ili mapato yaongezeke.

**Mhe. Mwenyekiti:** Hoja yako.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, nataka Mhe. Waziri anisaidie hili posho namna ya kuliongeza kwa Madiwani watatumia utaratibu gani, kwa sababu pia kuna mashaka ya utofauti wa Halmashauri na Halmashauri. Kwa sababu Manispaa Zanzibar wana uwezo mkubwa wa kubuni miradi na kuongeza mapato. Lakini kuna Halmashauri kama ya Wilaya ya Kati na Halmashauri ya Kaskazini A, mazingira yake kiuchumi na Kijiografia ni magumu. Kwa hivyo, tunategemea wataongeza mapato kwa njia gani.

Pia katika hilo posho anisaidie Mhe. Waziri, kwa sababu pia kuna malalamiko ya baina ya Madiwani wa Mjini na mashamba. Sasa kuweza kuonesha tofauti katika kuongeza hizi posho watatumia utaratibu gani angalau kuwaridhisha

Madiwani, baina ya wa Mjini na wa Mashamba, wakati wa mashamba baadhi maeneo yao hayana uchumi mkubwa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Umefahamika Mhe. Mjumbe. Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ**: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Ali Salum Haji, toka niko pale nilikuwa nikisema kilio cha Madiwani juu ya suala la kulipwa mishahara na mimi nilipoingia katika taasisi hii, nilikuta hicho kilio kwa kukaa mimi mwenyewe na Madiwani.

Lakini nataka nimuhakikishie Mhe. Ali Salum Haji, kwamba hicho anacho hofia yeye ambacho kimewahi kutokea kwa Baraza la Manispaa, sasa hakipo. Serikali imeamua kuchukua mishahara ya watumishi wote wa Baraza la Manispaa, kuwalipa moja kwa moja kwenye *pay roll* ya serikali. Kwa hivyo, hilo ambalo anasema liliwahi kutokea si dhani kama litatokea tena kwa utaratibu huu.

Kwa hivyo, hakuna mfanyakazi wa Baraza la Manispaa ambaye analipwa hivi sasa kutokana na zile fedha ambazo wanakusanya wenyewe. Lakini pia Madiwani watakapoweka utaratibu kwa mujibu wa Kanuni ambazo nitazitunga na zile Kanuni watakazozitunga, wanapopanga na kuidhinisha kwenye vyombo vyao wanaleta kwa waziri, na waziri lazima aone taratibu zote za fedha zinafuatwa na taratibu nyengine za nchi zinafuatwa. Kwa hivyo, hiyo hofu aliyoieleza nadhani itakuwa haipo.

Ama suala la kufanana kwa Mabaraza na Halmashauri za nchi nzima hilo tulitegemee. Kwa sababu Mabaraza na Halmashauri yanatofautiana katika ukusanyaji wao wa mapato kulingana na mazingira ya kiuchumi katika eneo lile. Ninachoweza kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kama nilivyosema pale, kwamba hivi sasa Madiwani wanalipwa maposho ya vikao na stahiki nyengine, lakini na marupurupu wanapewa kwa mwezi kuhakikisha kwamba kila Diwani mwisho wa mwezi anaondoka na kitu cha kuweza kufanyia shughuli zake. Hiki kimewekwa kwa sababu hawa sio wafanyakazi wa muda wote, wana shughuli zao nyengine ambazo wanazifanya.

Sasa hili alilolisema Mhe. Mjumbe ni tabia ya mtu, sasa tabia ya mtu kuiweka kwenye kuidhibiti kwa utaratibu huo tu wa kumlipa mshahara. Kwa hivyo, watuamini kwamba Madiwani sasa hivi tumewatengenezea mazingira mazuri. Lakini kutofautiana kati ya Baraza hili na hili, hilo litaendelea kuwepo na hizo Halmashauri ambazo amezisema ya Kati na ya Kaskazini A, sasa hivi zinakusanya vizuri tofauti na pale mwanzo zilivyokuwa. Halmashauri zote hata zilioko katika maeneo mengine kisiwani Pemba, zinakusanya vizuri na

ndio maana tumefikia pahala kwamba tumeweka utaratibu wa kuwapa marupurupu zaidi ya yale ambayo waliyokuwa wakipewa. Nilisema pale sitaki nizitaje wanapata kiasi gani, hiyo itakuwa ni siri yao, lakini naomba Mhe. Mjumbe aamini kwamba Madiwani sasa hivi tunawajengea mazingira mazuri.

Lakini suala la mshahara kwa sasa hivi halitakuwepo kwa mujibu wa sheria hii, mpaka hapo yale madaraka na mamlaka yatakapokuwa yameshafika vizuri sana na mambo yakibadilika vizuri kiuchumi katika Mabaraza na Halmashauri, basi serikali inaweza ikaja ikafikiria wakati huo, lakini kwa sasa tunahisi utaratibu huu uendelee uliopo hivi sasa.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Waziri wakati aliponipa ufafanuzi na mimi nilitaja hofu moja tu kwamba mwanadamu ndivyo alivyo na maumbile yake, kila mtu huangalia katika lile lake na nikasema kwamba Waheshimiwa Madiwani walijaribu kutafuta njia ya kutaka kuongeza posho, lakini idadi ya wafanyakazi imepungua, pamoja na kwamba hili suala lilichukuliwa serikalini. Lakini bado nataka kusema kwamba maombi ya posho ya Madiwani Mhe. Waziri yataendelea kuja kwako, lakini maombi ya posho yatakuja, lakini bado tufahamu kwamba hilo Baraza lenyewe sasa hivi wanaweza kuongeza posho za Madiwani wakashindwa na kazi za utendaji wao, kwa sababu lazima tukubaliane Mhe. Mwenyekiti. Moja tu Mhe. Waziri anikubalie hilo, kwamba hivi sasa Manispaa wanashindwa kumudu suala la kuzoa taka kutokana na uwezo wao ni mdogo katika mitaa.

Sasa mimi sina tatizo na hilo niseme tu ninachokihitaji kwa Mhe. Waziri kwake yeye na nikimaliza naomba nikae. Ninachohitaji kwake yeye ni kuona namna gani basi ya kuweza kusaidia katika pande zote mbili, katika kuongeza maposho kwa Madiwani lakini na ule ufanisi wa kazi zao pia uendane sambamba, isijekuwa tunaongeza nguvu upande mmoja halafu upande mmoja nguvu inapungua. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 38 Madiwani watakuwa watendaji wa kudumu pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 39

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, mimi nilimsikia vizuri sana Mhe. Waziri kifungu hiki aliposema kuwa tuwachie... *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sijaridhika na kauli ya Mhe. Waziri kwa kusema kuwa hawa waendelee kuteuliwa na Mhe. Waziri, unajua Mhe. Mwenyekiti tukisema Halmashauri ni kubwa sana na inaongoza watu wengi sana. Sasa

tukisema watu hawa bado waendelee kutangazwa na waziri ni kuwashusha hadhi yao, kwa sababu na wao wanaheshma kubwa ya kuweza kutangazwa na waziri.

Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba kifungu hiki kibadilike na kikae waziri asiweze, kwa sababu tunaepusha na mambo mengi hapa kama vile kutokuweka watu kwanza waziri anaweza akachagua mtu wake tu, ambaye atakuwa analegalega. Kutokana na hali hiyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti kibadilike na kibakie Rais ndiye atakayeweza kuwaapisha watu hawa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, sijui udogo wa waziri unapimwa kwa kipimo gani, lakini waziri pia ni mtu mzito maana yeye ndiye anayemsaidia Rais katika ile sekta, mimi ndiye ninayemsaidia Rais kwenye sekta hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sisi tunaona turidhike na tuendelee na utaratibu tuliouainisha kwenye sheria ya kwamba Rais ateue Mkurugenzi wa Jiji na Baraza la Manispaa na waziri aendelee kuteua Wakurugenzi wa Baraza la Mji na Halmashauri na utaratibu huo ndio unaofanyika sasa. Vile vile vigezo au sifa za kuteua Mkurugenzi zimewekwa, yaani zilizomo ndani ya sheria ndizo zitakazomfanya waziri ateue Mkurugenzi wa Halmashauri na Baraza la Mji na sifa hizo hizo zilizowekwa ndizo zitakazomfanya Rais aweze kuwateua wale wengine.

Mhe. Mwenyekiti, hatuteui ashakum simatusi wengine wamesema nisijenikateua mama zangu wadogo na wengine, hapana, isipokuwa nitateua watu kwa mujibu wa sifa zilizotajwa ndani ya Sheria na Sheria ya Utumishi wa Umma na wala sitateua mtu kwa sababu tu ni rafiki yangu hapana.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Mjumbe, najua hana matatizo sana aturuhusu tuendelee na utaratibu huu, tuu-*practice* na tukiona na kwa sababu hivi vyombo vina-*categories*, yaani kuna *standard* ya hivi vyombo na wala sikweli kwamba Baraza la Manispaa linalingana na Halmashauri yangu ya Kaskazini A kwa hivi sasa, lazima kuna mambo yamezidi katika utendaji kwenye Baraza la Manispaa na kule Halmashauri.

Hivyo, ndio maana tumeweka kwenye sheria utaratibu wa kupandisha viwango wa haya Mabaraza, kwamba ukitoa Manispaa uende kwenye Jiji ukotoka Baraza uende kwenye Manispaa na zikifikia Halmashauri zote Mabaraza yote na *standard* yake ni Manispaa, maana yake waziri sasa hapo

atakuwa haruhusiwi kufanya hiyo kazi, lakini kwa sasa tumeweka utaratibu huo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, sina tatizo, lakini nimeshtuka neno Wakurugenzi, kwa sababu Wakurugenzi sio mtu mdogo, hebu tuangalieni jamani na mimi sina tatizo, lakini tatizo hapa tusijetukachekwa, kwa sababu watu wengi huku wamesoma wana-diplomasia pamoja na mambo mengine, wasijewakasema tizameni wale Wawakilishi waziri leo kampa *power* anateua Wakurugenzi ndipo *knowledge* yangu ilipo hapa.

Sasa kama ipo sheria hasa inaonesha waziri anaweza kuteua Wakurugenzi na kuapisha *that is ok*. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

**Mhe. Mwenyekiti:** Tuendelee, Katibu.

Kifungu 39 Uteuzi wa Mkurugenzi.
Kifungu 40

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Salmin Awadh Salmin.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kwa ajili ya kutaka kupata ufafanuzi zaidi pamoja na kwamba Mhe. Waziri amejaribu kutoa ufafanuzi, lakini bado haujatosheleza.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nimezungumzia juu ya wasiwasi wangu kuhusu nafasi ya Mkurugenzi kuwajibika kwa kazi na majukumu yake, ambayo ni ibara 40(2) jambo ambalo bado halijanitosheleza na kutokana na nature ya matatizo yanayojitokeza katika taasisi kama hizi.

Sasa ninahitaji maelezo zaidi, kwa sababu lazima tufike hapana tukumbuke kwamba mabaraza haya sio idara za serikali na wakurugenzi mbali na kwamba wanateuliwa na Rais, kwani Rais kwake ni uteuzi tu, lakini wanatakiwa wawajibike katika vyombo vile. Kwa hiyo, kitendo cha kutokuainisha uwajibikaji wao kwa mabaraza kinaweza kikatuongezea matatizo pamoja na kwamba huko nyuma tumekuwa na matatizo, lakini watatuongezea matatizo.

Kwa maana hiyo, ningeona ili kuondosha matatizo haya kwa Wakurugenzi wanaoteuliwa na Rais na wajue kwamba wanawajibika kwa vyombo vile moja kwa moja, basi iwepo *statement* inayoonesha hivyo, pamoja na kwamba

mtu aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi atalazimika kuwajibika, lakini awajibike kwa Baraza lake, kazi zake pamoja na majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, ibara hii ya 41(1)(a) haitoshelezi kwa sababu hii inazungumzia uwajibikaji wa maamuzi ya *council* ambayo yamepatikana. Lakini kuna mambo ambayo yanaweza yasipelekwe kwenye *council* kwa maamuzi maana yake anaweza kufanya maamuzi yake.

Mhe. Mwenyekiti, *experience* ndogo tu ambayo sisi tuliiona kama nilivyosema kwenye taasisi hii wakati tulipokwenda kuchunguza. Hivyo, tuligundua kwamba wakati bajeti zile za *council* zinavyowasilishwa au ule mpango wa mapato na matumizi unavyooneshwa, basi Wakurugenzi wanapata nafasi ya kutekeleza moja kwa moja yale yaliyopitishwa mule na unapomuuliza atakwambia ni bajeti iliyoonesha, ambapo mfumo wa vyombo kile sivyo ulivyo.

Kwa hiyo, mfumo wa chombo kile au Mabaraza yale hata kama bajeti imeshapitishwa kwa hivyo katika utekelezaji wa mambo yale, yaani mambo yale yanavyotekelezwa ni lazima yapelekwe kwenye kamati zinazohusika na halafu yaidhinishwe na Baraza. Sasa unapotoa *loophole* hii maana yake Wakurugenzi watatekeleza moja kwa moja ile bajeti iliopo bila ya kupitia kwenye kamati zile za kisekta na kuwasilisha kwenye *council* kwa maamuzi.

Kwa hivyo, naomba *statement* ya Mkurugenzi kuwajibika kwa Baraza iwekwe kwenye ibara ya 40(2) kama kutakuwa na kazi zake, lakini atalazimika kuwajibika kwa Baraza lake na katika kazi zake na majukumu yake mengine. Hivyo hii lazima ioneshwe wazi kisheria na sio kwenye kanuni, yaani ionekane wazi kwamba Mkurugenzi anawajibika kwa Baraza lake pamoja na kwamba Rais amemteua, lakini chombo kile ndicho anachowajibika nacho.

Sasa kuondoka hilo tutaongeza matatizo katika taasisi hii. Mhe. Waziri naomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, alizingatie kwenye maandishi yake na ionekane hivyo.

**Mhe. Mwenyekiti:** Sawa tumekufahamu Mhe. Mjumbe. Mhe. Waziri. Mhe. Mwanasheria Mkuu.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, anachosema Mhe. Mwakilishi *of course* ukikisoma tu kifungu hichi kama kilivyo unaweza usipate ile tafsiri ambayo Mhe. Salmin Awadh Salmin amekuwa akiizungumza na hilo la kwanza.

Lakini la pili, ukisoma kifungu cha 41(1)(a) utaona kwamba katika kazi ambazo Mkurugenzi huyo amepewa moja ni hilo kuwajibika katika Baraza ambalo analifanyia kazi, hilo moja.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, madhumuni ya kifungu hiki ni kuhakikisha kwamba yule Mkurugenzi kama afisa *answerable* mkuu, anawajibika katika kufanya zile kazi zake za kila siku maana yake ukiacha hivi hivi unaweza kusema sasa na ukisoma sheria za zamani zile ambazo tumezifuta hukuti kifungu ambacho sasa kinakuwa sharti kwa Mkurugenzi kuwajibika katika kazi zake hizi.

Sasa ndio madhumuni ya kuwepo kwa kifungu hiki Mhe. Mwenyekiti na wala haina maana kama hatowajibika katika lile Baraza lake ambalo analifanyia kazi, yaani atawajibika kote kote.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Salmin Awadh Salmin.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo ambayo Mhe. Mwanasheria Mkuu ameyatoa juu ya kifungu cha 41(1)(a) na mimi nilisema mwanzo tokea mwanzo kimeeleza kwamba atawajibika na utekelezaji wa maamuzi yale yaliyofikiwa kwenye *council*.

Katika utekelezaji kuna mambo ambayo yanafanyika bila ya kuamuliwa katika vyombo vile na utayakuta mambo ambayo yako katika bajeti, yaani anatekeleza moja kwa moja Mkurugenzi na haya ndio matatizo yaliopo na lazima tuyakubali haya.

Kwa kweli, hapa hakuoneshi kifungu kinachoonesha kwamba huyu anawajibika kwa *council* yake hakuna, isipokuwa kinachoonekana hapa ni kwamba yeye atatekeleza kwa yale maamuzi tu, kwa sababu tumempa mamlaka kama ni mkuu wa idara vile ana mamlaka yake mwenyewe.

Kwa hiyo, lazima kuwepo na kifungu kinachoonesha kwamba yeye anawajibika kwa *council* yake lazima kiwepo, yaani lazima kifungu hicho kinachoonesha Mkurugenzi atawajibika kwa Baraza lake kwanza kwa sababu huyu mtu ameteuliwa na Rais.

Sasa anapoteuliwa na Rais maana yake atawajibika kwa Rais, hivyo kiwepo kifungu kwenye sheria ajue kwamba Rais yeye amemteua tu, lakini majukumu pamoja na wajibu wake anawajibika pale kwa Baraza la Madiwani, sasa lazima lioneshe hivi kwa sababu hii sio idara ya serikali.

**Mhe. Mwenyekiti:** Tumekuelewa Mhe. Mjumbe. Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salmin Awadh Salmin anahofu na binadamu kuwa na hofu ni wajibu wake. Lakini kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, kwamba ukikisoma hiki tu peke yake unaweza usipate maana na bado anahofu pia na kile kifungu cha 41(1)(a) kama hakitoshelezi.

Vile vile kuyaondosha maneno mtu aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi atalazimika kuwajibika katika kazi zake na majukumu yake anaona kama hakitoshelezi. Sasa labda mimi nataka niseme tuongeze maneno mtu aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi atalazimika kuwajibika katika kazi na majukumu yake na atawajibika vile vile kwa Baraza.

Kwa hivyo, lugha hapa wanasheria watatusaidia, lakini sasa tukiongeza na maneno haya hivyo haiwezi kuonesha kwamba huyu mtu pamoja na kuwajibika katika zile kazi zake za kila siku, lakini pia katika utekelezaji wa hizo kazi zake za kila siku atawajibika kwa Baraza la Manispaa au *whatever* lolote litakalokuwa. Tukifanya hivyo je, Mhe. Salmin Awadh Salmin haoni kama tunaweza tukawa tumekiweka vizuri. Nadhani tuongeze hayo maneno, ili kukidhi ile hofu ambayo anayo Mhe. Salmin Awadh Salmin.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Salmin Awadh Salmin.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Mhe. Mwenyekiti, kwa hilo ndio nilichokuwa nikisema kwamba lazima kuwe na *statement* inayoonesha hivyo, mbali ya kuwajibika kwa kazi yake na majukumu yake, lakini Mkurugenzi aelewe kwamba anawajibika kwa Baraza lake, ili kuondosha hii migongano iliipo. Kwa hivyo, *whatever* itakavyokuwa maandishi wanasheria lakini hicho kitu lazima kioneshe kwenye sheria. Tuendelee.

**Mhe. Mwenyekiti:** Tuendelee, Katibu.

| | |
|---|---|
| Kifungu 40 | Sfia za kuwa Mkurugenzi pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 41 | Kazi na majukumu ya Mkurugenzi. |
| Kifungu 42 | Kuanzisha na kazi za Baraza la Wadi pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 43 | Muundo wa Baraza la Wadi pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 44 | Mwenyekiti wa Baraza la Wadi. |
| Kifungu 45 | Katibu wa Baraza la Wadi. |
| Kifungu 46 | Ajira na sifa za Karani. |
| Kifungu 47 | Kuanzisha na Muundo wa Kamati ya Ushauri wa Shehia pamoja na marekebisho yake. |

Kifungu 48 Kazi na uwezo wa Kamati ya Ushauri wa Shehia pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 49 Sifa za Wajumbe wa Kamati ya Ushauri wa Shehia pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 50 Kazi za Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Shehia pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 51 Muda wa Mjumbe wa Kamati ya Ushauri wa Shehia pamoja na marekebisho yake.

**Sehemu ya Tano**

**Kamati na Idara za Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Kifungu 52 Kuanzisha Kamati ya Maendeleo ya Mamlaka ya Mitaa.
Kifungu 53 Kazi za Kamati ya Maendeleo ya Mamlaka ya Mitaa.
Kifungu 54 Kamati za Kudumu za Jiji, Manispaa, Baraza la Mji na Halmashauri ya Wilaya.
Kifungu 55 Kazi na uwezo wa Kamati za Kudumu.
Kifungu 56 Mipango ya Maendeleo ya Serikali za Mtaa.
Kifungu 57 Idara za Mamlaka ya Serikali za Mitaa.
Kifungu 58 Kazi za Idara.
Kifungu 59 Majukumu ya Mkuu wa Idara pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 60 Pamoja na marekebiso yake.

**Sehemu ya Sita**

**Wafanyakazi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa**

Kifungu 61 Pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 62 Pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 63 Pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 64 Pamoja na marekebisho yake.

**Sehemu ya Saba**

**Mipango na Masharti ya Fedha**

Kifungu 65 Uunganishaji wa Mipango Shirikishi.
Kifungu 66 Kitengo cha Mipango Fedha, Uchumi na Maendeleo.
Kifungu 67 Kazi na Majukumu ya Kitengo cha Mipango Fedha, Uchumi na Maendeleo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 68 Utekelezaji na Utendaji wa Mpango wa Baraza.
Kifungu 69 Vyanzo vya Fedha vya Mamlaka tya Serikali za Mitaa.

| | |
|---|---|
| Kifungu 70 | Vyanzo vya Mapato ya Mtaa. |
| Kifungu 71 | Michango ya Jamii. |
| Kifungu 72 | Ruzuku pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 73 | Mikopo. |
| Kifungu 74 | Kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Serikali ya Mtaa pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 75 | Mwaka wa Fedha na Bajeti ya Mamlaka. |
| Kifungu 76 | Utekelezaji wa Bajeti ya Baraza pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 77 | Ukaguzi wa Hesabu na Fedha pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 78 | Ukaguzi wa Hesabu ya Mamlaka ya Serikali ya Mtaa. |
| Kifungu 79 | Bajeti ya Muda. |
| Kifungu 80 | Bajeti ya ziada. |

**Sehemu ya Nane**

**Makosa na Masharti ya Hatua za Kisheria**

| | |
|---|---|
| Kifungu 81 | Mwenendo wa Kisheria pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 82 | Makosa na adhabu pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 83 | Kero pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 84 | Matumizi ya Ardhi yasiyoruhusiwa pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 85 | Adhabu za jumla. |

**Sehemu ya Tisa**
**Masharti Mengineyo**

| | |
|---|---|
| Kifungu 86 | Mikutano ya Wazi pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 87 | Ukomo wa Uwajibikaji pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 88 | Uwezo wa Kuvunja Baraza pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 89 | Polisi Wasaidizi ndani ya Mamlaka za Mitaa. |
| Kifungu 90 | Mawasiliano baina ya Serikali Kuu na Baraza pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 91 | Mchango wa Mamlaka ya Mtaa. |
| Kifungu 92 | Utowaji wa Taarifa za Mamlaka. |
| Kifungu 93 | Nyaraka au Notisi inayotolewa pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 94 | Kanunu. |
| Kifungu 95 | Kutufa na Kubakiza. |

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri wa (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

**Mhe. Waziri wa (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imepitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuwahoji wale wanaoafiki wanyooshe mikono, wasioafiki, wanaoafiki wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar ya mwaka 2014**

*(Kusomwa kwa Mara ya Tatu)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri wa (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

**Mhe. Waziri wa (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar wa mwaka 2014 usomwe kwa mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuwahoji wale wanaoafiki wanyooshe mikono, wasioafiki, wanaoafiki wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Mswada wa Sheria wa Serikali ulisomwa kwa mara ya tatu na kupitishwa)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kwa siku ya leo kuja kumaliza kazi yetu hii, ambayo ilikuwa tumejipangia. Sasa kama tulivyokwisha kumsikia Katibu, kwamba shughuli zetu za leo ambazo tulikuwa tumejipangia hapa zimefikia mwisho na muda bado tunao kidogo. Lakini inabidi nichukue fursa hii tuahirishe Baraza hili hadi kesho siku ya Alhamis tarehe 30 saa 3:00 za asubuhi.

*(Saa 1:23 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 30/10/2014 saa 3:00 asubuhi)*